# KISWAHILI

# KIDATO CHA NNE

# STUDY NOTES

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

# KUONGEZA MSAMIATI WA KISWAHILI

## UUNDAJI WA MANENO.

## MANENO

Kwa kawaida hakuna lugha inayojitosheleza kimawasiliano na kimantiki hivyo hakuna lugha iliyo bora kuliko nyingine.

Ili lugha itosheleze mawasiliano inahitaji kuwa na msamiati wa kutosha, msamiati ndio unaowawezesha wazungumzaji wa lugha kujieleza na kubainisha hisia zao kwa wale wanao wasikiliza.

Ili kukamilisha mawasiliano lugha inajikuta ikilazimika kuongeza msamiati wake, na sababu kuu zinazopelekea idadi ya msamiati kuongezeka ni pamoja na: -

- Muingiliano wa kiutamaduni baina ya jamii moja na nyingine kwa mfano, utamaduni wa waingereza umesababisha lugha ya kiswahili kuwa na maneno yafuatayo, gauni, shati n.k
- Aidha maendeleo ya sayansi na teknolojia yamesababisha uvumbuzi wa dhana mbalimbali mpya. Dhana hizo zinalazimika kutajwa na lugha husika mathalani kabla ya uvumbuzi wa simu, television n.k maneno haya hayakuwepo katika lugha.
- Pia jamii kutokana na matukio (misimu) mbalimbali kunasababisha kuibuka kwa dhana mbalimbali mpya ambazo lugha husika hulazimika kuzitafutia msamiati wa kuzitaja mathalani maneno mengi katika lugha ambayo yanaonesha uhusiano wa kijamii yanaibuka katika jamii. Ni ishara inayoonesha tabia ya lugha kuongeza msamiati wake. Mfano wa maneno hayo ni: - kasheshe, changudoa n.k

## NJIA ZA KUONGEZA MSAMIATI

1. **UBADILISHAJI WA VITAMKWA**

Lugha kwa kutumia vitamkwa ambavyo ni fonimu za lugha husika huvibadilisha mpangilio wake na hivyo kufanya uwezekano wa kuunda maneno mengi tofautitofauti mfano:- a,e,i,o,u vitamkwa hivi vinaunda maneno yafuatayo: - au,ua,ita, tai, uta, tua, tia, ute,utu, toi,tui, toa n.k

2. **UNYUMBULISHAJI WA MANENO**

Lugha ina kawaida ya kunyambulisha maneno yake na hivyo kuwa na uwezekano wa kuunda maneno mengi tofauti mfano: - piga, pigo, pigana, piganiana, piganisha, pigishwa, pigeni n.k

3. **UKOPAJI WA MANENO**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Lugha yoyote ina tabia ya kuchukua maneno toka lugha nyingine tofauti na kisha kuyatumia maneno hayo kama yalivyo kutoka lugha halisia. Mfano kiswahili kimekopa maneno toka lugha zifuatazo: -

| LUGHA | MANENO |
|---|---|
| (i) Kireno | Leso, meza n.k |
| (ii) Kijerumani | Shule, ela n.k |
| (iii) Kiingereza | Shati, gauni, skuli |
| (iv) Kiarabu | Sujudu, amini n.k |
| (v) Kifaransa | Sabuni, divai |
| (vi) Kichina | Umma |
| (vii) Kihindi | Chapati, Khanga, Doti, |

Manjumati n.k

4. **KUTOHOA MANENO**

Lugha ina tabia ya kuchukua maneno kutoka lugha nyingine tofauti na kuyatumia kwa namna tofauti kimaana na kimatamshi mfano: -

| LUGHA | NENO |
|---|---|
| (i) Kiingereza (mail) | meli |
| (ii) Kipare | kitivo |
| (iii) Kihaya | ngeli |
| (iv) Kinyakyusa | ugiligili (liquid) |

5. **UBATIZAJI WA MAANA**


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Lugha ina tabia ya kutoa maana mpya katika maneno ambayo tayari yapo. Mfano:- mashabiki wa chama au mchezo huitwa wakereketwa.

6. **UUNGANISHAJI WA MANENO**

Lugha ina tabia ya kuunganisha maneno tofautitofauti na kuunda neno jingine jipya

**(i) Nomina + Nomino**

Kuchwa + maji kuchwamaji

**(ii) Kitenzi + Nomino**

Funga + mlango fungamlango

Ponda + mali pondamali

**(iii) Kitenzi + kitenzi**

Kufa + Kwaja kufakwaja

**CHIMBUKO LA KISWAHILI**

Hakuna ajuae chimbuko la kiswahili ila kuna nadharia mbalimbali zinazoelezea chimbuko la lugha.

Mojawapo inadai kwamba, lugha inatokana na tabia za kuiga.

Binadamu wa kale wanasemekana kwamba hawakuwa na lugha lakini hoja ya mawasiliano miongoni mwao inazuka sauti mbalimbali zilizokuwepo katika mazingira yao, mfano waliiga sauti za wanyama, wadudu na mambo mengine mbalimbali.

Sauti zikiimarishwa kadri ya muda ulivyopita zikazua lugha na kufanya kiswahili na kuwa mojawapo ya lugha inayozungumzwa, pia kuna mjadala unaoeleza chimbuko la kiswahili.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

**MSWAHILI NI NANI?**

Kuna nadharia nyingi zinazoelezea chimbuko la kiswahili miongoni: -

**Mswahili ni**

(i) Mzaliwa wa pwani ya Afrika Mashariki

(ii) Mtu yeyote anayezungumza kiswahili

(iii) Mtu mwenye asili ya kiafrika

(iv) Mtu yeyote mjanja azungumzaye sana pia mwongo.

**NADHARIA YA CHIMBUKO LA KISWAHILI**

Kuna nadharia nyingi zinazoelezea chimbuko la kiswahili miongoni mwa hizo ni kiswahili ni **pijini** au **kreoli**

1. **PIJINI**

Ni lugha ambayo inazuka kutokana na mwingiliano wa lugha mbili tofauti. Inasemekana kwamba lugha ya kiarabu ni lugha za kienyeji zilizokuwa zikizungumzwa Afrika mashariki ndio iliyofanya au iliyosababisha lugha ya kiswahili.

**UDHAIFU WA NADHARIA HII**

Nadharia hii haiaminiki kwa sababu inashindwa kuelezea lugha za kienyeji zilizokuwa zikizungumzwa mashariki kabla ya ujio wa waarabu.

2. **KISWAHILI NI KRIOLI**

Kreoli ni pijini iliyokomaa ambayo imebadilika na kuwa lugha mama ya vizalia (ya kwanza)

**UDHAIFU WA NADHARIA HII**

Nadharia hii inashindwa kueleza chimbuko la kiswahili kwa uwazi kwa sababu haiangalii vigezo vingine vya lugha mfano, muundo wa vitenzi, lugha yenyewe, matamshi na sarufi za lugha, nadharia hii inazingatia msamiati wa kiarabu katika kiswahili.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

3. **KISWAHILI NI KIARABU**

Kuna nadharia isemayo kiswahili ni kiarabu kwa sababu zifuatazo

(a) Msamiati ambao hutumika katika mawasiliano ya kila siku katika kiswahili unatokana na kiarabu yaani asilimia arobaini na moja ya maneno yatumikayo katika kiswahili (41%)

(b) Kuna mfungamano wa ukaribu kiutamaduni baina ya waswahili na waarabu.

(c) Jina la kiswahili linatokana na sahel ambalo linamaanisha pwani, kutokana na upotoshaji wa matamshi neno hili linatamkwa swahili au suaheli.

**UDHAIFU WA NADHARIA HII**

(a) Ni tabia ya kawaida kwa kila lugha katika ulimwengu kukopa msamiati toka katika lugha nyingine, kwahiyo kiswahili kina idadi kubwa ya msamiati wa kiarabu ni jambo la kawaida Mfano: -

- Kipakistani kina asilimia 51% ya msamiati wa kiarabu lakini hakiitwi kiarabu.
- Kiingereza kina asilimia kubwa ya msamiati wa kigiriki, kilatini na kifaransa lakini hakiitwi kigiriki, kilatini wala kifaransa

(b) Mwingiliano wa lugha moja au nyingine ni jambo la kawaida mfano ;waswahili wenye tamaduni za kizungu hawawezi kuitwa wazungu.

(c) Kuwa na jina la kigeni hakumbadilishi mtu mwenyeji na kuwa na asili tofauti. Mfano mswahili akiitwa Abdallah au John hakumfanyi mtu huyo kuwa mwarabu au mzungu.

Watetezi wa nadharia hii ni wageni ambao hawakujua historia halisi ya waafrika. Kumbukumbu zilikuwa hazipatikani kwa sababu waafrika wa kale hawakuziweka kumbukumbu na kumbukumbu zilizoko hazitoshelezi upatikanaji wa taarifa. Kwahiyo wananadharia hii waliandika chimbuko la kiswahili kwa jinsi walivyoona wao. Kwa mantiki hiyo wamechangia maendeleo ya kiswahili

**4. KISWAHILI NI KIBANTU**

Wanapotetea nadharia hii wanatumia zaidi hoja ya kisayansi yaani wametafiti lugha ya kiswahili kwa kuangalia muundo (structure) (syritax) sarufi, matamshi (pronousition) na msamiati yaani (vocabulary).


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

**Pia hoja zao zimegawanyika katika vigezo vya historia, mfano:-**

Wamestadi historia ya lugha ya wenyeji.

Wamestadi historia ya wenyeji wa pwani ya Afrika Mashariki, asili na utamaduni wao, mwingiliano wao na wageni. Wengi wa watetezi wa nadharia hii ni wanaisimu wazawa ambao wameshirikiana na wageni wametafiti kibantu na yale yanayowazunguka wabantu.

Mfano; makabila ya wabantu na yale yanayowazunguka wabantu. Profesa Melcom Guthrie ambaye kwa muda wa miaka ishirini alizifanyia uchunguzi lugha za kibantu zinazozungumzwa kusini mwa jangwa la Sahara hadi Afrika kusini na vilevile kutoka mashariki hadi magharibi mwa Afrika.

Kutokana na hoja za watetezi wa nadharia hii, hoja zao zimegawanyika katika makundi mawili.

**(i) Hoja za kiisimu**

**(ii) Hoja za kihistoria**

**HOJA ZA KIISIMU**

Hoja hii imejikita zaidi katika muundo wa lugha mfano muundo wa vitenzi, majina, mnyambuliko wa maneno pia vipengele vya sintaksia, matamshi na msamiati.

Vipengele hivi kwa ujumla vinaonesha uhusiano wa karibu uliopo baina ya kiswahili na lugha nyingine za kibantu.

Mfano:-

**(a) Msamiati lugha**

- Kiswahili - maji
- Kibena - lulenga
- Kihaya - amaizi



Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

- Kinyakyusa - amaisi

**(b) Kisintakisia**

Lugha

- Kiswahili - mtoto analia sana
- Kipare - mwana eiya muno
- Kibena - mwana ivemba sana
- Kimeru - mwanaakeiya muno
- Kuhaya - omwana nalila muno
- Kijita - omwana kalila muno
- Kinyakyusa - mwana akulila fijo
- Kichaga - mana nekefila mno

Muundo wa kisintaksia wa sentensi za lugha za kibantu katika hali yakinishi zinazotangulia ni: -

J + T + E yaani jina, kitenzi au jina jingine na kitenzi.

**(c) KIMUUNDO WA KITENZI**

Vitenzi vya lugha ya kibantu huishia na irabu "a" vinapokuwa katika hali yakinishi.

Mfano : -

- Kiswahili - soma, piga, pita, kivemba

- Kihehe - kwiamba

- Kinyakyusa - Imba, koma

- Kivemba - (Zambia) Ponona (pijini)

Lugha zisizo za kibantu zina muundo tofauti na ule wa kibantu.

(d) Pia vitenzi vya lugha ya kibantu hunyambulika ili kuunda na kuzalisha maneno mengi wakati zisizo za kibantu zinakataa muundo huu.

Mfano: - pigana, piganiwa, pigwa, pigishwa, pigika (kiswahili)


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Kapa (piga) – kapana, kapanyia (Kichaga)

Ntoa (piga) kuntoa,kutoana (kizaramo)

(e) Pia vitenzi vya lugha za kibantu vina kawaida ya kudondosha irabu “a” nakupachika irabu “O” mwishoni mwa mzizi wa neno ili kuunda jina, mfano: -

- Kiswahili soma - somo

T N

- Kinyakyusa – kumana – lukumano (mkutano)

- Kipare – lya (lia) – kiyo

- Kiacholi (nilokiki) – gene – (tumaini) gen (matumaini)

Lugha zisizo za kibantu hazina kawaida hii

Mfano: - (Nirot) kacho (tumaini)

J T

Kach (matumaini)

(f) Kigezo kingine kinachodhibitisha kwamba kiswahili ni kibantu ni kanuni za ngeli za majina. Majina ya kiswahili na lugha za kibantu zinapangwa katika makundi kutokana na aina zake (ngeli) mfano majina yanayotaja viumbe hai yana kanuni inayotawala, hali kadhalika majina ya mimea, vitu n.k

Mfano: - kipepeo, mbwa, baba, sisimizi, yanaingia katika kundi la aina moja yaani kipepeo anaruka, baba anaruka, huwezi kusema kipepeo kinaruka.

Pia kwa kanuni za kibantu inabainishwa kwenye viambishi ngeli mwanzoni mwa majina.

**Mfano: -**

- Mtoto - Watoto


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- Mtu - Watu
- Mti - Miti

(g) Utafiti uliofanywa na profesa M. Guthrie kwa zaidi ya miaka ishirini 20 juu ya lugha za kibantu aligundua kwamba katika mizizi ya maneno 22000 mizizi hiyo imetapakaa katika lugha zote za kibantu kuanzia kusini mwa Afrika na pia Mashariki na Magharibi mwa Afrika mtawanyiko unapungua jinsi unavyokwenda toka katika eneo la kati mwa Afrika.

**HOJA ZA KIHISTORIA**

Habari za kihistoria ambazo zimepatikana zinaonesha au kudhibitisha kuwepo kwa lugha ya kibantu (kiswahili) kabla ya ujio wa wageni pwani ya Afrika mashariki. Ushahidi huu wa kihistoria ni wa muhimu kwani unadhibitisha kwamba kiswahili kilikuwepo tangu zama hizo.

Hoja za wanahistoria zinazotumika hapa zimechukuliwa au kunukuliwa kutoka kwa watu mbalimbali ambao waliwahi kufika au kupata kuzisikia habari za huku. Miongoni mwa hoja hizo ni pamoja na.

- Kuwa hoja za kihistoria tunaangalia chimbuko la watu jamii ya wabantu. Wabantu asili yao ni kusini mwa Cameroon kufikia karne ya tano (5) kulikuwa na kundi la wabantu wa Cameroon lililoondoka maeneo ya asili na kwenda kusini wakiambaa pwani ya Afrika ya Magharibi na wengine wako katika misitu minene ya ikweta na kutokea kwenye mabonde yenye rutuba ya kongo. Sababu kuu ya kusambaa kwao ni ongezeko la idadi ya watu na mifugo waliyokuwa nayo. Kuongezeka huko kulipelekea kupungua kwa maeneo ya kuishi na kulisha mifugo.

- Idadi iliongezeka tena katika makazi mapya ya Congo hii ikasababisha msambao mwingine tena , safari hii uelekeo wa makundi yao uligawanyika sana baadhi yao wakaja Afrika mashariki, kaskazini mashariki ya Kenya yaani katika maeneo ya Shungwaya. Kundi lingine lilielekea kusini zaidi mathalau Afrika ya kusini kundi lililoelekea shungwaya lilikutana na utawala wa watu kutoka maneno ya sudani ya kusini. Baada ya mgongano huo kundi hilo lilisogea kusini ya maeneo ya mto Tana. Hapo walijenga na kuimarisha tawala zao na baadae walipigana na watu kutoka kaskazini na hivyo wakahama kimakundi, wengine wakaambaa upande wa Afrika Mashariki na wengine wakaambaa na kuvuka bahari kwenda kusini visiwani kama visiwa vya unguja ungazija (Comoro) na Bukini (Madagascar) kundi la wale walioishi Afrika Mashariki ndio chimbuko la Kiswahili cha sasa. Na kundi la wabantu asili ni wale waliobaki Kongo kama vile Walingala, wamba na wabemba wa Zambia.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- Mgawanyiko wa Lahaja (Dialect) ni matawi ya lugha za kiswahili uliopo sasa kutoka kibantu asili umetokana na sababu kadhaa kama vile tofauti za kimazingira, nyakati na mwingiliano wa kiutamaduni baina ya wabantu na watu wasio wabantu.

- Wanahistoria na mabaharia mbalimbali ambao wamepata kufika maeneo haya waliandika katika taarifa za ustawi watu na utamaduni uliokuwepo zama hizo katika pande hizi za Afrika ya mashariki

Mfano: -

**(a) MWANAHISTORIA IBIN BATUTA (14 B.C) – 1331BC**

Huyu alifika Afrika ya mashariki mnamo karne ya 13 anasema " nilisafiri kutoka Mombasa mwendo wa siku mbili tukitokea visiwa vya Mafya. Hapo tuliwakuta wenyeji hawana chakuwa na nafaka zao wanazitoa uswahilini".

Nafaka na bidhaa za wakati ule zilitoka bara ambako kuliitwa uswahilini yaani walikoishi watu waliozungumza kiswahili.

## KUKUA NA KUENEA KWA LUGHA

Lugha kama phenomena ina tabia ya kuzuka na kukua kisha kuenea na wakati mwingine lugha hufa. Ukuaji wa lugha hutegemea viungo vifuatavyo:

(i) Lugha inapoongeza idadi ya misamiati yake.

(ii)Lugha inapoanza kutumika katika mawasiliano rasmi ya serikali na kitaifa au kijamii kama katika biashara, kidini na kishughuli za kiofisi pia inapoingizwa kwenye taaluma za kisayansi na kiteknolojia.

(iii)Lugha inapoanza kuandikwa kwa kutumia hati za maandishi na huifanya lugha idumu katika historia kwa kuwa inadumu katika kumbukumbu, kwa mfano: - kiswahili mwanzoni kilikuwa kinaandikwa kwa kiarabu baadae kwenye karne ya 19 ndio ikahama kuandikwa kwa herufi za kilatini kama hivi tunavyotumia.

(iv)Lugha inapofanyiwa utafiti wa kina juu ya chimbuko, matumizi yake pamoja na sarufi kisha ikasanifiwa. Kiswahili kilianza kusanifiwa mnamo mwaka 1925. Kusanifiwa ni kufanya kitu kiwe na muundo maalumu.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Kuenea kwa lugha kunatokana na wazungumzaji wa lugha hiyo. Pia inapopata wazungumzaji wengi kwa wakati huo inapoanza kuzungumzwa katika eneo pana zaidi ya eneo la chimbuko lake kwa namna nyingine ili kwamba lugha inaweza kuwekwa: -

- Inapotawanyika kwenye eneo lake la asili

- Inapopata wazungumzaji wengi

Shughuli za wageni wa kwanza kufika Afrika ya mashariki zilisaidia kukua na kuenea kwa lugha ya kiswahili, wageni hao walikuwa ni wapitaji tu. Shughuli hizo ni kama biashara, n.k

**(b) USHAHIDI WA FUMOLIONGO**

Ushahidi huu unasisitiza kwamba, kiswahili ni kibantu na kwamba ni lugha iliyokuwepo kabla ya ujio wa wageni unaopatikana katika lugha fasihi ya wakati huo. Mfano ushahidi wa Fumoliongo ambao uliandikwa karne ya 17 lakini ni wa zamani sana kabla ya nyakati hizo.

**(c) USHAHIDI WA PERPLUS**

Huu ni ushahidi ambao ni wa vitabu vya Perplus ambavyo ni mwongozo wa kijiografia kuhusiana na safari za baharini ilikuwa ni pamoja na bahari ya Hindi na visiwa vyake. Vitabu hivyo viliandikwa katika bandari ya Alexandria nchini Misri. Kutokana na vitabu hivyo, visiwa vya Afrika Mashariki vinatajwa pamoja na watu wake, visiwa vya unguja vinaitwa Zenj na pwani ya Afrika Mashariki inaitwa Azania.

**(d) USHAHIDI WA AL-MASUID (915 BK)**

Aliandika juu ya watu wa Pwani ya Afrika Mashariki. Wakazi wa pwani hii waliitwa wazenj. Hivyo neno Zanzibar ndivyo lilivyopatikana. Pia Al- Masud aliandika wazenj waliongozwa na wakili kwa maana ya wafalme. Anaendelea kusema kuwa wazenj walizungumza lugha fasaha na kwamba viongozi wao walihutubia kwa lugha ya kwao. Inaaminika kwamba baada ya majilio ya waarabu, kiswahili kiliitwa kiazania au kizenj.

**(e) USHAHIDI WA AL-IDRIS (1100 – 1166)**

Katika mahakama ya Rogers wa pili (II) katika visiwa vya sicily mwanabaharia Al-Idrisi alieleza kuwa pwani ya Afrika Mashariki kama kisiwa kiitwacho Unguja, pia aliandika


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Downloaded from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

vyakula vinavyopatikana huku mfano: - Mkono wa tembo,Kisukari ambayo ni majina ya ndizi.

Shughuli za wageni hawa wa kikoloni zilikuwa ni biashara, dini na utawala.

1. **KIDINI**

Waarabu pamoja na malengo yao mengine walikuja kueneza dini ya kiislamu. Katika uenezaji wa dini hiyo. Walitumia lugha ya kiswahili kuhubiri na pia walifungua shule za madrasa ambazo walifundisha Quran kwa lugha ya kiarabu huku wakifafanua kwa lugha ya kiswahili. Wanafunzi wa madrasa waliimba kaswida kwa lugha ya kiswahili.

Wakati huo kiswahili kilianza kuandikwa katika hati za kiarabu na pia misamiati ya kiarabu ikiingizwa katika kiswahili mfano: - Allah, Dini, Msikiti, Madrasa, Sujida, Amini n.k.

Wakati huohuo waarabu wakihubiri na kueneza dini ya kiislamu pia walikuwa wakijishughulisha na mambo ya biashara.

2. **BIASHARA**

Biashara ya wakati huo ilikuwa ni ya watumwa, nguo, madini na pembe za ndovu. Inasemekana waarabu hawa walifika kunako karne ya tisa (8th – 9th C)BK.

Kulikuwa na misafara mikubwa sana ya biashara ambayo ilipita maeneo mbalimbali ya Afrika Mashariki na ya kati. Katika misafara hiyo watu wengi walijumuika ambapo kulikuwa na wapagazi ambao walikuwa kwa makundi.

Misafara toka pwani kwenda bara au kutoka bara kwenda pwani ilichukua muda mrefu na wakati wote huo lugha ya mawasiliano ilikuwa ni kiswahili. Watu kutoka bara walikuja pwani na walikaa kwa muda mrefu, waliporudi kwao waliendelea kuzungumza kiswahili kwahiyo walikieneza.

Misafara hiyo ilikuwa na vituo kati ya eneo moja na jingine katika vituo hivyo kiswahili kikaenea. Misafara mikuu mitatu ilipita Tanzania na hivyo ikafanya kiswahili kuenea zaidi Tanzania kuliko Kenya na Uganda. Misafara hiyo ilikuwa kama ifuatavyo: -


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

(a) Msafara wa kutoka Pangani kwenda bara na kutoka bara kwenda Pangani.

(b) Msafara wa kutoka Bagamoyo kwenda bara au kutoka bara kwenda Bagamoyo. Wanyamwezi ndio walikuwa wapagazi wa msafara huo na Wagogo ndio walikuwa wahusika.

(c) Msafara kutoka Kilwa kwenda bara au kutoka bara kwenda Kilwa. Wayao ndio walikuwa wapagazi wa msafara huu.

(d) Msafara huu wanne ulikuwa wa nchi jirani ya Kenya na Uganda. Msafara huu ulikuwa ni wa kutoka Mombasa kwenda bara na kutoka bara kwenda Mombasa , Kenya hadi Uganda na Wakamba ndio walikuwa wapagazi wakuu katika misafara hii ya kibiashara wakati wa waarabu ni Wayao, Wagogo, Wanyamwezi (Tanzania), Wakamba wa nchi ya Kenya.

3. **UTAWALA**

Utawala wa waarabu walipohamia unguja walisaidia kuenea kwa kiswahili. Wakati wa utawala huo kilimo cha karafuu kilianzishwa Unguja. Wakati wa kuvuna vibarua wengi walichukuliwa bara kwenda Unguja (pwani) kuvuna.

Wageni hawa walichukuliwa muda mrefu huko unguja kuanzia miezi mitatu hadi sita, wakati wote huo walijifunza kuzungumza kiswahili na waliporudi kwao bara walieneza kiswahili.

Pia Sultani wa Oman aliyeishi Zanzibar aliambiwa na Mfalme Leopald wa II wa Congo ampelekee walimu ambao wangeunda kufundisha askari wa Kongo lugha ya Kiswahili.

Msamiati ulianzia kwenye kiswahili kutokana na Kiarabu ni pamoja na akida, adhuhuri, abudu, amini, hamsini, arobaini n.k

**WAJERUMANI**

Wajerumani ni kundi la pili la wageni walioingia Tanganyika. Shughuli zao hazikutofautiana na makundi mengine kama yale ya kiarabu.

**DINI**

Wajerumani walikuja kuhubiri dini ya kikristo, kabla ya kuingia walifikia kwanza Unguja ambako walijifunza lugha ya kiswahili. Kisha wakaitumia kuhubiri dini ya Kikristo.



Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Wamisionari walijenga na kufungua shule na seminari lakini Kiswahili kilikuwa ndio lugha ya mawasiliano. Pia Wajerumani waliandika vitabu vya kidini kwa lugha ya kiswahili mfano: -

Biblia takatifu, katekisimu, wamisionari nao walianza kuandika kiswahili kutoka katika hati za kilatini ambazo ndizo tunazozitumia hadi leo. Wamisionari kama vile Krapf na Menen waliandika kamusi hii ambayo ilizingatia lahaja za Kimombasa.

**BIASHARA**

Misafara iliyokuwepo wakati wa kiarabu iliendelea mpaka wakati huu ila biashara ya kitumwa haikuwepo, biashara nyingine ziliendelea kama zilivyokuwa awali.

**UTAWALA**

Utawala wa Kijermani ulichukua hatua za kukuza na kueneza kiswahili kwa kuwa lugha kuu katika mawasiliano ya ngazi ya chini ilikuwa kiswahili. Mathalani waliteua maakida, wajumbe kusimamia mashamba na shughuli zao nyingine na lugha hii ya mawasiliano iliyotumika na maakida ilikuwa kiswahili.

Wakati huu serikali ya Wajermani waliifanya kiswahili kuwa ni ligha ya kufundishia katika shule za msingi. Pia Wajermani walijenga shule ya kwanza ya Serikali huko Tanga (1892) shule hii ilikuwa na wanafunzi kutoka pande zote za Tanganyika na makoloni mengine kama Burundi na Rwanda.

Pia wajerumani walianza ujenzi wa reli ya kati ujenzi huu ulijumuisha watu kutoka sehemu mbalimbali na lugha waliyotuimia katika mawasiliano ilikuwa ni kiswahili. Pia walifungua mashamba makubwa ya karanga, pamba, katani n.k katika mashamba hayo waliajiriwa manamba kutoka maeneo kadhaa ya Tanganyika na waliwekwa katika makundi maalumu na huko walizungumza kiswahili na waliporudi kwao walikieneza.

## WAINGEREZA NA BAADA YA UHURU

Baada ya vita kuu ya pili ya dunia Tanganyika ilikuwa chini ya utawala wa mwingereza. Wakati wa utawala huo shughuli za utawala, kidini na biashara zilikuwapo zikiendelea.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Uenezaji wa dini ya kikristo uliendelea chini ya wamisionari ambapo kama ilivyokuwa kwa tawala zilizopita walifungua shule, hospitali, vyuo vya ufundi ambako lugha ya kiswahili ilitumika kama lugha ya kufundishia.

Waingereza hawakupenda wala kutaka mfumo ulioachwa na wajerumani hivyo waliamua kufanya kiswahili kuwa lugha ya kufundishia katika shule za msingi hadi darasa la nne na pia wakati huo wamisionari wenye asili ya kijerumani walihama kwa kuhofia utawala mpya wa mwingereza.

Shule nyingi zilizokuwa nchini zilikuwa na upungufu mkubwa wa walimu na pia zilikosa pesa za uendeshaji. Biashara kubwa iliyokuwa ikifanyika kwa wakati huo ilikuwa ni ya mazao ya biashara, madini na mazao yatokanayo na wanyama, nguo na biashara nyinginezo.

Utawala wa mwingereza pamoja na kuifanya lugha ya kiingereza kuwa lugha rasmi ya mawasiliano ilifanya juhudi za makusudi kukuza na kueneza kiswahili.

Kiswahili kiliposanifiwa katika miaka ya 1920 mambo mengi yalianzishwa na serikali ili kukieneza kiswahili mfano gazeti la mamboleo lilianzishwa mwaka 1925. Gazeti hili lilienezwa pande zote za nchi, waliojua kusoma walisoma, wasiojua kusoma walisomewa. Kulikuwa na ukurasa maalumu wa ushairi ambao ulipendwa sana wakati huo. Pamoja na gazeti hili yalianzishwa magazeti mengine mfano: - gazeti la Baraza la habari za wakilindi lilichapiswa unguja mwaka 1931.

Wakati wa utawala wa waingereza ndipo kituo cha redio kilianzishwa mwaka (1952) kilijengwa barabara ya kichwele kiliitwa sauti ya Dar es Salaam na baadae kilibadilishwa na kuitwa sauti ya Tanganyika. Kituo hiki mwanzoni kilitangaza maeneo ya Dar es salaam tu na eneo jirani na lugha iliyokuwa ikitumika ni kiswahili. Kiswahili ni lugha ya matangazo, Gavana wa kwanza aliamua kiswahili kisanifiwe mwaka 1923. Sababu zilizopelekea kusanifiwa kwa kiswahili ni kwamba hazionekani.

Mathalani mombasa walichukua lugha ya kihija, pemba waliongea kipemba, unguja waliongea kiunguja, tanga walizungumza kitanga

Kwahiyo basi ilikuwa ni vigumu kumtahini mwanafunzi lahaja mbalimbali, hivyo ulitakiwa mfumo ambao kungelikuwa na tawi moja la lahaja ambapo ingetumika kufundishia na kutahini mwanafunzi katika makoloni ya Uganda, Kenya, Tanzania, Malawi na Zaire.

Mwaka 1920 ilizinduliwa kamati iliyoitwa interrior language commitee na kazi zake zilikuwa ni kusanifu lugha ya kiswahili, na kuanza kazi yake mwaka 1925.

Kamati iliunganisha wakurugenzi wa makoloni ya waingereza kutoka nchi zilizotajwa na pia zilizohusisha wataalamu wa lugha na walimu wa lugha.

Mfano: Edward Steeve, Mchungaji Krapf, Naadeu na mkewe katika halmashauri hii iliteuliwa lahaja ya kiunguja kiusanifu.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

## SABABU YA KUTEULIWA LAHAJA YA KIUNGUJA

(I) Kiunguja kilienea zaidi kuliko lahaja nyingine

(II) Lahaja ya kiunguja ilikidhi hoja ya kimawasiliano.

(III) Kiunguja ni lahaja iliyokubali kubadilika kiurahisi

(IV) Kiunguja kilikubaliwa na wengi mwisho kufikia mwaka 1929 kiunguja kilifanywa lahaja rasmi na sanifu

## HATUA ZILIZOCHUKULIWA

1. Kamusi iliyoandikwa na Manan ilikubaliwa kufundishia.
2. Mafupisho yote ya vitabu vilivyobidi kufundishia mashuleni ilibidi vichapishwe na kamati ya lugha.
3. Kamati ilisimamia ukuaji na uendeshaji wa vipaji chipukizi wa kiswahili.
4. Kamusi ya kiingereza "Petrick Johnson" ilipitishwa kuwa ya urasimu.

## HARAKATI ZA KUPIGANIA UHURU

Kuanzia mwaka 1940 kulikuwa na vurugu za kupigania uhuru kote Afrika ya Mashariki.kulikuwa na vikundi mbalimbali vilivyoendesha harakati hizo.

Mfano: -

- Vyama vya kupigania uhuru U.P.C huko Uganda, KANU Kenya na T.P.P Tanganyika. Katika harakati hizo lugha ya mawasiliano ilikuwa kiswahili.

- Vyama hivyo vilikuwa na makundi ya umoja wa wanawake na vijana. Jumuiya hizi za chama zilitumika kuhamasisha harakati za ukombozi kupitia nyimbo, mashairi, ngonjera n.k.

- Na kwakuwa kampeni za kupigania uhuru ziliendelea hadi huko vijijini, lugha ya kiswahili ikawa hadi huko. Mwaka 1954 kilianzishwa chama ha UKUTA ambacho kilihamasisha wananchi wa sanaa ya fasihi hususani ushairi na ngonjera. Lengo kubwa lilikuwa ni kuinua vipaji vya washairi wadogowadogo.

## KISWAHILI AFRIKA MASHARIKI NA PWANI.

Kiswahili hakikuenea katika uwiano uliosawa katika nchi za Afrika Mashariki na kati. Kuna sababu nyingi ambazo zilizuia ama zilisaidia kukua na kuenea kwa lugha hii.

### (a) TANZANIA


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Kiswahili kilienea katika sehemu kubwa ya Tanzania kutokana na sababu zifuatazo.

- Wakati wa waarabu kulikuwa na misafara mikuu ya biashara ya watumwa pamoja na biashara nyinginezo. Misafara hii ilisaidia kwa kiasi kikubwa ukuaji na uenezaji wa lugha ya kiswahili.

- Hapakuwa na wanyama wakali wa kuweza kuzuia misafara hii kwenda bara.

- Wajerumani walipotawala nchi walifanya juhudi za kueneza na kukuza kiswahili.

- Kulianzishwa vyombo vya habari ambavyo ni kama redio, magazeti ambavyo kwa kiasi kikubwa vilitumia lugha ya kiswahili.

- Harakati ya kupigania uhuru zilisaidia kukua na kuenea kwa lugha ya kiswahili.

**(b) <u>KENYA</u>**

Kuenea kwa kiswahili Kenya kulikumbana na matatizo mbalimbali hata hivyo kiswahili kiliweza kujipenyeza katika maeneo kadhaa. Tatizo kubwa lilikuwa ni: -

- Wanyama wakali ambao walizuia misafara kutoka pwani kwenda bara

- Makabila makali kama wamaasai na wamang'ati ambao hawakuwaruhusu wageni kupita au kuingia katika himaya zao.

- Wakoloni walihimiza matumizi ya lugha za kienyeji kufundishia katika shule za msingi.

- Hata hivyo baadae kiswahili kiliweza kutumika zaidi katika sehemu za mjini kama vile Nairobi, na mashambani katika maeneo ya mizani, katika maeneo hayo kulikuwa na mkusanyiko wa watu kutoka sehemu mbalimbali za nchi.

**(c) <u>UGANDA NA RWANDA</u>**

Kiswahili katika nchi ya Uganda hakikupata msukumo wowote wa kimaendeleo, wageni kutoka pwani waliofika Uganda walikuwa ni waarabu. Lugha waliyotumia ilikuwa ni kiswahili na kwa sababu walihusisha na kiislamu. Pia tawala za kienyeji za Uganda zilikuwa na nguvu na utamaduni wowote wa kigeni haukukaribishwa.

Wamisionari wa kizungu ambao walikuwa ni wakatoliki pia walichochea chuki ya waganda dhidi ya waislamu na lugha ya kiswahili ilibaki kutumika kwa uchache maeneo ya mjini kama vile Jinja na Kampala na pia ilikuwa ni lugha inayotumika jeshini sababu iliwaunganisha maaskari toka makabila mbalimbali.

Misafara ya wageni kutoka pwani ya Afrika Mashariki ilipofika Rwanda ilipata vikwazo, wanyarwanda hawakupendelea mambo ya wageni, ilikuwa ni pamoja na lugha zao.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Wajerumani walipoanza utawala Rwanda kama sehemu ya Tanganyika mwishoni mwa karne ya 9 walikipenyeza kiswahili katika nchi ya Rwanda.

Katika utawala wao walihimiza matumizi ya lugha ya kiswahili waliotoka Tanganyika walikuwa na wakalimani wao ambao walijua kinyarwanda na kiswahili. Pamoja na maafisa wake wengine hii ikachochea wanyarwanda kujifunza kiswahili.

Baada ya wajerumani ikawekwa chini ya utawala wa kibelgiji waliofuata walikikuta kiswahili katika mawasiliano yao na badala yake wakaingiza kifaransa na wakati huohuo dini ya kikatoliki ikatawala kiswahili kikahusianishwa na kiislamu.

Wakati wa utawala wa kibelgiji kiswahili kilitumika katika sehemu chache mjini,mpakani mwa Tanganyika na Rwanda.

Baada ya uhuru wa Rwanda serikali iliimarisha uhusiano na majirani zake. Ilianza kufundisha kiswahili katika chuo kikuu cha KYELI na toka wakati huo idadi ya walimu wa kiswahili iliongezeka, vilevile redio Rwanda ilianza matangazo ya kiswahili ambayo yalikuwa saa moja hadi masaa mawili kwa siku. Vipindi vilivyokuwa vikitangazwa ni matangazo ya mpira, salamu na maombi ya wasikilizaji.

**<u>BURUNDI</u>**

Kama ilivyokuwa kwa Rwanda.

Kiswahili nchini Burundi hakikuwa na nafasi ya kuenea kwa sababu tawala za kabila zilikuwa na nguvu sana.

Wajerumani walipotawala Burundi walihimiza matumizi ya kiswahili kwa maeneo machache ambayo kiswahili kilipenya kama mjini Bunjumbura, wabelgiji walipoanza kutawala Burundi na Rwanda walihimiza matumizi ya kifaransa kiutawala, mashuleni na maeneo ya mipakani, kiswahili kiliendelea kutumika kama lugha ya kuunganisha waburundi na nchi jirani, hata hivyo kiswahili chao kilitofautiana na kile cha wale wanaopakana na Zaire ambao wanazungumza kiungwana, mpakani mwa Burundi na Tanganyika wanazungumza falsafa ya kiasi kikubwa kwa Mrundi wa mashariki anaposema ***"Nitakuja jumamosi au jumapili"*** na yule wa mpakani mwa Zaire anasema ***"Nitakuja siku ya posho au msosi"***

Baada ya uhuru serikali ya Burundi iliamua na ilianzisha somo la kiswahili katika shule za sekondari na vyuo.

Tatizo kubwa lilikuwa ni upatikanaji wa walimu. Hata hivyo uenezaji wa kiswahili huko Burundi umechangia maendeleo ya Burundi kwa kuwa na redio ya idhaa ya kiswahili.

**<u>ZAIRE</u>**


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Kiswahili nchini Zaire kilipelekwa na misafara ya biashara kutoka Afrika Mashariki mfalme Leopard II alimwomba Sultani wa Zanzibar ampelekee walimu wa kiswahili katika jeshi lake, vilevile wahamiaji kutoka sehemu nyingine za Afrika Mashariki walikwenda kufanya kazi katika migodi mfano. Ukanda wa shaba huko walipeleka kiswahili. Hata hivyo katika maeneo ya mjini kama vile Kinshansa, lubumbashi kiswahili kilitumika kama somo.

Baada ya uhuru serikali ya Zaire ilianzisha somo la kiswahili katika shule za sekondari na vyuo. Tatizo kubwa likawa upatikanaji wa walimu, hata hivyo uenezaji wa kiswahili nchini Zaire ulichangiwa na redio ambayo ilikuwa na idhaa ya kiswahili.

Baada ya uhuru kiswahili kilifanya kama idhaa mojawapo ya lugha ya Taifa na kuwa na idhaa inayojitegemea nchini humo. Hadi sasa asilimia 25% ya wazaire wanazungumza kiswahili.

## JUHUDI ZA KUKUZA NA KUENEZA KISWAHILI BAADA YA UHURU

Baada ya uhuru mwaka 1961 juhudi nyingi zilifanywa kukuza na kueneza lugha ya kiswahili, hata hivyo juhudi hizo zilitofautiana kati ya nchi na nchi.

Tanzania baada ya kupata uhuru mwaka 1961 kiswahili kilitangazwa kuwa ni lugha ya Taifa na mwaka 1962 Raisi wa kwanza wa Tanzania Mwl. Nyerere alihutubia bunge kwa lugha ya kiswahili, na kufikia mwaka 1964 kiswahili kilifanywa lugha ya kufundishia shule za ufundi na vyuo vya ualimu, vilevile kikawa ni somo katika shule za sekondari na shule za juu.

Kuanzia kipindi hicho vyombo mbalimbali viliundwa na kushughulikia ukuaji na uenezaji wa lugha ya kiswahili vyombo hivyo vimekuwa vikishirikiana katika kueneza kiswahili hadi sasa.

### 1. USANIFISHAJI WA LUGHA YA KISWAHILI (UKUTA) 59

Chombo hiki kiliundwa kabla ya uhuru mwaka 1959. Kiliundwa ili kustawisha lugha ya Kiswahili na ushairi ili kuendeleza utamaduni wa kiswahili nchini.

### KAZI ZAKE

(a) Kuchochea na kuamsha hali ya matumizi fasaha ya kiswahili pamoja na kuendeleza vipaji vya ushairi kwa vijana waliochipukia.

(b) Kukuza na kuendeleza utamaduni pamoja na michezo ya kuigiza mfano: - ngonjera n.k

(c) Kuendeleza mashindano ya kimataifa ya sanaa pamoja na uandishi na fasihi. Wamechapisha kitabu kiitwacho ngonjera.

### 2. BARAZA LA KISWAHILI TANZANIA (BAKITA)

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Chombo hiki kilianzishwa mwaka 1967 kwa mujibu wa sheria za Bunge, na chombo hiki ndicho chenye kauli ya mwisho kuhusu uongozi wa lugha ya chini kuonesha matumizi ya maneno mbalimbali ya lugha ya kiswahili.

**KAZI YA CHOMBO HIKI**

(a) Kusimamia na kueleza maendeleo fasaha ya kiswahili nchini Tanzania mfano: -

- Kuhamasisha watu wenye nia ya kuandika lugha ya kiswahili.

(b) Kutoa ushauri juu ya matumizi sahihi ya lugha ya kiswahili

(c) Kuunda msamiati na istilahi za taaluma mbalimbali.

(d) Kupitisha msamiati na istilahi mpya katika juma

3. **TAASISI ZA UCHUNGUZI WA LUGHA YA KISWAHILI**

Taasisi hii ilianzishwa rasmi mwaka 1963 ilitokana na kamati ya lugha ya Afrika Mashariki ambayo iliundwa wakati wa ukoloni kufikia mwaka 1964 taasisi hii iliundwa rasmi kwa mujibu wa sheria ya Bunge.

Madhumuni yake makubwa ni uchunguzi katika kuendeleza kiswahili katika nyanja zake zote, mfano ni

(a) Kuhifadhi ufasaha wa lugha.

(b) Kufanya uchunguzi wa lugha kwa madhumuni ya kukuza na kustawisha Kiswahili.

(c) Kuhamasisha watu wapendao kuwa waandishi wa vitabu kwa lugha ya Kiswahili.

(d) Kutunga na kuandaa kamusi,
(e) Kushirikiana na taasisi mbalimbali ulimwenguni kote zinazojishughulisha na utafiti wa kiswahili.

(f) Kukusanya historia na fununu mbalimbali kuhusu kiswahili duniani kote.

(g) Kuandaa warsha na makongamano ya wataalamu na watafiti wa lugha ya kishwahili.

4. **IDARA YA KISWAHILI CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM (1970)**

Idara hii ilianzishwa rasmi mwaka 1970, madhumuni yake ni kuanzisha na kuandaa wataalamu wenye shahada ya masomo ya kiswahili ili kuweza kutumika katika nyanja mbalimbali.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Masomo yanayotolewa na idara ya kiswahili na matumizi ya miundo na nadharia za isimu. Idara hii tangu ianzishwe imehitinisha walimu ambao wanafundisha sekondari au vyuo vikuu nchini.

Pia idara inayowadhamini wachache wanaoandika tasnifu kwa ajili ya shahada ya juu. Vilevile idara hii imeanzisha chama cha kiswahili ambacho malengo yake ni: -

(a) Kuwasaidia wanachama, kuvumbua na kukuza vipaji vyao katika isimu na fasihi ya kiswahili.

(b) Kuamsha ari ya mapinduzi katika kuendeleza fani za lugha ya Kiswahili katika lugha ya maandishi.

(c) Kuandaa mashindano ya lugha na sanaa kitaifa.

(d) Kutoa misaada kwa vyombo vinavyoendeleza kiswahili.

(e) Kushirikiana na idara za lugha zifundishazo kiswahili katika vyuo vikuu mbalimbali duniani kote.

**TAASISI YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIGENI ZANZIBAR (TAKILUKI)**

Taasisi hii ilianzishwa rasmi mwaka 1974 kwa mujibu wa sheria za bunge la 4 Baraza la wawakilishi na baadae ikafanywa sheria.

Kazi zake ni pamoja na: -

(a) Kutoa mafunzo ya masomo ya kiswahili kwa kiwango cha juu kwa watumishi wa Serikali na viongozi ili kukuza ujuzi wao wa lugha ya kiswahili kwa ujumla chombo hiki kinasimamia matumizi fasaha ya lugha ya kiswahili.

(b) Kuendesha mafunzo ya kiswahili na lugha za kigeni kwa wanafunzi wenyeji wa nje.

(c) Kufanya utafiti wa lahaja na fasihi simulizi ya kisasa.

**BARAZA LA MITIHANI TANZANIA**

Lilianzishwa mwaka 1973 lengo lake ni kutunga mitihani mbalimbali ya shule na vyuo vya ualimu ili kupima viwango vya uelewa kwa watahiniwa.

Baraza hili hutunga mitihani ya kiswahili ili kupima uelewa wa watahiniwa na maarifa yao katika lugha ya kiswahili mfano: -

- Mitihani ya waalimu daraja A & B pia
- Mitihani ya shule za msingi na kiswahili kwa sekondari.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

1. **<u>WIZARA YA ELIMU</u>**

Kazi zake ni: -

(a) Kusimamia maendeleo ya shule zote za elimu ya msingi na sekondari.

(b) Kusimamia ufundishaji wa masomo yote pamoja na kiswahili.

2. **<u>TAASISI YA ELIMU – 1966</u>**

Ilianzishwa MWAKA 1966 NA KAZI YAKE KUBWA ni: -

(a) Kutayarisha muhtasari wa vitabu vya kufundishia masomo shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu

3. **<u>TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA</u>**

Ilianzishwa mwaka 1963 kikiwa ni chombo cha kuongoza masomo ya kujiendeleza kwa watu wazima wasio wanafunzi shuleni

Kazi zake: -

(a) Kubaini maneno mbalimbali ya kukidhi hoja ya misamiati au istilahi za taasisi ya Elimu ya wataalamu na wageni wanaokuja kufanya kazi nchini.

(b) Kufundisha na kueneza kiswahili kwa kutumia njia ya masomo ya jioni na kampeni za Taifa za maendeleo.

## <u>VYOMBO VINGINE VINAVYOKUZA NA KUENEZA KISWAHILI</u>

1. **Vyombo vya habari na waandishi**

Kwa muda mrefu waandishi wa vyombo vya habari wamekuwa na mchango mkubwa katika kukuza na kueneza lugha ya kiswahili kwa mfano redio na magazeti yana uwezo wa kufikia eneo kubwa. Na hivyo kuwezesha kuisambaza lugha katika eneo kubwa zaidi mathalani magazeti yanafika katika maeneo mengine ambayo redio na televisheni haviwezi kufika.

Aidha vyombo vya habari vimekuwa mstari wa mbele kueneza msamiati na maneno mapya kila siku.

2. **TAASISI MBALIMBALI ZA ELIMU**

Taasisi za elimu kama shule za msingi, sekondari na vyuo kwa kiasi kikubwa zimekuwa zikichangia kukua na kuenea kwa lugha ya kiswahili kote nchini kwa takribani shule moja ya msingi katika kila tarafa hapa nchini.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Taasisi hizi zimekuwa zikieneza lugha ya Kiswahili kila mwaka kwa wahitimu kadhaa wanaomaliza katika shule hizo. Nao huwa wazungumzaji wa lugha ya kiswahili.

3. **MIUNDO, MBINU NA UKUAJI WA MIJI**

Ujenzi wa miundombinu ya kisasa inayorahisisha mawasiliano kati ya miji na vijiji kutoka sehemu moja na nyingine kumesababisha ukuaji na uenezaji wa lugha ya kiswahili kote nchini.

Kwa mfano uwezekano wa usafiri kati ya eneo moja la nchi na jingine kusaidia kuhusisha mwingiliano wa watu na maeneo tofauti tofauti. Hali hii imesaidia kukua na kuenea kwa lugha ya kiswahili katika meneo yote ya nchi.

---

# UTUNGAJI- WA KAZI ZA FASIHI

**UTUNGAJI WA MASHAIRI**

- Mashairi ya kale yanajulikana kama mashairi ya kimapokeo mashairi haya hutungwa kwa kufuata kanuni zifuatazo: -

- Kutokana na kanuni hizo shairi la kimapokeo litakuwa na

1. **KICHWA**

Shairi lazima liwe na kichwa, kichwa cha shairi hutokana na jambo linalojadiliwa katika shairi. Kichwa hicho huandikwa kwa kutumia maneno machache yasiyozidi matano.

2. **BETI**

Vifungu vya maelezo katika shairi huitwa beti. Shairi halina budi kuwa na beti. Idadi ya beti hutegemea utashi wa mtunzi. Hata hivyo shairi zuri ni lile ambalo idadi ya beti zake hazizidi kumi.

3. **MUUNDO**

Muundo wa shairi ni namna shairi linavyogawanyika katika beti zenye idadi maalumu ya mistari. Shairi la kimapokeo sharti liwe na muundo maalumu katika beti zake zote.

- Miundo ya beti za mashairi ya kimapokeo ni

- Mathra/tathnia – mistari miwili katika ubeti
- Tathilitha – mistari mitatu kila ubeti


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- Tarbia – mistari minne kila ubeti
- Takhmisa – mistari mitano

- Sudusia - mistari sita au zaidi kila ubeti

4. **MIZANI**

Silabi zinazounda mistari ya beti za mashairi huitwa **mizani**

Mfano: -

- Si leo toka zamani , mkulima mtu duni
- Anatabu maishani, tena hupewa dhamani
- Yafaa umakini, kisha tuyachunguzeni
- Si leo toka zamani, mkulima mtu duni

Ubeti huu una mistari yenye mizani 16 kila mmoja

| | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Si | Le | O | To | Ka | Za | Ma | Ni | M | Ku | Li | Ma | M | Tu | Du | ni |
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 |

Mbinu za kupata ulinganifu wa mizani katika mistari ya mashairi ni pamoja na kutumia maneno ya mkato mfano “alosema”badala ya “alilosema” “kicholetwa” badala ya “kilicholetwa”

5. **VINA**

Silabi zinazofanana sauti katika shairi huitwa vina. Katika mashairi ya kimapokeo vina hutokea katikati na mwishoni mwa kila mstari wa ubeti wa shairi au utenzi.

Kwa mfano katika ubeti huu vina vya kati na vya mwisho ni **[ni]**

6. **KITUO**

Mstari wa mwisho katika kila mstari wa beti wa shairi huitwa kituo. Kwa mfano, **si leo toka zamani, mkulima mtu duni** ni kituo

Kazi ya kituo katika shairi ni kuonyesha msisitizo juu ya jambo ambalo linajadiliwa katika shairi.

Kituo kinaweza kubadilika au kutobadilika. Vilevile vina vya kituo si lazima vifanane na vya mistari ya juu.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

7. **UTOSHELEZI**

Utoshelezi wa shairi ni namna, kila ubeti unavyotoa ujumbe unaoeleweka bila kutegemea ubeti mwingine .

kwa mfano: -

- Wazalendo himahima, uchumi kuufufua
- Tena tusimame wima, hatua kuzichukua
- Jambo lililolazima, mbinu bora kutumia
- Tuzingatie haya, wala tusirudi nyuma

Ubeti huu japo ni mmoja ujumbe wake unaeleweka pasipo hata kuhitaji maelezo zaidi ya ufafanuzi. Ubeti huo unazungumzia umuhimu wa kukuza uchumi wa nchi.

8. **MUWALA**

Shairi pia linatakiwa kuwa na muwala. Muwala ni mtiririko wa maelezo ya shairi ambayo yanatolewa kuzingatia utangulizi, kiini na mwishio.

Na si kiini, utangulizi na mwisho au mwisho, utangulizi na kiini

9. **LUGHA YA MASHAIRI**

Mashairi hutakiwa kutumia lugha ya kishairi. Lugha nzuri ya kishairi ni ile ambayo ina matumizi ya misemo na semi tofauti kama vile nahau, methali , maumbo, tamathali za semi, picha, maneno ya mkato na uchezeshaji wa maneno.

Mfano, ubeti unaotumika katika utunzi wa mashairi

Oa utunze cheo, na jina lipate kuwa

Oa upate mkeo, uambiwe umeolewa

Oa kama waowao, moyo usilie ngowa

Oa ujue kukuwa, mpendane na mkeo

1. **TASWIRA AU PICHA**

Ili shairi liweze kuwa na mvuto ni muhimu kutumia lugha yenye picha. Hii ni mbinu ya kuunda picha ya jambo linaloongelewa katika shairi. Utumizi wa picha katika shairi husaidia sana kuchochea hisia za msomaji wa shairi.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

2. **URARI WA MISTARI**

Urari wa mistari katika shairi ni namna kila mstari katika beti unavyotokea katika nafasi yake sahihi kulingana na maelezo yaliyomo katika mstari huo.

**KANUNI ZA UTUNZI WA TENZI**

Tenzi ni tungo ndefu za kishairi ambazo zinasimulia kuhusu kisa au historia fulani.

Mara nyingi maudhui ya tenzi huwa ni ya kuadilisha ambayo hutolewa kwa kutumia mtindo wa usimulizi.

Tenzi za usimulizi mara nyingi ni sahili na hazifumbi.

Kanuni za utungaji wa utenzi hazitofautiani na kanuni za utungaji wa mashairi ya kimapokeo. Tenzi kama ilivyokuwa kwenye mashairi ya kimapokeo hutakiwa kuwa na kichwa, beti, muundo na mistari yake. Vilevile tenzi sharti ziwe na vina, kituo, utoshelezi, muwala, urari wa mistari ya beti, lugha ya kishairi pamoja na matumizi ya taswira.

Silabi za mwisho za kila mstari katika utenzi si lazima zifanane tangu mwanzo hadi mwisho.

Hii yote hutegemeana na mtunzi wa utenzi. Mstari wa mwisho wa kila ubeti huitwa kituo silabi za mwisho za kila kituo zinaweza kufanana katika utenzi mzima. Ikiwa ni hivyo silabi hiyo inayorudiwa rudiwa mwishoni mwa kila kituo huitwa bahari. Hata hivyo silabi ya mwisho ya kituo si lazima ifanane na ya kituo cha ubeti mwingine.

**TOFAUTI KATI YA TENZI NA MASHAIRI**

Tenzi na mashairi hutofautiana hasa katika vipengele muhimu vifuatavyo: -

1. **MUUNDO**

Tenzi hutumia muundo wa tarbia katika beti zake ambapo mashairi yanauhuru wa kutumia muundo mingine tofauti kama vile tathilitha, takhmiso.

2. **UREFU**

Tenzi kwa kawaida ni ndefu kwa vile hutoka zikiwa katika mtindo wa usimulizi na hivyo kuwa na beti nyingi sana ili kukamilisha usimulizi wa kisa ambapo mashairi kwa kawaida hutumia beti chache.

3. **VINA**


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Tenzi zina vina vya mwisho tu, hazina vina vya kati ambapo mashairi yana vina vya kati na vya mwisho.

4. **UREFU WA MSTARI**

Tenzi mistari yake ni mifupi, haigawanyiki katika nusu ya kwanza na ya pili. Mashairi mistari yake ni mirefu na hugawanyika mara mbili, nusu ya kwanza na nusu ya pili huitwa vipande.

5. **IDADI YA MIZANI**

Tenzi katika mistari yake huwa na mizani nane tu, mashairi huwa na mizani 16 katika mistari yake.

6. **KITUO**

Kituo cha utenzi hubadilikabadilika kutoka ubeti mmoja hadi mwingine, kituo cha shairi kinaweza kubadilika au kutobadilika.

**KANUNI ZA UTUNZI WA NGONJERA**

Ngonjera ni tungo za kishairi zinazowasilishwa kwa kutumia mazungumzo ya majibizano baina ya watu wawili au zaidi, majibizano hayo huwa ni mjadala wa malumbano yenye lengo la kutoa ujumbe maalumu kwa wasilikizaji.

Katika majibizano hayo mhusika mmoja hueleza jambo fulani kwa ubeti mmoja, mhusika wa pili hujibu kwa kupinga au kwa kuunga mkono hoja za mhusika aliyetangulia. Mwishoni mwa ngonjera wahusika hao huwa wanaondoa tofauti zao kwa kuwa na msimamo mmoja.

Hali hiyo hutokea pale mhusika mmoja anapokubali kulegeza msimamo wake au kukubaliana na mtazamo wa mwenzake.

Kanuni za uandishi wa ngonjera hazitofautiani na kanuni za utungaji wa mashairi ya kimapokeo. Ngonjera sharti iwe na kichwa, beti, vina, mizani, muwala, utoshelezi, kituo na urari wa mistari ya ubeti. Ngonjera hutakiwa kutumia lugha ya kisanaa kama ilivyokuwa katika mashairi.

**TOFAUTI KATI YA NGONJERA NA MASHAIRI**

Ngonjera hutofautiana na mashairi katika vipengele vinne navyo ni.

1. **WAHUSIKA**

Ngonjera hutumia wahusika wanaojibizana, wahusika hao wanaweza kuwa wawili au zaidi ambapo shairi hutumia mhusika mmoja tu anayezungumzia au anayetoa mawazo yake pasipo kujibizana na mtu.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

2. **UWASILISHAJI**

Ngonjera huwasilishwa kwa njia ya uzungumzaji wa kujibizana, mashairi huwasilishwa kwa njia ya uimbaji.

3. **KITUO**

Ngonjera huwa na vituo tofauti kwa vile kila mzungumzaji huwa na kituo chake lakini shairi huwa na kituo kimoja tu hata kama kitabadilika badilika huwa mwishoni mwa ubeti ili kuonesha mtazamo wa ukinzani wa mada inayojadiliwa kama ilivyo kwa vituo vya ngonjera.

4. **MATUMIZI YA LUGHA**

Ngonjera hutumia sana lugha rahisi lakini mashairi hutumia sana lugha ya kuzama.

**ZOEZI: -**

Andika insha kuhusu umuhimu wa Tembo

**UMUHIMU WA TEMBO**

Tembo ni mnyama mkubwa sana anayeishi msituni na pia anakula majani, Tembo anaweza kuishi zaidi ya miaka 50 hata hivyo tembo ni muhimu katika maisha ya binadamu.

Uwepo wa Tembo ni kivutio cha utalii kwa nchi. Watalii wengi hupenda kuwaona Tembo hivyo husafiri kutoka sehemu moja kwenye nyingine kwenda kuwaona Tembo.

Hata hivyo Tembo ni chanzo cha fedha za kigeni kwa nchi. Kutokana kuwepo na Tembo taifa hupata fedha za kigeni.

Pia meno ya Tembo na pembe zao vina thamani kubwa sana na kutokana na uthamani huo tembo huwindwa sana. Hata hivyo Tembo wana madhara kwa binadamu na hii hutokea pale tembo wanapopita kwenye makazi ya binadamu hasa kwenye njia zao madhara yao ni: -

- Huaribu mazao na mali kama vile nyumba, mahindi na mpunga pale wanapopita karibu na makazi ya watu.
- Tembo pia huweza kusababisha kifo kwa binadamu hii ni hutokana na mwingiliano wao na binadamu.
- Kila kwenye mafanikio hupiganiwa kutokana na thamani hii binadamu tunawadhuru Tembo.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- Ujangili – huu hufanywa na watu huwaua Tembo ili kupata pembe zao na meno yao ambayo ni thamani sana.

Tembo pia ni chanzo cha dawa na chakula baadhi ya jamii nyingine hutumia kinyesi, maini kama dawa na wengine hutumia nyama ya Tembo kama chakula.

Tembo ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi hivyo ni muhimu kuwalinda na kuwatunza kwa ajili ya uwepo wao na tupate faida kutoka kwao na pia kutoa adhabu kali kwa majangili.

**HOTUBA**

Wewe ni diwani wa manispaa fulani yenye viwanda vinavyochafua mazingira kwa kelele, takataka na maji taka.

Andika hotuba yenye maneno kati ya 150 na 200, itakayotolewa kwenye viwanda ili kuepuka uchafuzi wa mazingira.

Ndugu wamiliki wa viwanda, wananchi wengine na wafanyakazi kwa ujumla. Habari za saa hizi, napenda kuwashukuru kwa kunipa nafasi hii kuzungumzia kuhusu uchafuzi wa mazingira unaotokea hapa katika Wilaya/kata yetu kutokana na viwanda vyetu

Uwepo wa viwanda hivi ni chanzo kikubwa cha uchafu wa mazingira.

Uchafuzi wa mazingira ni kuweka kitu kisichohitajika kwenye mazingira, una madhara mengi sana mfano ni yafuatayo: -

- Hupelekea kuenea kwa magonjwa ya ngozi na milipuko kama malaria, kipindupindu n.k. hivyo huongeza gharama ya matibabu kwa serikali.

- Pia uchafuzi wa mazingira hufanya mazingira salama kwa maisha ya binadamu.

Ndugu wamiliki wa viwanda napenda kuwapa umuhimu wa utunzaji wa mazingira na hivyo tuepuke uchafuzi huo.

Kwa kutunza mazingira tutaepuka na madhara yote ya uchafuzi wa mazingira haya tunayoishi na madhara yake.

Napenda kuwashukuru sana kwa kunisikiliza leo hii hapa katika mkutano huu. Asanteni sana na ninaomba tuyatunze mazingira kwa ajili ya vizazi vijavyo. Asanteni sana kwa kuweza kunisikiliza.

**UANDISHI WA HOTUBA**


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Hotuba ni maelezo ambayo yanatolewa na mtu mbele ya watu fulani. Hutolewa kwa madhumuni mbalimbali kwa mfano inaweza kutolewa kwa madhumuni ya kuhimiza kazi, kufanya kampeni fulani au kutoa taarifa fulani kwa watu fulani.

**MUUNDO WAHOTUBA**

Hotuba imegawanyika katika sehemu kuu tatu sehemu hizo ni

1. **UTANGULIZI**

Sehemu hii huwa ni maelezo ya kuwavuta wasikilizaji au wasomaji wa hotuba. Maelezo haya hufunguliwa na salamu. Kwa mfano: - Udumu uhuru na demokrasia! Au wananchi oyeeee!

Utangulizi huu wa utambulisho hulingana na vyeo. Mathalani mheshimiwa mgeni rasmi, au ndugu wananchi. Licha ya utambulish utangulizi huwa na shukrani wa hotuba itakayotolewa.

2. **KIINI CHA HOTUBA**

Kiini cha hotuba ni sehemu ambayo inaonesha jambo linalowasilishwa kwa wasikilizaji, kwa kawaida kiini hufuata utangulizi. Kiini ndicho huonesha ujumbe muhimu wa hotuba kwa wasikilizaji.

3. **HITIMISHO**

Hitimisho ni sehemu ya mwisho ya hotuba. Mwisho wa hotuba kwa kawaida huwa ni muhtasari wa yale yaliyoelezwa kwa ajili ya kusisitiza na kutoa shukrani au kuungana. Aghalabu hotuba huhitimishwa kwa maneno haya: -

- Natoa shukrani zangu kwa wote mlionisikiliza
- Asante kwa kunisikiliza
- Baada ya kusema hayo machache

Ili hotuba ibebe ujumbe ipasavyo haina budi kuwa na vipengele vifuatavyo: -

**MSEMAJI/ MTOA HOTUBA**

Huyu ndiye anayeandaa na kutoa hotuba kwa watu. Mtu huyu hanabudi kuijua barabara mada anayozungumzia, mada anayoifanyia ufasihi na awe na lengo maalumu kama vile kupasha habari kuelimisha au kukanusha mada fulani. Pia hana budi kumudu stadi za mawasiliano kama vile matumizi ya lugha , viungo vya mwili n.k.

**UJUMBE**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Hayo ni mambo ambayo mtoaji hotuba amekusudia, ujumbe hauna budi kuwa wa kina na mapana. Vilevile huwa na mtiririko unaofaa kama, utangulizi, kiini na hitimisho.

**HADHIRA**

Hawa ni watu wanaopokea hotuba. Huwa na malengo na matarajio yao, hivyo mtoa hotuba hanabudi kufahamu hali za kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni kabla ya kutoa hotuba ili aweze kuandaa hotuba inayoeleweka na isiyoleta matabaka kwa hadhira yake.

**MUKTADHA**

Ufahamu wa muktadha utamwezesha mtoa hotuba kutoa hotuba ambayo haitofautiani na hadhira yake anayoishi katika mazingira fulani. Inatakiwa mhutubiaji ajue kiada za watu wanaoishi katika eneo husika ili ujumbe wake uweze kupokelewa kiurahisi.

**LUGHA**

Lugha inayotumika katika utoaji hotuba haina budi kuendana na hadhira husika. Hali hii itasaidia sio tu kufikisha ujumbe kiurahisi bali pia kufanya hadhira iwe na hamu kusikilizwa ikiwa ni pamoja na kujiona kama jamii moja.

**UANDISHI WA RISALA**

Risala ni hotuba fupi iliyoandikwa na kusomwa kwa niaba ya kundi fulani la watu au mgeni rasmi ili kutoa maelezo au msimamo wa kundi kwa kiongozi huyo.

Kwa vile risala husomwa, msomaji hana budi kutoa sauti ya kutosha na yenye kuzingatia lafudhi ya lugha husika ili iwe nzuri.

Pia yampasa kusoma kwa kuzingatia kanuni na taratibu za uandishi bora , taratibu hizo ni kama vile, vituo, uwekaji wa mkazo n.k

Hivyo risala inatakiwa iandikwe kwa lugha sanifu na yenye kuvutia sikio. Pia hoja zake hazinabudi kupangwa kimantiki au katika mtiririko unaojenga na barabara.

**MUUNDO WA RISALA**

Risala yoyote ile ina muundo ufuatao

**MWANZO**

Hii ni sehemu ya kichwa cha risala pamoja na salamu ambapo maneno ya utambulisho hufanywa kichwa cha risala. Huandikwa kwa kwa herufi kubwa na kupigiwa msitari.

**KIINI**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Hii ni sehemu ambayo hutaja lengo la risala kwa kuonesha mafanikio ya changamoto zinazokubali kundi husika.

**MFANO WA RISALA**

RISALA YA UONGOZI WA SHULE YA SEKONDARI CHANIKA

KWA MHESHIMIWA JUMANNE MAGEMBE WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MB) KATIKA SHEREHE ZA KUTIMIZA MIAKA MITATU YA SHULE HII TAREHE 26.01.2008.

Ndugu mgeni rasmi , waziri wa elimu na mafunzo ya ufundi (MB) ndugu mwenyekiti wa bodi ya shule, ndugu walimu na wanafunzi mabibi na mabwana kwa niaba ya uongozi mzima wa shule hii tunayo furaha kubwa kuwakaribisheni katika shule ya sekondari ya Chanika ili muweze kuona na kusikia mambo yanayotendeka hapa shuleni hususani shughuli za kitaaluma, karibuni sana.

Ndugu mgeni rasmi shule yetu ilianzishwa mwaka 2006 tarehe kama ya leo ikiwa na jumla ya wanafunzi 800, waalimu 12 na wafanyakazi wasio waalimu 8, kwasasa shule yetu ina jumla ya wanafunzi 2000, waalimu 30 na wafanyakazi 10. Shule ni ya michepuo ya sanaa na biashara.

Tangu kuanzishwa kwa shule hii leo imetimiza miaka mitatu, tangu kipindi hicho shule hii imekuwa na matukio ya kujivunia. Shule hii imekuwa ikiongoza kitaaluma hasa katika matokeo ya kidato cha pili katika wilaya nzima ya Chalinze. Haya ni mafanikio makubwa ya kujivunia.

Ndugu mgeni rasmi shule hii imefanikiwa kuvuta maji ya bomba. Yamekuwa yakitumika katika shughuli mbalimbali zikiwemo za umwagiliaji wa maua na kadhalika.

Pia shule imefanikiwa kuwa na mgahawa ambao mbali na kuiingizia shule kipato kwa ajili ya matumizi mbalimbali, vilevile umesaidia kupunguza kero kwa wanafunzi kwenda nje ya mipaka ya shule kwa ajili ya kifungua kinywa na chakula cha mchana.

Shule yetu imefanikiwa kujenga zahanati ambayo mbali na kuhudumia wanafunzi wanaopata matatizo ya kiafya wawapo shuleni, pia inahudumia wananchi waishio karibu na eneo hili na kuchangia gharama kidogo. Tunashukuru serikali kwa kutuletea wataalamu wa afya.

Ndugu mgeni rasmi kutokana na mafanikio hayo shule inakabiliwa na changamoto mbalimbali kwanza upungufu wa walimu wanne wa Fizikia, Bailojia na Kemia na mmoja wa somo la biashara, hali hii imekuwa ikileta matatizo ya kiutendaji katika masomo husika.

Pia shule yetu inakabiliwa na tatizo la ukumbi mkubwa wa mkutano. Ukumbi tulionao hautoshelezi mahitaji ya wanafunzi na wafanyakazi shuleni, ukumbi ni mdogo kuliko


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

mahitaji. Wanafunzi zaidi ya 1500 pia walimu wanaongezeka. Mikakati yetu ni kujenga ukumbi mkubwa utakaotosheleza mahitaji yetu ingawa tunakabiliwa na upungufu kwa ujumla ya shilingi Millioni arobaini na tano, milioni ishirini na tano zimeshapatikana kutokana na michango ya wazazi, wadau mbalimbali na mapato ya shule yatokanayo na miradi ya shule hii. Ni mategemeo yetu kuwa serikali itatupiga jeki kwa hili.

Tatu, shule yetu haina gari kwa ajili ya shughuli za kishule, hali hii imesababisha baadhi ya shughuli hasa za kitaaluma zisifanyike kwa wakati hivyo kuchelewesha malengo yetu kwa wakati.

Tunaiomba serikali kupitia wizara yako itusaidie kupata gari litakalokidhi mahitaji yetu. Hata hivyo tuko tayari kupokea mkopo wa gari utakaokubaliwa na wizara yako kutoka taasisi yoyote.

Ndugu mgeni rasmi tunatumaini kuwa utatusaidia katika kukabili changamoto zinazotukabili. Tunakushukuru sana kwa kuitikia wito wetu, asante sana Mungu akubariki.

Risala hii imeandaliwa na mkuu wa shule ya sekondari Chanika.

**UANDISHI KUMBUKUMBU ZA MKUTANO**

Muhtasari wa mambo muhimu yaliyojadiliwa katika mkutano huitwa kumbukumbu za mkutano. Mwandishi wa kumbkumbu za mkutano husaidia kurahisisha utekelezaji wa mambo yaliyojadiliwa/amuliwa pia kumbukumbu za mkutano hutumika kwa ajili ya marejeo kwa ajili ya vizazi vya baadae.

Katika kuandika kumbukumbu za mkutano mambo yafuatayo hujadiliwa.

(a) Kichwa cha kumbukumbu

Kuonesha kuwa mkutano unahusu nini, mahali ulipofanyika na tarehe uliofanywa.

(b) Mahudhurio

Mwandishi anapaswa kuandika orodha ya majina ya watu waliohudhuria mkutano na wasiohudhuria.

**UFUPISHO**.
Ufupisho wa habari uliyoisoma au kuisikia nikitendo cha kueleza habari hiyo kwa kifupi,kwa kutumia maneno yako mwenyewe.Ufupisho huu ukamilika pindi tu msomaji aunganishapo mawazo yake mwenyewe.
Ufupisho: Ni kuwapa wanafunzi uwezo wa kupambanua walichokisoma au walichokisikia na kudondoa mawazo makuu bila kupoteza kiini cha habari ya awali.

**MATUMIZI YA UFUPISHO:**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

1.Hutumika wakati wa kutayarisha ripoti na kumbukumbu za mikutano.
2.Husaidia wakati wa kudondoa hoja kutokana na mihadhara, hotuba.
3.Hutumika katka kuandika shijara au kumbukumbu za kila siku.
4.Husaidia katika uhariri wa habari
5.Hurahisisha habari na kuokoa muda wakati wa kusoma.
6.Huoka fedha, mfano wa upelekaji wa simu za maandishi.

**UFUPISHO UNAWEZA KUGAWANYWA KATIKA AINA TATU ZIFUATAVYO**.
1.Ufupisho wa kuchagua mambo kadhaa muhimu kutokana na habari uliyosoma , kwa mfano wakati wa kutafuta hoja kuu katika aya.
2,Ufupisho ambao msomsji hutakiwa aeleze kifupi habari alivyoisikia aukusoma kwa maneno yake mwenyewe.
Ufupisho aghalabu huwa theluthi moja yahabari ya awali kwa hiyo kama habari ya awali ilikuwa na maneno 3000, ufupisho huwa maneno mia moja hivi.

**KANUNI ZA UFUPISHO**.
1.Mwanafunzi awe na ustadi utakiwao katika kusoma ,yaani ufahamu , ugunduzi na upangaji wa mambo maalumu yataakiwayo.
2.Habari ziwe fupi.
3.Taarifa na maneno muhimu tu ndiyo yanayohitajika.
4.Habari ieleweke, isipoteze kiini chake.
5.Hoja na mawazo yaungane ,yafuatane na yachukuane.
6.Sentensi ziwe kamili.

**HATUA ZA KUFUATA KATIKA UFUPISHO** .
1. Soma habari yote mpaka uilewe.
2. Chagua taarifa na maneno maalumu.
3. Linganisha taarifa muhimu na habari ya asili
4. Andika muhtasari kama ilivyotakiwa
5. Linganisha usawa wa ufipisho na habari ya asili.

(c) Agenda

Agenda ni mambo yanayozungumzwa katika mkutano baada ya mkutano, mambo yanayojadiliwa katika kila agenda ni sharti yaandikwe kwa muhtasari kwa kila agenda mwandishi hutakiwa aoneshe kama agenda hiyo ilikubaliwa au kukataliwa

(d) Kufungua mkutano

Mwenyekiti alishafungua mkutano, mwandishi aandike saa ya kufungua kikao na muhtasari wa yale yaliyozungumzwa.

(e) Kufunga mkutano


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Baada ya majadiliano ya agenda, mwenyekiti afunge mkutano. Mwandishi aandike muda au wakati kikao kilipofungwa. Kumbukumbu hizo zitiwe saini na mwenyekiti na katibu.

Muundo wa uandishi kumbukumbu za mkutano

- Kichwa

- Mahudhurio

- Agenda

  - Kufungua mkutano
  - Uchaguzi wa kamati ya maandalizi ya mahafali
  - Mengineyo
  - Kufunga mkutano

Kama Mkutano utafanywa kwa mara ya pili au zaidi muandishi hanabudi kuzingatia vipengele vifuatavyo: -

(a) Kusoma na kuthibitisha kumbukumbu

(b) Yatokanayo na kumbukumbu

**KUSOMA NA KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU**

Baada ya kufungua mkutano, kumbukumbu za mkutano uliopita husomwa na kuthibitishwa kuwa ni za kweli kisha mwenyekiti na katibu hutia saini.

**YATOKANAYO NA KUMBUKUMBU**

Haya ni mambo yaliyojadiliwa mkutanoni kutokana na mkutano uliopita.

Baada ya kusoma kumbukumbu na kuthibitisha wajumbe hujadili mambo yaliyoamuliwa na kutekelezwa maelezo kuhusu utekelezaji kutolewa na uamuzi mwingine kufanywa.

**UFAHAMU.**

Ni ile hali ya kujua na kuelewa jambo na kuweza kulifafanua au kutoa taarifa zaidi zinazohusiana na habari au jambo hilo.

**AINA ZA UFAHAMU.**

1. Ufahamu wa kusikiliza
2. Ufahamu wa kusoma.

**UFAHAMU WA KUSIKILIZA.**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Huu ni ule ambao mhusika anapata taarifa kwa kutumia masikio (Taarifa hiyo inaweza kuwa ya kusimuliwa au kusomewa)
Ili kupata habari iliyosikilizwa au iliyosomwa lazima msikilizajiazingatie mambo yafuatayo:
i. Kuwa makini kwa kile kinachosimuliwa au kinachosomwa
ii.Kuhusisha mambo muhimu na habari isimuliwayo.
iii.Kujua matamshi ya mzungumzaji
iv.Kubaini mawazo makuu
Katika ufahamu wa kusikiliza , msikilizaji hana budi kuwa katika hali ya utulivu.yaani mawazo yote yanatakiwa yae katika jambo analosilkiliza ili asipitwe na neno lolote.

**Muundo wa mara ya pili**

- Kichwa
- Mahudhurio
- Kusoma na kuthibitisha kumbukumbu
- Yatokanayo na kumbuklumbu
- Mengineyo
- Kufunga mkutano.

**UFAHAMU WA KUSOMA:**
Huu ni uelewa unaopatikana kwa njia ya kusoma .Msomaji huzingatia maana za maneno,sentensi na habari yote.
Msomaji pia huweza kutambua mpangilo wa herufi ,maneno na tarakimu na kuzitofautisha,huweza kueleza maana ya misemo na nahau kulingana na jinsi zilivyotumiwa katika habari hiyo.
Msomaji hubainisha mawazo makuu ,maana ya maneno na misemo na kujibu maswali yatokanayo na habari aliyoisoma.

**UFAHAMU WA KUSOMA HUPATIKANA KWA NJIA YA:**
-Kusoma kwa sauti
-Kusoma kwa haraka na kimya
-Kusoma kwa makini

**KUSOMA KWA SAUTI**.
Ni aina ya usomaji ambao humwezesha msomaji kupata ujumbe nakuweza kutamka kwa lafudhi ya kiswahili sahihi.

**KUSOMA KWA KIMYA.**


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Ni njia ambayo msomaji anapitisha macho kwenye maandishi kwanharaka bila mazingatio ya kina .Lengo la usomaji huu ni kupata maana ya jumla na si ya undani

**KUSOMA KWA MAKINI.**
Huu ni usomaji wa kimya ambao msomaji huvuta fikra zake zote kwa kile anachokisoma.

**UPIMAJI WA UFAHAMU**.
Ili kujua kwamba kilichosomwa kinaeleweka msomaji hupewa maswali.Akijibu kwa usahihi inaonesha ameelewa ,akijibu vibaya huonesha hajaelewa.

**KUBAINISHA MAWAZO MAKUU.**
Mwandishi au msimulizi akizungumza huwa ana ujumbe anaotaka uwafikie watu.

---

# ITABU TEULE VYA FASIHI

## RIWAYA

**RIWAYA: WATOTO WA MAMA NTILIE**

**MWANDISHI : EMMANUEL MBOGO**

**Utangulizi :**

Watoto wa mama Ntilie ni riwaya iliyotungwa na mwandishi maarufu wa riwaya na tamthilia Emmanuel Mbogo na kuchapishwa na Heko Publishers Ltd Mwaka 2002. Ni riwaya inayochambua kwa kina adha wazipatazo watoto wa mama ntilie. Hawa wametapakaa mjini huku wakifanya biashara ya kuuza vyakula ili kutafuta chochote cha kuwawezesha kutunza familia zao.

Mwandishi hapa anatueleza kuwa wakina mama hawa wanaishi maisha magumu. Watoto wao ambao wangewasaidia hapo mbeleni hawapati elimu kutokana na kukosa mahitaji muhimu ya shule, matokeo yake wanajiingiza katika matendo maovu ikiwa ni pamoja na matumizi ya madawa ya kulevya, uvutaji bangi na ujambazi.

**MAUDHUI**
Mama ntilie: Ni riwaya ambayo imesheheni maudhui ambayo kimsingi yanazungukia maisha ya mama ntilie na familia zao kama sehemu ya walala hoi waishio katika miji na vitongoji mbalimbali hapa nchini. Katika


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

riwaya hii mwandishi amejadili dhamira mbalimbali na kutoa ujumbe mzito katika jamii na dhamira hizo ni kama zifuatazo.

**DHAMIRA**

Dhamira zilizojitokeza katika Riwaya hii ni kama vile suala la umaskini, elimu, mapenzi, malezi, ujambazi, nafasi ya mwanamke, ulevi wa pombe n.k.

Dhamira zilizojitokeza katika riwaya hii ni kati ya hizi zifuatazo:

1. **UMASKINI**

Hili ni suala ambalo limeongelewa kwa kiasi kikubwa katika Riwaya hii, takribani wahusika wote waliozungumzaiwa katika riwaya hii ni maskini. Tukiwaangalia Mama ntilie na familia yake tunaona kwamba katika familia hii maisha hayawezi kwenda bila mama ntilie kwenda kwenye biashara zake za kupika chakula. Katika genge lake la Urafiki (UK.14) kilichopatikana kuishia tumboni.

Ni Umaskini huu pia uliwakabili Dotto na Kurwa watoto mapacha walioachwa yatima baada ya wazazi na walezi wao kufariki (UK54). Ni hali hii ya Umaskini iliyowakabili Dotto na Dani kwa kufanya wizi ambao uliwagharimu maisha yao yote (UK.43-47)

Pamoja na mipango mizuri ya serikali katika kuondoa umaskini. Mbogo anatueleza kwamba hakuna jipya bado watu wanaishi katika lindi la Umaskinini ambayo ilidhirishwa na wahusika Kurwa, Dotto, Peter na watu wengine wengi wakubwa kwa watoto wanaopigana vikumbo kule dampo.(UK.26). Mwandishi anasema:

“ watu waliosongamana! Kupigania mchele, wengine walikuwa na vikapu, wengine magunia.

2. **SUALA LA ELIMU**

Elimu ni kitu muhimu kwa watoto kama taifa linataka kuendelea hapa watoto kutoka familia maskini bado hawana uhakika wa kupata elimu licha ya porojo mwandishi anawasaili watoto wa shule ya msingi Makurumla na mwalimu wao mkuu Chikoya. Mwandishi anasema:

“Wote ambao hamna ada na sare hakuna shule! Nisizione sura zenu bila ada na sare. Waambie wazazi wenu hivyo” (UK.1)

Hapa tunaona kuwa kumfukuza mtoto shule eti kosa hana Ada au Sare ya


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

shule ni kunyima mtoto haki yake ya msingi ya kusoma.
Mwandishi anatueleza kuwa Peter alipenda sana shule, pamoja na kufukuzwa shule alijitahidi kutafuta Ada na Sare za shule ilikuweza kurudi shuleni (UK.9) hata hivyo ndoto yake haikutimia umaskini ulimkaba mpaka akashindwa kufurukuta.

3. **SUALA LA MALEZI**

Riwaya hii imejadili suala hili kwa kina kwa kutumia wahusika Musa, Dani, Dotto na Kurwa, Peter na Zita. Hapa mwandishi anaonyesha umuhimu wa kuwa wazazi wote wawili. Musa katika Riwaya hii hana baba (UK,17) amelelewa na mama tu hali kadhalika Dani (UK38). Hali ni mbaya zaidi kwa Doto na kurwa kwani hawana wazazi wala walezi mambo ni tofauti kwa watoto wa mama ntilie Zita na Peter pamoja na maisha Duni wanayoishi lakini hawakujiingiza katika uovu.

4. **NAFASI YA MWANAMKE KATIKA JAMII**

Mwandishi wa kitabu cha Watoto wa mama ntilie amechora mwanamke kama ni mhimili wa kiuchumi na kijamii katika familia. Mfano ni mama Zita na Peter alikuwa akiuza chakula na kuweza kuwahudumia watoto wake.

Kwa wale wanawake walioajiriwa katika kazi za kijungujiko na pengine zinazowadhalilisha kama vile uuzaji baa, kazi anayoifanya Zenabu (UK5.na 29). Ni ukweli usiopingika kwamba asilimia kubwa ya wafanyakazi wa baa ni wanawake.

Hapa wanawake wamesawiriwa kama watu wenye huruma na roho ya kupenda kutoa msaada.

Wanawake watatu wametumiwa na mwandishi kujadili suala hili kama Jane, rafiki yake Mama Kurwa huyu aliwahurumia watoto wa marehemu na aliwatunza hadi kifo chake(UK37)
Mwingine ni Kurwa aliyemhurumia Peter wakati Doto amempiga na mwenye huruma ni Zenabu.

5. **ULEVI**

Dhamira hii pia imejitokeza katika riwaya hii ya watoto wa mama ntilie. Mwandishi anelezea habari za mzee Lomolomo, mlevi wa chang'aa mataputapu na gongo (UK10,70,71,72) hapa kwa kutumia mzee

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Lomolomo, Emmanuel Mbogo anaisawiri barabara jamii ya Tanzania kuwa badala ya kuthamini familia na kazi wao wanaendekezeka pombe.

6. **WIZI, UJAMBAZI NA BIASHARA YA MADAWA YA KULEVYA**

Hapa mwandishi anelezea jinsi wizi, ujambazi na biashara ya madawa ya kulevya ilivyo haribu watoto, vijana wengi wamechora kwa kukimbilia vitendo hivi vichafu kama suluhisho la umaskini unaowakabili: Mfano Dani kwa kukosa malezi anaamua kujiingiza katika wizi (UK.38) mwingine ni Doto na dada yake Kurwa. Walifanya mpango na kwenda kuvamia duka la Rhemtula (UK40-43).

Wahusika wengine waliojihusisha na mambo ya wizi na ujambazi ni Dotto pamoja na Kurwa

Matokeo ya ujambazi huo yalipelekea kuuwawa kwa Dani na Dotto (UK.45) Mwandishi anatuelezea namna walivyouwawa:

"Paa! Paa! Bastola ililia, Mlinzi Simango alifyatua bastola. Kivuli cha juu kilitoa ukulele wa uchungu "Aaa!" kikadondoka chini."

"Kivuli cha chini hakikuzubaa, kilitumia mbio kama swala, chaa!

"Wapi! Simango alilenga Paa! Paa! Paa! Mara tatu Kurwa alisikia tena sauti ya uchungu "Aaa!"(UK.45)

7. **MAPENZI**

Mhusika Peter ndie anayeiwakilisha dhamira ya mapenzi ya kweli dhidi ya binti Kurwa. Hapa pamoja na misukosuko aliyoipata Peter toka kwa dada yake (Zita) Piter hakusita kuonyesha dhamira yake ya kusaidia kurwa.

"Tungoje mama arudi, lakini siwezi------ hatuwezi kumfukuza, tukamwacha ateseke tu huko mitaani(UK.65)

**MIGOGORO**

Migogoro kadhaa imejidhihirisha katika Riwaya hii hivyo si mingi sana ikilinganishwa na kazi nyingine za mwandishi kama vile Tone la Mwisho ngoma ya ng'wanamalundi, Giza limeingia ambazo ni tamdhilia. Migororo takribani yote ni ya akina Siye, wao kwa wao.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Mfano kuna mgogoro kati ya Doto na Peter

Mgogoro kati ya Zita na Kurwa.

Mwandishi pia amefaulu kujenga mgogoro wa nafsi Kurwa anachora akiwa na mgogoro wa nafsi, Anawaza juu ya maisha yake na namna alivyokosa mapenzi ya wazazi baada ya kuwaona watoto wawili wakipita na mama yao.

**MAFUNZO NA MAADILI**

Mwandishi wa watoto wa mama ntilie ni mwalimu na mwandishi wa jamii.

**Kwanza** : tunapata ujumbe kwamba uhalifu haulipi mema, ndivyo ilivyo tokea kwa wahusika Dani, Doto, Musa na Peter.

- Wakati Dani na Doto wanapoteza maisha, Musa na peter wanaishia jela.

**Pili** : tunapata ujumbe kwamba si vizuri kuwafukuza watoto shule eti kwa sababu ya kukosa Karo au Sare maana wao hawaba hatia katika hilo.

**Tatu:** Akina mama ntilie wana kazi nzito ya kulea taifa la kesho, hivyo jamii lazima iwasaidie katika kuubeba mzigo huo.

**Nne:** Pia ujumbe mwingine ni kwamba ulevi si kitu kizuri mf. Mzee Lomolomo.

**Tano** : Mwisho watoto yatima wanahitaji msaada katika jamii.

**FANI**

Wahusika wa riwaya ya watoto wa mama ntilie wanaweza kugawanywa katika makundi mawili ya wahusuka wakuu a wasaidizi. Wahusika wa kuu wanajitokeza tanngu mwanzo mwa hadidhi hadi mwisho.

**WAHUSIKA:**

**Mama ntilie (mama Zita)**


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Huyu ni mke wa mzee Lomolomo

**Mzee Lomolomo**

Mumewe mama ntilie na baba yao Zita na Peter

**Peter**

Ni mototo wa kiume wa mama ntilie

**Zita**

Ni mototo mwiingine wa mzee Lomolomo na mama ntilie

**Mwalimu chikoya**

Ni mwalimu mkuu wa shule ya msingi makurumla

**Doto na Kurwa**

Hawa ni watoto mapacha hawakumjua baba yao

**Zenabu**

Msichana rafiki na jirani wa mama ntilie

**Musa**

Ni mmoja wa wanfunzi waliofukuzwa makurumla

**MUUNDO**

Visa katika riwaya ya watoto wa mama ntilie vinaelezwa kwa namna ya kurukiana

**MTINDO**

Mwandishi ametumia zaidi nafsi ya tatu, umoja na wingi. Huu ni mtindo wa kawaida na uliozoeleka. Aidha kuna matumizi ya nafsi ya kwanza nay a pili katika vipengele vichache tu vinavyotumia dialogia.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Aidha mwandishi ametumia mtindo wa kifasihi simulizi, mtindo ambao unajitokeza katika matumizi ya nyimbo mbalimbali.

## MATUMIZI YA LUGHA

Riwaya ya mama ntilie imeandikewa katika luhga ya moja kwa moja na inayoeleweka kwa walengwa

## MANDHARI

Watoto wa mama ntilie ina mandhari ya jiji la Dar es salaam. Mitaa ya jiji mfano kisutu kiwanda cha Urafiki, Manzese, shule ya msingi Makurumla, dampo la Tabata n.k. Ni kwamba kwa wasomaji walio kwishafika jijini Dar es salaam watakuwa wanapata picha ya maeneo hayo.

## TAMTHILIYA

**Jina la Kitabu: ORODHA**

**Mwandishi: STEVE REYNOLDS**

**Wachapishaji: MACMILLAN**

**Mwaka: 2006**

## (a) PITIO LA KITABU

Orodha ni tamthiliya ambayo inaonyesho moja na onyesho lenyewe lina sehemu ishirini (20).

### Sehemu ya kwanza

Inaanza kwa kuonyesha vifani vinne vimeganda. Kifani cha kwanza, wahusika wameganda katika mikao inayotambulisha wasifu wa wahusika. Kifani cha pili kinaonesha wagonjwa wakiwa katika mateso. Kifani cha tatu kinaonesha wahusika wakiwa katika maumivu makali sana.

### Sehemu ya pili

Ni siku ya msiba wa Furaha. Padri James yupo Kwa ajili ya mazishi. Mama

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

yake Furaha anaeleza umati wa watu kuwa Furaha aliacha barua yenye orodha. Mama Furaha anaomba asome hiyo barua.
Anasema, ningependa kusema maneno machache kuhusu Furaha, binti yangu aliyetutoka."Padri James anajaribu kumzuia mama Furaha asiseme yale aliyoombwa na Furaha enzi za ugonjwa wake.

Padri James anasema, 'Mama Furaha, ninapinga! Haya ni majishi na wala si onyesho la pembeni la futuhi! Hapa si mahali pa..." (uk. 3)
Habari za uwepo wa barua yenye orodha inaleta hofu kwa watu wengi kijijini. Kwa mfano, Bw.Ecko anakiri hili kwa kusema,
"Lazima nikiri nina wasiwasi kuhusu maudhui ya hiyo barua..."

**Sehemu ya tatu**
Sehemu hii inatuonyesha maisha ya familia ya Furaha. Baba yake Furaha akiwa anasubiri chakula anatoa maelekezo kwa Furaha kuwaelekeza wadogo zake ili wafahamu tabia njema. Baba hafurahishwi na mwenendo wa mwanae Furaha na kumtamkia maneno mabaya. Anamuonya kuwa kwa mwenendo alionao hatapata mtu wa kumuoa isipokuwa "Washamba wa kule baa."

**Sehemu ya nne**
Chumbani kwa furaha na ndugu zake wamelala kwenye kitanda kimoja. Wamejifunika shuka moja. Mary anasikika akimwamsha Furaha watoroke. Dada mdogo wa Furaha anaamka na kumshitukiza dada yake (Furaha) kuwa anataka kutoroka kwenda kwa wanaume. Anatishiwa na Furaha kuwa akimwambia mtu atamchinja.

**Sehemu ya tano**
Mary na Furaha wanaingia baa, wanawakuta jamaa zao Ecko na Juma. Wanakunywa na kucheza. Anaona pombe ile ni chungu kwake. Mary anamshauri Furaha anywe na awe mwema kwa Ecko. Maana atamnunulia vitu vingi.

**Sehemu ya sita**
Furaha amekwenda kuungama dhambi zake kwa padri James. Alikunywa pombe na kukutana na wanaume hivyo alikuwa na dhambi za kutubu. Padri James anamshauri Furaha aje kesho yake saa moja usiku katika chumba chake cha kujisomea, nyuma ya nyumba ya kanisa. Padri anamueleza Furaha kuwa mlango utakuwa wazi na taa zitakuwa


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

zimezimwa kuficha utambulisho.
Furaha alifika kama alivyoagizwa. Padri anashikwa na tamaa za mwili na kuarnua kumliwaza Furaha. Ni ungamo ambalo analikiri.

**Sehemu ya saba**
Baba Furaha anakabiliana na Furaha sebuleni. Anamuonya Furaha kuhusu ulevi na umalaya. Furaha anaomba msamaha kwa baba yake. Mama Furaha naye anamuonya Furaha na kumtahadharisha.

**Sehemu ya nane**
Kitunda anasikiliza muziki. Furaha naye anaungana naye. Alikuwa ametumwa sokoni na mama yake. Wanazungumzia maisha ya Dar-es-Salaam. Furaha anababaika sana anaposikia kuhusu uzuri wa maisha ya Dar-es-Salaam. Kitunda anajaribu kumshawishi Furaha kuvuta bangi. Hata hivyo Furaha hakubali.

**Sehemu ya tisa**
Salimu anaingia kijijini kutoka Dar-es-Salaam. Alikuwa huko kwa muda wa miaka miwili. Wanakutana na Mary, habari zinamfikia Furaha. Salimu na Furaha ni wapenzi wa siku nyingi. Furaha akiwa na wasiwasi wa kuachwa na mchumba wake wa zamani (Salimu), Salimu anaingia nyumbani kwa Furaha.

**Sehemu ya kumi**
Salimu na Furaha wanakutana na kusalimiana. Wanaulizana mambo yaliyopita na kuelezea hatima ya mahusiano yao.

**Sehemu ya kumi na moja**
Wanakijiji wanazungumzia ujio wa Salimu. Wanazungumzia pia mahusiano ya Salimu na Furaha. Wanakijiji wanasikitishwa na tabia ya umalaya wa Furaha. Wanaionea huruma familia ya Furaha. Wankijiji wanamtaarifu mama Furaha kuhusu mwenendo wa mwanae.

**Sehemu ya kumi na mbili**
Mama Furaha anaamua kumuuliza Furaha ili kupata ukweli. Furaha anakataa kukiri tuhuma. Hata hivyo, hali yake inaonekana kudhoofu kwa kuumwa kikohozi na magonjwa mengine. Mama yake anahofu hali ya mwanae. Kwake hicho hakikua kikohozi tu, homa, malengelenge mwili mzima, mitoki, kupungua uzito kwa kasi, kukohoa damu, malaria vilimpa wasiwasi kuhusu afya ya mwanae.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**Sehemu ya kumi na tatu**

Furaha yupo sebuleni kapiga magoti akisali. Baba yake Furaha anamhoji mwanae Furaha kuhusu afya yake. Anamweleza binti yake kuwa ahakikishe ameolewa na Salimu.

**Sehemu ya kumi na nne**

Hali ya Furaha inazidi kuwa mbaya. Mama yake anaamua kumpeleka kwa daktari kuchukua vipimo vya damu. Furaha anagundulika ana UKIMWI. Mama Furaha pia anamuuliza Furaha kama amewahi kulala (kuternbea) na Salimu. Mama furaha anamweleza bintiye njia kuu zinazotumika kueneza UKIMWI.

**Sehemu ya kumi na tano**

Wanakijiji wanaeneza habari za ugonjwa wa Furaha wanajadili namna mtu anaweza kuupata ugonjwa huo. Habari za kuwepo kwa orodha iliyoandaliwa na Furaha zinazagaa na kuleta hofu kijijini hapo. Bw.Ecko, Salimu, padri James, Juma na Kitunda wana wasiwasi na mambo mawili:

(i) Kuambukizwa UKIMWI

(ii) Majina yao kuwa katika orodha hiyo.

**Sehemu ya kumi na sita**

Salimu anamtembelea Furaha baada ya kutoonana muda mrefu. Furaha anamweleza Salimu kuwa amekuwa mgonjwa muda mrefu kiasi hawezi kusimama. Salimu anamueleza Furaha kuhusu maneno anayosikia mtaani hususani hiyo barua yenye orodha. Furaha anaamua kumueleza Salimu kuwa ana UKIMWI. Salimu anachanganyikiwa na kudhani kuwa kaambukizwa. Hata hivyo anajipa moyo kwa kuwa wakati wote wamekuwa wakitumia kondom. Salimu anahitaji kuiona hiyo barua na mama Furaha anaingilia kati kuwa hapaswi kumtendea hivyo Furaha. Mama Furaha anamtia moyo Furaha na Furaha analala usingizi wa milele (amekufa).

**Sehemu ya kumi na nane**

Padri James anaomba radhi kwa lugha yake ya maudhi. Anawapa pole kwa msiba. Mama Furaha anamweleza padri James kuwa Furaha aliacha barua ambayo ingepaswa kusomwa siku ya mazishi. Padri James anaomba kuiona kwanza kabla hajairuhusu isomwe. Mama Furaha

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

anakataa kumpatia. Anaachwa sebuleni peke yake. Padri James anatumia nafasi hiyo kuitafuta barua bila mafanikio.

**Sehemu ya kumi na tisa**

Ni asubuhi ya siku ya mazishi. Ecko, Juma na Salimu wanaonekana wakitafakari namna ya kuhakikisha barua haisomwi wakati wa mazishi ya Furaha. Hata hivyo wanashindwa kupata namna sahihi ya kutekeleza azima yao.

**Sehemu ya ishirini**

Kwenye mazishi, Mama Furaha anaapa kuwa ukweli ni lazima isomwe katika umati huo. Padri James anapingana na mama Furaha kuhusu kuisoma barua hiyo. Mama Furaha anamuonya Padri James kuwa hana la kuficha.

Salimu anatoka katika kundi la watu na kumpora mama Furaha orodha na kuichanachana katika vipande. Mama Furaha anakasirishwa na hilo. Hata hivyo inasomwa barua hiyo ambayo inaelezea mambo yaliyochangia kifo chake na namna kijiji kinachopaswa kuchukua tahadhari na ugonjwa huo kwa kuelezea mambo 10 ili kuepukana na ugonjwa huo.

**1. Maudhui**

*Orodha* ni tamthiliya ya tanzia — ramsa ambayo inachambua tatizo la UKIMWI katika sehemu za vijijini katika bara la Afrika. Ni tamthiliya ambayo inajaribu kutumia mazingira halisi ya vijiji vyetu vya kiafrika, mila na desturi za kiafrika ili kuweza kueleza namna ugonjwa huu unavyotafuna maisha ya watu wengi barani Afrika na kwingineko. Mwandishi anajaribu kuonesha umuhimu wa kutambua uzito wa tatizo hili katika mazingira ya kijijini ambalo hawaelewi vizuri kuhusu tatizo hili.

Mwandishi wa tamthiliya anapevuka zaidi katika namna ya kulielezea tatizo ambalo waandishi wengine wamepata kulieleza. Kupitia Furaha na Mama Furaha mwandishi anajaribu kuvunja ukimya na kuamua kueleza mambo ya msingi ya kuzingatia katika mapambano haya ya kutokomeza gonjwa hili hatari la UKIMWI. Mwandishi anaorodhesha mambo hayo kuwa ni:

(a) Matumizi ya Kondomu.

(b) Utoaji wa elimu sahihi.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

(c) Uelewa wa tatizo na watu wenye tatizo hill iii kuepuka unyanyapaa.

(d) Uwazi wa kuzungumzia tatizo lenyewe.

(e) Uadilifu wa watu wote katika jamii.

(f) Uwajibikaji kwa jamii nzima kwa nafasi tulizonazo.

(g) Ukweli ill kutuweka huru.

(h) Upendo ndani ya jamii ili kuepusha ukuaji wa tatizo na pia kuwatia moyo waathirika.

(i) Msamaha ni muhimu ili tusihukumu wala kuwa na visasi kwa walioathirika na ambao hawajaathirika.

Kwa ujumla, mwandishi amezungumzia namna watu wanavyopata maambukizi, dalili na hatua za kuchukua ili kupambana na ugonjwa hatari wa UKIMWI.

**DHAMIRA ZINAZOJITOKEZA**
**Dhamira Kuu: Mapambano Dhidi ya Ugonjwa wa Ukimwi**
Tamthiliya hii ya Orodha inahusu UGONJWA WA UKIMWI. Mwandishi amekusudia kutoa taarifa muhimu kuhusu ugonjwa hatari wa UKIMWI. Katika utangulizi wake mwandishi anasema: *"Wazo langu la msingi lilikuwa kuchunguza mazingira ya msichana wa kijijini anayekufa kwa* UKIMWI..., Orodha ni kichekesho na wakati huohuo ni tamthiliya ya kielimu kwa wale wasiojua VVU/UKIMWI."

Kwa hakika mwandishi anatumia ucheshi kuelezea tanzia kubwa tuliyonayo ndani ya jamii zetu. Tanzia ambayo imeletwa na ugonjwa huu hatari wa UKIMWI. Dhamira hii kuu ya UKIMWI imeelezwa kwa namna ambayo watu wanaelimishwa kuhusu mambo hayo yanaweza kuwekwa katika makundi yafuatayo:

- Ukosefu wa elimu sahihi kuhusu VVU/UKIMWI.

- Umaskini.

- Mmonyoko wa maadili, kutowajibika na kutokuwa waadilifu.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

-  Kukosekana kwa uwazi, ukweli na upendo.

Mwandishi anaona kuwa mambo hayo, ndio kiini cha tatizo hili la ugonjwa wa UKIMWI. Ili jamii inusurike na janga hili, hatuna budi kuzingatia:

- Ngono salama
- Uadilifu
- aminifu
- Uwajibikaji
- elimu
- Ukweli
- welewa
- Upendo
- uwazi
- Msamaha.

Katika waraka aliouacha Furaha kabla hajaaga dunia anasema,

*Kwa kijiji changu kipendwa. Nawashukuru kwa kufika kwenu na kuyasikiliza maneno yangu ya mwisho. Msiogope, kwani nadhani maneno haya yanaweza kuwasaidia. Katika hii miezi ya mwisho nimelala kitandani nikifa nikizidi kuugua. Nilipata muda mwingi wa kufikiri, kubadilika, kukua kama mtu: Hata ninapokuwa nakufa. Katika ukurasa unaofuata kuna orodha ya vitu ambavyo vilisaidia kuyafupisha maisha yangu, orodha ambayo inaonesha kwenu nyote ukweli juu ya kifo changu …..Kondom, uadilifu, elimu,*

*welewa, uwazi, uadilifu, uwajibikaji, ukweli, upendo na msamaha... ukosefu wa mambo yote haya ndio ulioniua. Ufuatiliaji wa mambo yote haya unaweza kuwaokoa ninyi nyote..."(uk 44 - 45).*

Kwa ujumla, dhamira ambazo zinajenga dhamira kuu ni pamoja na hizi zifuatazo:

(a)  Umaskini

(b)  Kukosekana kwa elimu/ujinga

(c)  Dhana potofu

(d)  Mmomonyoko wa maadili

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

(e) Unafiki

(f) Mapenzi na ndoa

(g) Ukosefu wa huduma za afya

(h) Unyanyapaa

(i) Uwazi wa ukweli

(j) Kukosekana kwa uadilifu na kutowajibika

Kuondolewa kwa mambo hayo hapo juu, kutatusaidia sana katika mapambano yetu dhidi ya tatizo hili la UKIMWI.

**(a) Umaskini:**

Hii ni hali ya mtu au jamii kukosa uwezo wa kupata uhitaji katika maisha yao ya kila siku. Kwa neno jingine, hufahamika kama `ufukara.' Katika tamthiliya hii, mwandishi anabainisha kuwa umasikini ni moja ya vyanzo vikuu vinavyofanya wasichana kutumbukia katika mambo yasiyofaa kama ulevi na umalaya. Hivyo, huwa ni vigumu kufanya maamuzi yenye busara ya kujilinda na maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Haya yanajitokeza pale Mary anaposema:

*"(Akimvuta Furaha kando) Nimekwambia hawa jamaa ni burudani.... hata yule mshamba Juma. Sikia, pata burudani na kuwa mwema, kwa Ecko. Anaweza kukununulia vitu vingi sana! Unadhani wasichana wadogo kijijini hapa wanapataje viatu vipya, magauni na mabegi mapya ili wapendeze... wapendeze kiasi cha kuwavutia vijana wazuri wa kiume?-" (uk. 7 — 8).*

Mwandishi anaonesha kuwa jamii ya kijijini sehemu kubwa ina watu wasiojiweza kiuchumi. Kutokana na hilo, wasichana hujirahisisha kwa wanaume wenye pesa ili wapate pesa za kupata mahitaji yao muhimu kama vile nguo, mabegi na viatu vipya.

Mwandishi wanaona kuwa vita dhidi ya UKIMWI iende sambamba na ukombozi wa kiuchumi. Vinginevyo mtu ambaye hajajikomboa kiuchumi huwa na nafasi ndogo sana ya kujilinda na maadui kama maradhi na ujinga.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

***(b)*** **Kukosekana kwa elimu/ujinga**

Elimu ni maarifa yanayomsaidia mtu kupambana na maisha. Mtu asipokuwa na elimu siku zote huwa ni mjinga wa mambo mbalimbali. Mwandishi wa tamthiliya hii ameonesha kuwa kikwazo kingine cha vita dhidi ya ukimwi ni ujinga (kukosekana kwa..elimu). Mwandishi anaona kuwa elimu ya ukimwi inapaswa kutolewa kwa watu wa vijijini. Watu wanapaswa kuelewa ukimwi ni nini? Unaambukizwa kwa njia zipi? Matibabu yake yakoje (dawa za kurefusha maisha)? Mtu anaweza kuepuka vipi? Je, wagonjwa wahudumiwe vipi katika vipindi vyote vya ugonjwa huu, n.k.

Katika kijiji ambacho Furaha alikuwa akiishi inaonekana watu wengi hawafahamu vyema kuhusu Ukimwi. Ukweli wa hoja hii unaweza kuthibitishwa na mazungumzo ya wanakijiji.-

Mwanakijiji wa1: *Ndio, lakini katika ofisi ya daktari kaambiwa ana huu ugonjwa wa AIDS!*

Mwanakijiji wa 4: *Hicho si kitu kizuri*

Mwanakijiji wa 1: *Wanauita slim kwa sababu ugonjwa wenyewe hukufanya ukondeane.*

mwanakijiji wa 3: *Lakini anawezaje kuupata ugonjwa kama huo!*

Mwanakijiji wa 1: *Rahisi! Kuna mtu kamroga...*

Mwanakijiji wa 2: *Nasikia unaupata kwa kugusa tu!*

Mwanakijiji wa 4: *Au hata kwa kuiva nao katika chumba kimoja!*

Mazungumzo ya wanakijiji hawa yanadhihilisha wanakijiji wengi hawafahamu njia zinazosababisha maambukizo. Wanadhani ugonjwa wa Ukimwi unaambukizwa kwa kurogwa, kugusana na mtu mwenye virusi na kwa njia ya hewa. Haya ni mawazo potofu na yanachangia kuzorotesha mapambano. Ili tuweze kutokomeza gonjwa hili hatari ni lazima wananchi wapewe elimu sahihi na endelevu kuhusu ugonjwa wa ukimwi na virusi vya ukimwi.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

### *(c)* Mmomonyoko wa maadili

Hii ni hali ya kuporomoka kwa mwenendo mwema ndani ya jarnii ambapo hutokana na jamii kutokuzingatia mafundisho na maonyo mema katika jamii. Baadhi ya maadili mema ni pamoja na kuepuka kufanya mambo yanayokatazwa na jamii kama vile ulevi, uvutaji wa bangi, uzinzi, uasherati na umalaya.

Mwandishi wa tamthiliva hii anaonesha kutoridhika na namna jamii inavyomomonyoka kimaadili. Mwanclishi anaona kuwa mmomonyoko wa maadili ni chanzo kingine kinachochangia kuenea kwa ukimwi na hivyo kufanya vita hii kuwa ngumu. Kwa mfano; Furaha na Mery wanashindwa kuzingatia mwenendo ulio mwema na badala yake, wanajiingiza katika ulevi na umalaya ambao unapelekeaFuraha kufa kwa UKIMWI. Haya yanaweza kuthibitishwa kutoka katika kitabu
pale baba anapomsura mwanae Furaha;

"*Nilichokuwa nafahamu.. hadi sasa Furaha…ni kwamba umekuwa ukitoroka*

*nyumbani wakati wa usiku wa manane!.. kutoroka... bila ruhusa!.baa... wanaume...*

*wewe... Malaya usiye na shukurani!" (uk 11).*

Mwandishi pia anaona kuwa si wasichana tu ndio hawazingatii maadili mema pia hata watu ambao wameaminiwa na jamii kuwa viongozi wa kusimamia maadili mema. Bila woga mwandishi anabainisha kuwa hata viongozi wa dini sasa wamepoteza mwelekeo na mwenendo mwema. Mfano mzuri ni Padri James.

Badala ya Furaha kuona ametenda dhambi anaamua kwenda kuungama dhambi zake ili arejee katika tabia yake njema. Badala ya kumsaidia kiroho, Padri James anatumia nafasi yake kumrubuni Furaha na kufanya ngono katika chumba cha kusomea. Padri James nasema; (uk. 10).

*"Furaha alikuja kama alivyoagizwa na...ee...Ekaristi Takatifu ikapatikana. Lazima uelewe jinsi ilivyo vigumu kwa mtu wa hadhi yangu na wadhifa*


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

*wangu. Kuna shinikizo kubwa, vishawishi vingi! Kwa watu hawa, mimi ndie padri wao... lakini mimi pia ni mwanadamu! Mahitaji yote haya ya mwanadamu: Peke yangu katika jumuiya hii.*

*Nafanya kile niwezacho kufanya... na bado, kwangu yaelekea kwamba alikwisha bikiriwa, kwa hiyo ingeleta tofauti gani? Nilidhani pengine hata ningeliweza kumliwaza? Lakini mtu lazima awe mwangalifu... katika jumuiya ndogo namna hii... taarifa husafiri... wakati wowote ……kitu fulani huropokwa".*

Kwa ujumla, kuporomoka kwa maadili katika jamii ni tatizo au kikwazo katika mapambano dhidi ya UKIMWI.

**(d) Mapenzi na ndoa**

Hii ni dhamira nyingine ambayo imejadiliwa katika tamthiliya hii ya Orodha. Mwandishi anaona kuwa mapenzi yasiyo ya dhati katika ndoa na katika jamii kwa ujumla ni kikwazo kikubwa kwenye mapambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI. Mapenzi yasiyo ya dhati hupelekea watu wasiwe waaminifu kwa wenzi wao. Mfano mzuri ni Bw. Ecko. Hakuwa na mapenzi ya dhati kwa mkewe na matokeo yake yeye mwenyewe Bw. Ecko na mkewe wapo katika hatari ya maambukizo ya virusi vya UKIMWI. Mazungumzo ya Bw. Juma na Ecko yanashadidia maelezo haya:

*Bw. Ecko: Kwa kweli! Najaribu kukinusuru kijiji hiki kutokana na aibu.*

*Bw. Juma: Bila kumtaja mkeo!*

*Bw. Ecko: Nimesema bila kumtaja!*

*Bw. Juma: Hivyo ndivyo niliyosema. Bila kumtaja! Sasa, hiyo orodha iko mapi?... (uk. 32).*

Hofu ya orodha inamfanya Bw. Ecko aisake hiyo barua kwani anajua alishamsaliti mkewe na kwamba hata hiyo orodha alidhani itakuwa na jina lake kama mtajwa au muathirika. Laiti Bw. Ecko angekuwa na mapenzi ya dhati angemlinda mkewe kwa kutoisaliti ndoa yake. Vilevile mapenzi yasiyo


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

ya dhati yamejitokeza kati ya Furaha na Bw. Ecko, Mapenzi yao yaliegemea kwenye pesa na vitu. Furaha alifanyamapenzi na bwana Ecko ili kupata pesa na vitu kama ambavyo rafiki yake, Mary alivvomtanabaisha;

*"...kuwa mwema, kwa Ecko. Anaweza kukununulia vitu vingi sana! Unadhani wasichana wanapataje viatu vipya, magauni na mabegi mapya..."*

Furaha na wasichana wengi wa kijijini walijali zaidi vitu na fedha badala ya mapenzi ya dhati. Matokeo yake wanaishia kuambukizwa ugonjwa wa UKIMWI na kufanya vita dhidi ya UKIMWI kuwa ngumu zaidi.

***(e)*** **Ukosefu wa huduma za afya.**

Kijijini maisha ya watu yanapotea kwa sababu huduma za afya zipo mbali sana. Maisha ya waathirika yanahitaji huduma za afya ziwe bora na karibu na pale walipo. Huduma za afya zinazoelezwa hapa ni pamoja na utoaji wa elimu ya afya inayohusu magonjwa hatari kama malaria, kifua kikuu, saratani ya uzazi na UKIMWI, Upimaji wa magonjwa hayo, Matibabu na kuwashirikisha wananchi katika mapambano ya UKIMWI. Huduma hizi zote hazipatikani kwa urahisi kijijini.Haya yanaweza kuthibitishwa na mama Furaha anaposema,

*"Kadri muda ulipoendelea, ndiyo Furaha alivyozidi kukondeana,:.. Furaha alikuwa kadhoofika mno hakuweza kuinuka kitandani. Daktarii kutoka mji wa karibu alifika na kuchukua sampuli ya damu ili kupima malaria. Mzee wa kijiji alifika na dawa zake zauganga. Daktari wa mjini alirudi. Alitaka ampeleke Furaha kwenye hospitali ya karibu... "(uk.23).*

Hii inathibitisha kuwa kijijini hakuna huduma za afya na hili ni tatizo kubwa katika mpambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI na maradhi mengine ambayo ni nyemelezi.

***(f)*** **Uwazi na ukweli**


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Hii ni dhamira ambayo inajaribu kuonesha umuhimu wa watu kuwa wazi na wa kweli ili kutoa msukumo na mtazamo mpya kuhusu vita hii dhidi ya UKIMWI.

Msanii anaona kuwa umefika wakati wa kuwa wakweli na wawazi kama kweli tuna nia ya kutokomezaUKIMWI. Katika hali ya kejeli, ucheshi anatumia "orodha" ambayo itabaini ukweli. Ukweli upi? Hiki ni kitendawili kinachowasumbua wanakijiji Bw. Ecko, Salim, Juma na Padre wanajaribu kila namna kuona wanaipata orodha hiyo ili kuficha ukweli. Wanadhani ni orodha ya majina ya watu waliotembea na Furaha. Mathalani Padri James anapopinga waziwazi kuhusu kusoma hiyo orodha, mama Furaha anamjibu:

*"Hakika, Padri; Wewe huna la kuficha!"*

Ingawa mama Furaha anaongea na Padri James lakini matumizi ya wewe yanatugusa sote. Hatuna jambo la kuficha Ni lazima tuvunje ukimya. Tuzungumze mambo yote yanayohusu ugonjwa huu ili kunusuru watu wetu. Siyo ukweli huo tu peke yake, Furaha anapoelewa tatizo linalomsumbua anaamua kueleza ukweli kuhusu tatizo alilonalo. Anaamua kumueleza Salim na wanakijiji wote. .‘anasema,

*" nina ukimwi, Salim" (uk.29)*

Kwa kutaka jamii yake isiangamie, Furaha anaamua kusema ukweli kuhusu mambo yote yajiyochangia kuangamiza maisha yake. Anakuwa muwazi kwa kuandika barua ambayo ndiyo inabeba dhamira kuu ya mchezo huu. Furaha anasema yafuatayo katika barua yake,

*"...Kondomu, uaminifu, elimu, welewa, uwazi, uadilifu, uwajibikaji, ukweli, upendo na msamaha... ukosefu wa mambo yote baya ndio ulioniua. Ufuatiliaji wa mambo yote haya unaweza kuwaokoa ninyi nyote... wanusuruni watu wetu...wanusuruni watoto wetu ili wasiwe yatima. Muinusuru Afrika... yetu nzuri!"*

Ni maneno mazito sana. Furaha anakuwa muwazi na mkweli ili kunusuru jarnii yake na Afrika nzima. Anatambua madhara ya UKIMWI kwa jamii. Haoni sababu ya kuficha. Kwa hakika ukweli huleta uhuru. Ukweli na uwazi utasaidia sana katika mapambano yetu dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

### *(g)* Kukosekana kwa uadilifu na kutowajibika

Katika jamii kuna watu ambao wanapewa dhamana mbalimbali ili kuiongoza jamii katika nyanja mbalimbali. Watu wenye dhamana wanapaswa kuwa mfano mzuri. Wanategemewa kuiongoza jamii katika njia iliyo sahihi.

Mwandishi anaonekana kukerwa sana namna viongozi na watumishi wengine kutokuwa waadilifu katika nafasi walizopewa ndani ya jamii. Kutokuwa waadilifu kwa jamii zao kunakwamisha,vita ya maadui watatu ambao ni maradhi, umaskini na ujinga.

Mwandishi anamtumia Padri James kama mfano wa watu wasio waadilifu katika jamii. Padri James alipaswa kuwa mstari wa mbele kuwatahadharisha kuacha kuzini, kulewa na maovu mengine badala yake yeye kama Padri anashindwa kutambua nafasi yake katika jamii kwa kujihusisha na mambo machafu kama uasherati. Padri James aliweza kufanya ufuska wake katika nyumba takatifu ya Mungu. Huu ni ukosefu wa maadili. Padri James anasema,

*"Furaha alikuja kama alivyoagizwa...ee...Ekaristi takatifu ilipatikana lazima uelewe jinsi ilivyo vigumu kwa mtu wa hadhi yangu na wadhifa wangu"(uk.10).*

Baada ya kufanya ufuksa Padri James anaeleza na namna ilivyo ngumu kwa mtu wa wadhifa na hadhi yake kufanya uchafu kama alioufanya. Vita dhidi ya UKIMWI inahitaji watu kuwa waadilifu vinginevyo jamii nzima itaangamia kwa UKIMWI.

### *(h)* Upendo

Hii ni hali ya kuhusudu kitu, mtu kwa moyo wako katika nyakati mbalimbali bila kujali matatizo yatakayojitokeza. Kitu au mtu kuwa ndani ya moyo wako kwa kuwa unakuwa umetoa nafasi hiyo. Upendo ni silaha kubwa sana katika vita hii dhidi ya UKIMWI. Uwepo wa upendo ndani ya jamii utasaidia kulea wagonjwa wa UKIMWI na watoto yatima waliopoteza wazazi wao kwa UKIMWI. Mfano mzuri ni mama Furaha. Huyu ni mtu


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

ambaye alionesha upendo kwa Furaha katika kipindi chote cha ugonjwa wake hadi kumfia mikononi mwake. Haya yanajitokeza katika ukurasa 30.

*Furaha:Mimi...mimi sikuwa mtoto mzuri wakati wote, mama.*

Mama Furaha: *(akicheka). Mimi pia, mwanangu! Hakuna mtu aliye kamili. Lakini uliwaangalia wadogo zako. Na kila mahali ulipokuwapo, kulikuwa na nuru ya jua!*
*Ulikuwa binti mzuri………binti yangu mzuri…. (Furaha analegea wakati akiongea). Inaelekea kana kwamba umezaliwa Jana tu. Na wakati huo ulizidikufanya nisubiri,*

*wakati nikiwa na mimba yako. Nakumbuka jinsi ilivyookua, ukikimbia, shambani mwetu, ukijaribu sana kumfurahisha baba yako...unajua, anakujali kwa namna yake...(ananyamaza kidogo wakati akimtazama Furaha ambaye ananyong'onyea mikononi mwake, Analia). Amelala sasa... lala mwanangu.*

Upendo wa namna hii unapaswa kuoneshwa kwa wagonjwa wote.

Furaha pia anaonekana kuonesha upendo kwa kijiji chake anapoamua kuandika barua ya wosia ili kuwaepusha watu na ugonjwa huu. Furaha anaanza barua yake kwa kusema;

*"Kwa kijiji changu kipendwa" Haya ni meneno ambayo yanaeleza hisia zake kwa kijiji  chake.*

*Anaeleza mambo muhimuya kuzingatia*. Anaendelea kusema,

*"Ukosefu wa mambo vote haya ndio uloniua. Ufuatiliaji wa mambo yote haya unaweza kuwaokoa ninyi nyote".*

Furaha anamaliza baua yake kwa kusema,

*"Wenu awapendae, Furaha."*

Hakika Furaha ni msichana ambaye anaonekana alikuwa na upendo na watu wote kwa kusema,

*"Chukueni orodha yangu na muinakili. Ipelekeni kwenye vijiji vingine, miji mingine na*


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

*mengine katika hii nchi yetu Wanusuruni watu wetu ili waweze kuyafaidi maisha kikamikfu. Wanusuruni watoto wetu ili wasiwe yatima. Mwinusuru Aftika...Afrikayetu nzuri!"*

Ni barua inayobaini upendo na uzalendo kwa nchi yake. Kwa upendo alionao ameamua kuokoa jamii nzima, anapigana vita dhidi ya UKIMWI kwa kutoa elimu kwa jamii. Upendo ni silaha ya kupambana na unyanyapaa na UKIMWI kwa ujumla.

**(i) Ulevi**

Katika tamthiliya hii ya Orodha, tunaambiwa kuwa ulevi ni tatizo kubwa na ndiyo chanzo kikubwa cha watu kushindwa kujitawala. Msanii anaeleza kuwa watu wanapokuwa wamelewa huwa na maamuzi mabaya ambayo huleta majuto baadaye. Katika kuonesha ulevi ni kikwanzo kikubwa katika mapambano dhidi ya UKIMWI anatuonesha wahusika, Furaha, Bw. Ecko, Bw. Juma na Mery kuwa walikuwa walevi na matokeo yake wakaangukia katika uzinzi na uasherati ambao unaleta majuto makubwa. Hebu tumwone mhusika mkuu jinsi ulevi ulivyomletea matatizo.

Baba: Hakudhamiria nini? Kweli, ulidhani kwamba, ungaliweza kikficha hiyo siri yako ndogo!

Furaha: Siri yangu ndo...unajua pombe?

Baba: Pombe!

Mama Furaha: Pombe!
Furaha: Ndiyo, kule baa!

Mwandishi anaonesha kuwa Furaha alijiingiza katika ulevi na ndivo ikawa chanzo cha yeye kujiingiza katika umalaya ambao unamsababishia kupata ugonjwa wa UKIMWI. Bw. Ecko anathibitisha hill kwa kusema,

*"Jambo baya zaidi; Hakika? Tuseme tu kwamba hata tulipofika kwenye 'chumba changu cha ukapera' nyumba yangu ya pili tulikuwa tumelewa chakari, hasa!.."*

Kwa ujumla ulevi wa aina voyote huwa na madhara makubwa katika mfumo wa ufahamu wa binadamu na matokeo yake ni kushindwa kutoa


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

maamuzi sahihi na kushindwa kujitawala. Mwandishi anaonesha kuwa ni kikwanzo kikubwa katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI.

**(j) Malezi**

Mwandishi anajaribu kuonesha jamii kuwa malezi ni suala ambalo linapaswa kuangaliwa upya. Malezi kwa watoto yanapaswa kuzingatiwa na jamii nzima badala ya kuachia wazazi. Msanii anaonesha namna wazazi wa Furaha walivyojaribu kumlea mtoto wao kwa namna iliyo njema. Furaha alipobadilika mwenendo wake wazazi walimkalisha chini na kumkanya. Kwa mfano. Baba yake Furaha anasema,

*"Furaha! Wewe unategemewa kuwaongota watoto hawa. Hawaelekei kufahamu tabia njema hapa nyumbani!"*

Hii inaonesha namna ushirikiano unavyotakiwa katika suala zima la malezi ndani ya familia au nje ya familia. Baba anaamua kushirikisha Furaha katika malezi ya wadogo zake. Vilevile, mtoto hakui kwa wazazi wake. Baba anapoona mwenendo wa Furaha pia sio mzuri, anaamua kuongea na mama yake anasema,

Baba: *Huyu msichana hatafanikiwa chochote maishani. Nina hakika bado hajafanya aliyopewa shuleni! Siku hizi hata hasaidii shambani kama alivyokuwa akifanya zamani.*

Mama: *Nafahamu, mpenzi:  Hata sijui nifatye nini?... wacha  niongee naye....Nadhani yuko katika umri ambao...*

Baba: *Ni afadhali ufanye hivyo: vinginego, hapa  kijijini hakuna mtu atakayetaka kumwoa! Ila tu kwa wale ambao ni washamba wa kule baa!*

Hata hivyo malezi ya wazazi na ndugu tu hayatoshi bali jamii nzima inapaswa kushirikiana kuwaweka vijana katika mwenendo ambao unastahili. Mwandishi anaonekana kusikitishwa na tabia ya baadhi ya watu badala ya kusaidia kuelekeza njia sahihi baadhi ya vijana badala yake huwapotosha. Mwandishi anatumia Padri James, Bw. Ecko na Bw Juma kuwa ni mfano mbaya katika jamii kwani wao wameshiriki kuwapotosha na kuwaharibu vijana kama vile Furaha na Mery.

Jamii inapaswa kushirikiana katika malezi ya watoto ill kuwaepusha katika janga hili la ukimwi kwa ujumla.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

## 2. Ujumbe

Ujumbe tunaoupata kutoka kwenye tamthiliya hii ya orodha ni pamoja na:

**(i)** Asiyesikia la mamaye hufunzwa na ulimwengu. Furaha ni msichana ambaye alikuwa akikaidi ushauri na wazazi wake wote wawili kuwa mwenendo alionao sasa haufai lakini yeye akakaidi. Matokeo yake alijikuta ameambukizwa virusi vya UKIMWI na kumsababishia mateso ya mwili kwa kuumwa muda mrefu hadi mauti yalipomkuta. Tunapaswa kufanyia kazi ushauri muhimu unaohusu maisha yetu kwa ujumla ili kuepuka madhara makubwa.

**(ii)** Tamaa mbele mauti nyuma. Tamaa za kutaka kupata fedha na vitu mbalimbali harakaharaka vilimtokea puani Furaha. Furaha alishawishika kujiingiza kwenye umalaya ili apate vitu vizuri. Matokeo ya tamaa zake ni kupata ukimwi.

**(iii)** Ulevi ni chanzo cha matatizo. Furaha alikuwa ni msichana mwenye maadili mema. Mara baada ya kuanza kujiingiza kwenye ulevi ndipo matatizo mengi yalianza kuibuka. Alipewa majina mabaya, alikosana na wazazi na hatimaye kufa kwa UKIMWI.

**(iv)** Elimu ni silaha muhimu katika mapambano dhidi ya ukimwi. Elimu humkomboa mtu katika giza na kumpeleka katika nuru. Elimu ndogo kuhusu ukimwi ndiyo chanzo cha kushindwa kujikinga na maambukizi. Elimu sahihi ndio njia muhimu ya kuwaokoa watu katika hatari ya maambukizi ya virusi vya ukimwi na ugonjwa wa UKIMWI.

**(v)** Kondomu, Uaminifu, uadilifu, ukweli, upendo na uwajibikaji ndiyo mambo muhimu ya msingi ya kuzingatia ili kuiokoa jamii katika janga hili la ugonjwa huu hatari wa UKIMWI

**(vi)** Umasikini, ulevi, na makundi yasiyofaa ni chanzo cha uchochezi wa uhalifu wa maisha ya vijana kama Furaha hivyo hufanya watu watumbukie katika matatizo makubwa yakiwemo madawa ya kulevya kama ilivyo kwa kitunda na umalaya kama ilivyo kwa Furaha na Mery. Ili tupige vita dhidi ya UKIMWI tunapaswa kupambana na umasikini, ulevi na makundi mabaya katika jamii.

## 3. Migogoro


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Ifuatayo ndiyo migogoro iliyojitokeza katika tamthiliya hii ya orodha:

**(i)** Mgogoro kati ya mama Furaha na Padri James kuhusu kusoma orodha aliyoandika Furaha. Padri James anampinga mama Furaha kusoma orodha hiyo. Mama Furaha anamuonya Padri James kuwa hana cha kuficha hivyo aliisoma hiyo barua kwa nguvu. (uk. 3 na 43).

**(ii)** Mgogoro kati ya Furaha na dada mdogo. Katika harakati za kutoroka usiku kwenda baa. Dada mdogo hapendenzwi na tabia hiyo na kumtishia kumsemea kwa mama yao. Mvutano huo unaisha kwa Furaha kumtishia kumchinja mdogo ikiwa atatimiza azma yake ya kumsemea kwa mama. (uk.6)

**(iii)** Mgogoro kati ya Baba na Furaha kuhusu kutoroka bila ya ruhusa ya wazazi na Pia kujihusisha na ulevi na umalaya. Suluhisho la mgogoro huu ni baba kumpiga mwanae na kumuonya kwa maneno makali. (uk.10 — 12).

**(iv)** Mgogoro kati ya mama Furaha na Salim kuhusu orodha. Salim hakubaliani na uamuzi wa mama Furaha na kulazimika kupora orodha na kuichana vipande. Suluhisho ni mama Furaha kunikumbusha fadhila za Furaha kwa Salim nakuamua kusoma karatasi iliyobaki na kuokota vipande vile na kuviunganisha na kusoma orodha. (uk. 43-44).

**(v)** Mgogoro kati ya Salim na Furaha kuhusu orodha. Salim analazimishwa apewe orodha hiyo aisome kwanza lakini Furaha anakataa na kumueleza kuwa itabidi asubiri. Wanarushiana maneno yenye visa hadi mama Furaha anaingia na kuamuru Salim atoke nje na aaende zake.

**(vi)** Mgogoro wa kinjisia uliomo ndani ya Salim, Ecko, Padri James na Juma. Kila mmoja alitembea na Furaha na wanasikia kuna orodha wanaingiwa na hofu ya majina yao kuwepo au kuambukizwa UKIMWI. Kila mmoja anaamua kuondoa hofu hiyo kwa kwenda kuisaka orodha hiyo bila mafanikio. Wanajaribu kuleta hila iii isisomwe lakini wanashindwa. Inaposomwa wanagundua haikuwa orodha ya majina yao. (uk. 31-45).

**4. Msimamo wa mwandishi**

Mwandishi wa tamthiliya ya Orodha anamsirnamo wa kiyakinifu. Amechambua ugonjwa wa ukimwi kwa jicho la kipembuzi bila ya kuficha jambo. Amejadili mitazamo ya watu wa kijiji kuhusu ufahamu wao kuhusu


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

ukimwi na changamoto mbalimbali zilizopo katika nchi zinazoendelea hususani nchi za kiafrika kuhusu suala zima la UKIMWI.

Mwandishi amebainisha kuwa ukosefu wa konndomu vijijini, uadilifu, Elimu, uelewa, uwazi, uwajibikaji, ukweli, upendo na msamaha ndiyo huchangia vifo vya watu wengi. Vilevile mwandishi anaona kuwa ufuatiliaji wa mambo haya na usambazaji wa mambo haya sehemu mbalimbali ndio itakuwa njia sahihi za kutokomeza ukimwi na madhara yake kwa ujumla. Anasema ujumbe huu ndiyo iwe barua kwa wote ili kuokoa kizazi hiki.

**5. Falsafa ya mwandishi**

Mwandishi wa tamthiliya hii anaelekea kuamini kuwa ukweli, uwazi na uadilifu ni mambo muhimu sana katika jamii inayotishiwa na majanga makubwa kama ya UKIMWI. Sehemu kubwa ya wahusika amewaumba kwa namna ya kuonyesha namna ya kukabili ukweli na kuwa wazi. Wapo wahusika wamefanikiwa kwa hilo akiwemo Furaha na mama Furaha, wapo wahusika wanaoshindwa au kuwa na hofu. Mfano. Bw. Ecko, Salim na Bwana Juma.

**6. Fani**

**(a) Muundo**

Mwandishi wa tamthiliya ya orodha ameweza kuweka kazi yake yote katika onyesho moja. Onyesho hili lina jumla ya sehemu ishirini (uk. 20).

Mpangilio wa visa na matukio kwa ujumla ni changamano. Sehemu ya kwanza na ya pili inazungumzia matukio ya siku ya mazishi ya Furaha. Sehemu ya tatu hadi ya kumi na sita (16) inazungumzia maisha ya Furaha hadi kifo chake. Sehemu ya 17 hadi 19 inahusu mzozo wa uwepo wa orodha aliyoandika Furaha enzi za uhai wake. Sehemu hizi zinazungumzia harakati za kuitafuta barua hiyo kwa udi na uvumba bila mafanikio. Sehemu ya ishirini inahusu mazishi na usomaji wa barua yenye orodha na na mchezo unaishia hapo.

Kwa ufupi muundo ni changamano kwa kuwa sehemu ya 1-2 ni mazishi na 3-20 ni moja kwa moja yaani mwandishi kaanza na kifo cha Furaha sehemu ya kwanza na pili halafu maisha ya Furaha hadi kifo na mazishi yamejitokeza kwa mtiririko wa moja kwa moja kuanzia sehemu ya 3-20.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**(b) Mtindo**

Mtindo ambao umetumika ni dayolojia. Mwandishi ametumia mtindo wa majibizano kwa kiasi kikubwa katika kazi yake. Ni sehemu chache sana mwandishi ametumia monolojia (uk. 10) Padri James nasema;

*"Furaha alikuja kama alivyoagizwa na.........ee.. Ekaristi takatifu ilipakana. Lazima uelewe jinsi ilivyo vigumu kwa mtu wa hadhi yangu na wadhifa wangu. Kuna shinikizo*

*kubwa, vishawishi vingi! Kwa watu hawa, mimi ndiye Padri wao... lakini mimi pia ni mwanadamu! Mahitaji yote haya ya mwanadamu peke yangu katika jumuiya hii.*

*Nafanya kile niwezacho kufanya... na bado, kwangu,yaelekea kwamba..."*

Huu ni mfano to wa matumizi ya monolojia. Padri James alikuwa akizungumza peke yake kabla ya kuondoka. Sehemu nyingine ambazo mwandishi ametumia monolojia ni uk 23, 37, 39, 40, n.k. Kuna matumizi ya barua ambayo ndiyo imebeba ujumbe wa mwandishi. Barua hiyo inapatikana(uk. 44 — 45). Barua yenyewe inasomeka hivi;

*"Kwa kijiji changu kipendwa;*

*Nawashukuru kwa kufika kwenu na kuyasikiliza maneno yangu ya mwisho. Msiogope, kwani nadhani maneno haya yanameza kuwasaidia. Katika hii miezi ya mwisho nimelala kitandani nikifa, nikizidi kuugua.*

*Nilipata muda mwingi wa kufikiri, kubadilika, kukua kama mtu; hata ninapokuwa nakufa. Katika ukurasa unaofuata kuna orodha ya vitu ambago vilisaidia kuyafupisha maisha yangu. Orodha ambayo inaonyesha kwenu nyote ukweli juu ya kifo changu. Mama tafadhali wasomee watu wote orodha hii.*
*Uepukaji*

*Uaminfu*

*Elimu*

*Welewa*


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/ Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

*Uwazi*

*Uadilifu*

*Uwajibikaji*

*Ukweli*

*Upendo*

*Msamaha*

*Ukosefu wa mambo yote haya ndio ulioniua. Ufuatiliaji wa mambo yote haya unaweza kuwaokoa ninyi nyote. Chukueni orodha yangu na muinakili. Ipelekeni kwenye vijiji vingine, miji mingine na majiji mengine katika hii nchi yetu nzuri. Wanusuruni watoto wetu ili wasiwe yatima. Muinusuru Afrika....Afrika yetu nzuri!*

*Kwa kijiji changu, kiishi maisha marefu na kiwe na furaha! Msinihukumu mapema mno. Kwa mama, baba na ndugu zangu nawapenda. Jaribuni kuwa wenye furaha na muishi maisha ya furaha wakati mnaweza kufanya hivyo!*

*Wenu awapendaye, Furaha".*

Matumizi ya barua hii katika tamthiliya unaleta athari kubwa sana kwani ni kumbukumbu tosha na ni wosia kwa watu wote ili kuwaepusho na ukimwi. Mwandishi ametumia nafasi zote tatu. Nafsi ya pili imetawala sana kwa sababu mwandishi ametumia mtindo wa dayolojia.

Mifano:

(i) Nafsi ya II

**Mama Furaha:** *Unathubutuje, Salim?... (uk.44).*

(ii) Nafsi ya III

**Mama Furaha;...** *Kabla hajafa alitaka nimwahidi kumfanyia kitu Fulani; Hapo kwenye mazishi. Ingawaje alikuwa na maumivu na mateso... (uk. 43).*



Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

(iii) Nafsi ya I

**Salim:** *nilikuwa na shughuli nyingi.......Nikijijenga katika kazi yangu mpya ya ualimu... na sikuwa na muda wa kumwona Furaha kwa muda... (uk.27).*

Pia mwandishi ametumia mtindo wa lugha ya mtaani ili kuakisi lugha ya watu wa mtaani, kijiweni na lugha ya mateja.

Mfano:

**Kitunda:** *Mshikaji, poa! Unaweza kuniamini: tunaweza kutazama picha, kusikiliza muziki ....unaweza hata kuvuta ganja langu kidogo, mwanangu.*

**Furaha:** *Kuvuta nini lako...? (Anarudi nyuma)*

**Kitunda:** *Mezea, mtoto, lazima ujifune lugha za mitaani vinginevyo Dar kutakuwa noma tu! Mwanangu! Ni kwamba unaweza kujaribu majani... manjuani! (uk. 14).*

**(c) Wahusika**

Mwandishi ameweza kuumba wahusika ambao wameweza kudhibiti nafasi zao. Wahusika ambao amewatumia ni Furaha, Mama Furaha, Baba, Mary, Bw. Chaka, Ecko, Bw. Juma, Padri James, Kitunda, Salim, Wanakijiji, Daktari na Dada mdogo.

Wasifu wa wahusika katika tamthiliya ya Orodha

**(i) Furaha**

- Huyu ni msichana wa mri wa kati ya miaka 13-19.
- Ndiye mhusika mkuu katika tamthiliya hii.
- Ni msichana asiye na msimamo thabiti kwani aliweza kuyumbishwa kwa urahisi na Mary.
- Ni muathirika wa ugonjwa wa UKIMWI.
- Ni mkweli.
- Ni muwazi.
- Ni malaya.
- Ni mlevi.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Mhusika huyu anafaa kuigwa kwa uwazi na ukweli kuhusu ugonjwa wa UKIMWI.

Hafai kuigwa kuhusu tabia ya umalaya na ulevi.

**(ii)** ***Mama Furaha***

- Huyu ni mama mzazi wa Furaha.
- Ni mchapakazi.
- Ni mpole.
- Ni mama mwenye upendo.
- Ni mkweli.
- Ni muwazi.
- Ana msimamo.

Anafaa kuigwa katika jamii kwani ni mama asiyetetereka katika ulezi wa watoto na familia nzima.

**(iii)** ***Baba***

- Ni baba mzazi wa Furaha.
- Ni mkali.
- Ana upendo.

Ana lugha kali kwa wanawe

***(iv) Mary***

- Ni msichana.
- Ni rafiki yake Furaha.
- Ni malaya.
- Ni mlevi.

Hafai kuigwa na jamii.

**(v)** ***Bw. Ecko***

- Ni mwanaume mtu mzima.
- Ni mfanyabiashara.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- Ni mlevi.
- Ni mzinzi.
- Si muadilifu au mwaminifu kwenye ndoa yake.
- Anatamaa.
- Ni muathirika wa ukimwi.

Hafai kuigwa na katika jamii.

**(vi) *Bw. Juma***

- Ni mwanaume mtu mzima.
- Ni rafiki yake Bw. Ecko.
- Ni mlevi.
- Ni mzinzi.
- Ni mtu mwenye tama.
- Ana lugha chafu.

Hafai kuigwa na jamii.

**(vii) *Padri James***

- Ni mtumishi wa Mungu katika kanisa la katoliki.
- Ana cheo cha upadri.
- Si muadilifu.
- Ni dhaifu kwa wanawake.
- Anaweza kuwa muathirika wa UKIMWI.
- Si mkweli.

Hafai kuigwa na

**(viii) *Kitunda***

- Ni kijana wa mtaani.
- Ni mlevi.
- Ni mvuta bangi.
- Ni mhuni.
- Ana lugha ya kihuni.

**(ix) *Salim***

- Ni kijana wa kiume.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- Ni rafiki wa kiume wa Furaha.
- Ni msomi.
- Anaweza kuwa muathirika wa UKIMWI japokuwa alitumia Kondomu baadhi ya siku alizokutana na Furaha.
- Si mtu adilifu.
- Si muwazi.
- Si mkweli.

**(x) *Wanakijiji 1-3***

- Ni wanakijiji wa kijiji cha akina Furaha.
- Ni majirani wa wahusika wengine.
- Ni marafiki wa Kitunda.
- Ni watu wasiokuwa na ufahamu kuhusu UKIMWI.
- Wana dhana potofu.
- Ni wambea.

**(xi) *Dada mdogo***

- Huyu ni ndugu wa kike wa Furaha.
- Ni mdogo kwa umri.
- Ni mwoga.
- Hapandezwi na nyendo za dada yake.

***(xii) Daktari***

- Ni mtaalamu wa afya kutoka mjini.
- Ndiye alichukua sampli ya damu.
- Ni mchapa kazi.

Uainishaji wa Wahusika katika tamthiliya ya Orodha.

Wahusika katika tamthiliya ya Orodha wamegawanyika katika ma kundi makuu matatu:

(a) Wahusika wakuu.

(b) Wahusika wasaidizi au wadogo.

(c) Wahusika wajenzi.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Katika tamthiliya ya Orodha ina mhusika mkuu mmoja tu ambaye ni Furaha. Huyu ndiye anayejitokeza toka sehemu ya 1-20. Mhusika huyu ndiye kabeba dhamira kuu ya mchezo huu. Dhamira kuu ni UKIMWI na ni mhusika pekee aliyekufa kwa UKIMWI.

Wahusika wasaidizi ni: Mama Furaha, Bw. Ecko, Bw. Juma, Padri James, Mary, Salimu, Baba na Kitunda. Hawa ni wahusika ambao wametumika kumjenga mhusika mkuu. Wahusika hawa wamebeba dhamira ndogondogo zisizojenga dhamira kuu.

Kwa mfano:

(i) Mama Furaha - dhamira ya upendo, ukweli na uwazi

(ii) Padri James - uadilifu na Uwajibikaji

(iii) Salim - elimu

(iv)  Bw.Ecko, Bw. Juma - ulevi, uaminifu, n.k.

Wahusika wajenzi ni Dada mdogo, Daktari na  Mzee wa kijiji wahusika hawa wamejitokeza ama mara moja au wametajwa tu. Ukiondoa Dada mdogo ambaye amejitokeza kama mara mbili katika ukurasa wa 5 na 6 wahusika wengine wametajwa tu na wahusika wengine ukurasa wa 23, 24 na 25.

***(d) Matumizi ya Lugha***

Lugha iliyotumika ni ya kawaida, inaeleweka na imeshahenezwa kwa kiasi fulani tamathali za semi na mbinu nyingine za kisanaa.

**(i) *Misemo/Nahau***

Misemo/ iliyotumika katika tamthiliya hii ni kama ifuatayo:

- *"Shuga dadi "...* (uk. 6) unamaanisha wanaume wenye umri mkubwa wanaopenda kutembea (kufanya mahusiano ya kimapenzi na wasichana wadogo wa umri wa binti zao).

- *"Mshamba"....* ark. 7) ni mtu ambaye hajui mambo mengi ya mjini au mambo ya kileo.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- *Furaha anavuna mbegu ya kifo aliyoipanda.....(uk. 27).* Kuvuna mbegu ni msemo unaomaanisha kupata kitu kutokana na matendo uliyotenda. Ni msemo unatokana na msemo usemao *"Utavuna ulichopanda".*

**(ii) *Misimu***

Mwandishi ametumia lugha ya misimu kuweza kutambulisha mhusika. Misimu iliyotumika ni ile ya mtaani au misimu ya vijana katika vijiwe. Lugha hii imtumika (uk. 12-14). ni mazungumzo ya kitunda na Furaha.

Mifano ya misimu:

- Mshikaji — (uk 12, 13, 14)

- Bomba mchizi — (uk .13)

- Poa — (uk. 14)

- Ganja — (uk. 14)

- Majani — (uk. 14)

- Nitakulinda — (uk.14)

- Mwanangu — (uk. 14)

- Kuvinjari— (uk.14)

Haya ni maneno yanayotumika mtaani, hususani hutumiwa na vijana wa vijiweni katika miji. Maneno hayo yana maana zifuatazo:

(i) Mshikaji — rafiki au jamaa

(ii) Bomba mchizi — sawa rafiki au ndugu

(iii) Poa — vizuri au sawa

(iv) Ganja, majani - bangi

(v) Nitakulinda - nitakusaidia

(vi) Mwanamgu — mtu wa karibu au rafiki yangu

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

(vii) Kuvinjari — kuzunguka au kutalii

**(iii) *Tamathali za Semi***

**Tashibiha:**

Katika tamthiliya hii ya *Orodha* mwandishi ametumia tashibiha chache. Tashibiha zilizotumika ni kama zifuatazo:

*"Yeye ni kama punda wa kijiji..."* (uk 18)

Mwanakijiji wa 1 alikuwa anamfananisha Furaha kuwa yuko sawa na punda ambaye kila mtu alimpanda. Tashibiha imetumika pia (uk.13) pale kitunda anapojaribu kulinganisha jiji la Dsm na lile la New York. Anasema,

*"Kisura, ni kama jiji la New York"*

Mfano mwingine wa tashibiha unapatikana (uk. 43) mwandishi anaposema,*..."vipande vinaanguka kama theluji."*

**Sitiari**

Sitiari nazo zinatumika kwa kiasi fulani kwa mfano: Baba anaposema, " nyie, *mbu wadogo ...."(uk* 4, 10)

Baba anawafananisha watoto wake na mbu wanaonyonya damu

**Mubalaagha**

Katika uandishi wake kuna maelezo ambayo mwandishi anaonekana kutia chumvi.

Kwa mfano:

"*Furaha: sijui unachokiongea. Nani aliyesema mambo hayo?*

*Mama Furaha: Nusu ya kijiji kizima...."*

Mama Furaha alipaswa kusema wengi badala yake anatia chumvi kuwa ameambiwa na watu karibu nusu ya kijiji.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**Kijembe na Kejeli**

Kejeli na vijembe vimejitokeza katika tamthiliya hii, mwandishi ametumia kuonesha bezo la dhana fulani.

*"Nieleze waewe. We ni mzee wa kutosha kuwa baba yangu!"* (uk. 7)

*"Inafurahisha kuona hufikiri i wewe mwenyewe tu."* (uk 41)

Bw. Juma alitoa kejeli hii kwa Bw. Ecko ambaye ni mbinafsi.

**Tafsida**

Kuna matumizi ya tungo ambazo zimesaidia kuficha makali ya maneno. Tafsida zimetumika sehemu kubwa ya tamthiliya. Mwandishi anaonekana kuelewa utamaduni wa Waswahili kuwa kuna baadhi ya maneno hayatajwi hadharani.

Kwa mfano:

*Mary: Hiyo ni bia yake ya mwanzo*

*Furaha: Ni chungu*

*Mary: Ladha yake utaizoea tu!*

*Bw. Juma: Kama ulivyozoea wewe, mayai yangu madogo!*

*Bw. Ecko:Unaona! Inashangaza jinsi ambavyo mtu unaizoea haraka ladha hiyo! Bw.Juma (Kwa Mary): Kama ulivyofanya wewe, mishikakiyangu*

*midogo.....(uk.* 7)

Bw. Juma anapotaja "Mayai yake madogo" na "Mishikaki midogo" anamaanisha sehemu zake za siri. Mifano mingine ya tafsida kutoka katika tamthiliya hii ni pamoja na:

**(iv) Mbinu nyingine za Kisanaa**

**Mdokezo:**

Kwa mfano:


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- *Furaha........... fur........... tuta............. (uk. 9)*

- *Ndiyo, padri.... Ni.......    (uk. 8)*

- *Misamaha, padri: Mi (uk. 36)*

*...kuendelea na.....  (uk. 39)*

- *Uepukaji............ (uk.* 44)

Mbinu hii imetumika kwa kiasi kikubwa sana katika tamthiliya hii ya *Orodha.* Mwandishi amekuwa akianza neno au maneno na kuyacha bila kumalizia.

**Takriri**

Kumekuwa na hali ya kurudiarudia, maneno au sentensi katika tamthiliya hii. Mwandishi ametumia mbinu hii kwa lengo la kuonesha msisitizo. Kwa mfano: *Padri James: ..... Hili ni jambo zito sana..... sanasana..... sana hasa....(uk.* 9).

Mwanakijiji  wa 2: Kondom

Mwanakijiji wa 3: Elimu

Mwanakijiji wa 4: Welewa

Mwanakijiji wa 1: Uwazi

Kitunda: Uadilifu

Padri James: Ukweli

Mary: Upendo

Salimu: Msamaha ........ (uk. 44).

Maneno haya yamejirudia tena (uk. 45) kwa mtiririko uleule na wahusika wale wale.

**Tanakali Sauti:**



Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Mwandishi ametumia miigo ya sauti ili kuonesha uhalisia na hisia za wahusika.

Kwa mfano:

(a) Myaau! — ( uk 33 — 34).

(b) Oooowww! — (uk . 35).

(c) Owww!........... (uk. 35).

***(v) Picha na Taswira***

Mwandishi ametumia lugha ya picha. Mfano mzuri ni matumizi ya neno "Mbu" Baba anaposema, "K*aribu nitakufa njaa hali nyie mbu wadogo mwainyonya damu yangu yote?"* (uk. 4).

"Mbu" ni neno lililotumika kuleta taswira ya utegemezi kwa njia ya kunyonya damu.

***(e) Mandhari***

Mandhari iliyotumika katika tamthiliya hii ni ya kijijini vijiji vilivyotumika ni vile vya Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla. Matukio yametokea katika viunga na barabara za vijijini, sehemu za baa na nyumbani. Kwa ujumla mwandishi ametumia mazingira ya vijijini ambako watu hawajapata elimu sahihi kuhusu ugonjwa wa UKIMWI.

***(f) Jina la Kitabu***

*Orodha* ni jina la kitabu ambacho kimetafsiriwa katika *"The List"* ambapo iliandikwa kwa kiingeraza. *Orodha* ni jina la kitabu ambalo linasadifu yaliyomo ndani ya kitabu. Ndani ya kitabu mhusika mkuu Furaha kabla ya kifo aliacha barua yenye orodha ya mambo muhimu ya kuzingatia ili kuiokoa jamii nzima kutokana na habari ya kuambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Orodha inayowachanganya watu kijijini kwani walidhani ni Orodha ya majina ya watu ambao walitembea (fanya mapenzi) na Furaha. Ni kichekesho chenye mafunzo, mambo yanayoorodheshwa ndiyo msingi wa dhamira mbali mbali zinazojenga dhamira kuu ya UKIMWI. Orodha


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

yenyewe ni kondom, uaminifu, elimu, welewa, uwazi, uadilifu, uwajibikaji, ukweli, upendo na msamaha.

Kwa hiyo jina la kitabu linasadifU yaliyomo katika kitabu kwani ndani ya kitabu kuna *"Orodha"* inavyoweza kuokoa jamii katika janga la ugonjwa wa UKIMWI.

## KUFAULU NA KUTOFAULU

### Kufaulu kwa Mwandishi

Mwandishi amefaulu kufikisha ujumbe wake kwa walengwa. Mwandishi ameweza kujadili vyema tatizo la UKIMWI kwa kutumia mazingira ya kijijni. Mwandishi ameeleza wasiwasi wake kuhusu uelewa wa watu waishio kijijini kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Lakini pia ameweza kueleza mambo ya msingi ya kuzingatia katika mapambano kwa kutumia mbinu ya waraka (barua) (yenye orodha ya mambo hayo muhimu kuzingatia). Barua ile inatumika kama wosia ambao unasomwa siku ya mazishi. Siku yenye huzuni na hofu mioyoni mwa watu ili kuleta athari ya hofu na woga kuhusu UKIMWI.

Anatumia wahusika wachache ambao hawamchanganyi msomaji. Wahusika wa rika na jinsia mbalimbali wametumika kuwasilisha mawazo ya watu mbalimbali kuhusu UKIMWI.

Kutokana na uzito wa tatizo linalojadiliwa, mwandishi amefaulu kutumia lugha inayoeleweka kwa urahisi iliyojaa ucheshi ikinyunyiziwa tamathali za semi na mbinu mbalimbali za kisanaa. Vilevile mwandishi amekuwa makini kujali utamaduni wa jamii husika kwa kutotumia lugha ya matusi na badala yake ametumia tafsida kulinda miiko ya utamaduni wetu katika kutumia lugha.

Mwandishi amefaulu pia kupangilia matukio kutokana na ukubwa wa tatizo linalozungumziwa. Mwandishi anaanza na msiba kuonyesha kuwa jambo lililopo mbele yetu ni msiba wa jamii na anamaliza sehemu ya mwisho kwa msiba kuonesha msisitizo wa dhamira kuu.

Kwa ujumla, mwandishi amefaulu kifani na kimaudhui kufikisha ujumbe aliokusudia kwa jamii.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**Kutofaulu kwa Mwandishi**

Mwandishi ameshindwa kueleza njia mbalimbali zinazoeneza UKIMWI. Toka mwanzo hadi mwisho wa kitabu mwandishi ameonesha njia moja tu ambayo ni kufanya mapenzi yasiyo salama. Hii ni muhimu ili kupunguza unyanyapaa.

Mwandishi ameshindwa kugawa kitabu katika maonyesho mbali mbali. Kitabu kizima kina onesha moja lenye sehemu ishirini. Mwandishi angeweza kuweka sehemu 20 katika maonesho matatu. Hii ingeweza kusaidia kufuatilia matukio kwa urahisi zaidi kuliko ilivyo sasa.

**Jina la Riwaya: JOKA LA MDIMU**
**Mwamfcsbi: ABDALA J.SAFARI**
**Mchapisha: JK HUDA PUBLISHERS**
**Mwaka: 2007**

**UTANGULIZI**
Riwaya ya *Joka la Mdimu* ni riwaya ambayo inaakisi vizuri matatizo ya kiuchumi ya miaka ya themanini nchini Tanzania. Riwaya hii inaaksi tu, haihakiki, hali ya maisha katika kipindi cha dhiki ya ukosefu wa bidhaa muhimu kama vile nguo, chakula, mafuta, spea za mashine, n.k. Wakati huu wa dhiki watu wengine wanateseka na kuumia, kuna wengine wachache wanaotumia nafasi zao kuchuma kadri wanavyoweza, hasa kwa njia haramu. Katika *Joka la Mdimu* vilevile wengine wanaotanafusi katika maisha yao wanakuwa hivyo kwa kupitia njia zisizo halali.

Mwandishi wa *]oka la Mdimu* anaonekana kuwa alifanya uchunguzi mkali kabla ya kuandika riwaya yake. Hii inajidhihirisha kutokana na jinsi anavyopenya katika nafsi za nje na ndani za wahusika wake, akiwapatia lugha, mavazi, vyakula, tabia na mazingira yanayochukuwana nao na ujumi wa makundi yao, na hivyo kuhalisisha uhusika wao kwa namna inavyomlidhisha msomaji. Kwa jinsi riwaya hii inavyoaridhia vizuri matukio ya kipindi cha mwanzo cha miaka themanini katika Tanzania inabeba sifa ya kuwa ni riwaya kiistiara.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**PITIO LA KITABU**

***Sehemu ya kwanza: Mindule***

Amani ambaye ni dereva wa taxi anatafakari kitandani namna ya kupata mafuta. Anaondoa gari yake ya Zalpher 6 kwake na kusaka mafuta na wateja. Mafuta ni shida kuyapata na yanapatikana kwa magendo.

Ugumu wa maisha unawafanya vijana wa kike kujitumbukiza kwenye biashara ya ukahaba na kufungua madangulo ilimradi wapate fedha za kujikimu maisha.

***Sehemu ya mbili: Tino***

Maisha ya wakazi wananchi wa Sega kwa kiasi kikubwa ni duni. Huko ndiko alikoishi Tino, mvuta kwama. Mvua kubwa kubwa inanyesha na kusababisha mafuriko. Tino anamuokoa bibi na mafuriko, anaendelea na shughuli zake za kukokota kwama na kubeba mizigo. Tunahadhithiwa kuhusu watu kukataa kulima kahawa kwani ujka wake ni mdogo. Hali ya chakula, mafuta na fedha za kigeni ni mbaya.

***Sehemuya tatu: Jinja Maloni***

Jinja Maloni analetewa taarifa kuhusu kifo cha rafiki yake mpenzi Omar Mahafudh. Anaombwa kwenda kuchimba kaburi. Marehemu alikuwa mfanyabiashara maarufu wa nguo. Jinja alikuwa mzibua vyoo pia.

Jinja Maloni anamuokoa mwanamke aliyekuwa anabakwa na wanaume wawili. Anaamua kupigana na wale wahuni ili kumuokoa yule mwanamke. Anafanikiwa kumuokoa na kumsindikiza nyumbani kwao.

***Sehemu ya nne: Sega***

Wakazi  wengi wa Sega ni waislamu. Tino naye ni mmoja wa waislamu. Ni mpenzi  wa timu ya Sega Warriors. Alichezea timu hii licha ya umri wake kusonga. Siku ya mchezo kati ya Sega Warriors na City Devils ilimpa hofu sana Tino. Viongozi wanakabidhiwa dawa ya kuleta ushindi toka kwa Sangona. Katika mchezo, huo, Sega walipata ushindi uliotokana na bao pekee lililofungwa na Tino. Amani anaamua kuwaandalia sherehe ya kuwapongeza Tino na Zitto. Wanakunywa na kula ukumbini G.V. Tino alirudi nyumbani baada ya mkesha. Alikutana na familia yake ikiwa imerudi



Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

toka safarini. Tino anabeza sherehe za uhuru wa nchi. Tino anafanya maandalizi ya Iddi El Fitri.

**Sehemu *ya Tano:Boko***

Amani anakwenda posta kuchukua barua. Anampatia Tino telegramu yake. Telegramu ilimtaarifu kuhusu kuumwa kwa Cheche. Tino anasafiri kumwona Cheche. Cheche alikuwa ameumia vibaya na amelazwa katika hospitali.

***Sehemu ya Sita: Brown Kwacha***

Amani anaendesha gari kuelekea hazina. Ndani ya gari kuna tajiri aitwae SHIRAZ BHANJ. Bhanj alikuwa anataka kumuona Mkurugenzi wa fedha za kigeni aliyeitwa
BROWN KWACHA. Brown alipenda anasa hususani ufusika na uasherati. Brown Kwacha anafanya biashara ya nyara za Serikali. Brown anakaidi kuwahudumia wageni wengine isipokuwa kwa wasichana kama vile Leila na Josephine.

Brown Kwacha ananunua viwanja 2 vya kujenga nyumba. Anafanya sherehe za kuzindua nyumba. Siri ya mahusiano mabaya kati ya Brown na mkewe inaelezwa.

***Sehemu ya Saba: Kwale***

Brown Kwacha anatoa udhuru wa kutokuwepo kazini. Anajiandaa kwa safari ya kwenda mbuga ya wanyama na Leila. Walienda hifadhi ya taifa ya KWALE. Anapanga mipango na maharamia kumletea nyara (pembe za ndovu).

***Sehemu ya Nane: Dakta Mikwala***

Hospitalini Mindule, amelazwa Cheche. Afya yake inazorota, wazazi wanajawa na simanzi. Mama yake analia, Cheche anakata tamaa ya kupona, anasema, "Mimi siponi baba" (uk. 123) Tino anampa matumaini ya kupona mwanae Cheche. Daktari Denis Kaya wa hospitali ya Manga anamshauri Tino ampeleke hospitali ya Glasgow, Uingereza. Tino na Amani wanapanga namna ya kumpata Daktari bingwa wa mifupa. Daktari Mikwala anapendekeza Cheche apelekwe Glasgow — Uingereza kwa matibabu zaidi.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

***Sehemu ya Tisa: Cheche***

Amani anakwenda ofisi ya hazina kuonana na Brown Kwacha kuhusu uwezekano wa kupata fedha za kigeni za kumtibia Cheche nje ya nchi. Taarifa kutoka kwa Brown Kwacha zinamsononesha Tino na anaonekana kukata tamaa kuambiwa kuwa zinatakiwa laki tatu na pia kulipia nusu ya gharama za matibabu ambazo zinagharimu kiasi cha milioni tano. Nyumba mbili za Kashogi zinaungua, majirani na gari la zimamoto wanasaidia bila mafanikio.

Amani ananunua bastola kwa askarijeshi mmoja. Tino na Amani wanatumia bastola hiyo katika tukio la wizi katika benki. Wanaiba milioni 20 kwa kutumia gari aina Peugeot 504. Fedha hizo zinatumika kumtibia Cheche.

***Schema ya Kumi: Moto***

Brown Kwacha analazwa katika hospitali ya rufani jijini Mindule kufuatia kuziba kwa tundu la mkojo kwa siku mbili. Brown Kwacha anapata mstuko baada ya kusoma gazeti la 'Time' lenye habari za wabunge kudai maelezo kuhusu meli ya mafuta. Daktari anamshauri Kwacha afanyiwe upasuaji katika kibofu cha mkojo.

Waziri wa fedha anafika nyumbani kwa Brown Kwacha kupata mahesabu ya matumizi ya fedha za kigeni, Brown Kwacha anamuahidi Waziri kuwa atawatuma vijana walete hayo mahesabu. Baadaye anapiga simu hazina ambako anamwita mhesabu na karani wa idara ya fedha, mazungumzo yanafanyika na Brown Kwacha anasisitiza jambo mara baada ya kuwapatia milioni thelathini.

Jengo la hazina linawaka moto, magari ya zinamamoto kutoka Halmashauri ya jiji, bandari na kikosi cha zimamoto kutoka uwanja wa ndege wa kimataifa wa Mindule kinajumuika punde tu kujaribu kuzima moto ambapo milango na madirisha ya vioo vinateketezwa, Amani anasimama mbali na jengo huku akishindwa kuamini akionacho. Siku inayofuata Brown Kwacha na familia yake wanapanda ndege kwenda Geneva kwa ajili ya matibabu mara tu mahesabu ya wizara yanapotengenezwa na kutengemaa na Bunge kuridhia. Miezi mitatu baadaye Tino, mkewe na Amani wanakwenda uwanjani kumpokea Cheche na muuguzi wake kutoka kwenye tiba Glassgow, Uingereza. Tino namkewe wanamkumbatia Cheche machozi ya furaha yakiwabubujika.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

UHAKIKI WA MAUDHUI

**Dhamira Kuu: hali ngumu ya maisha**

*Joka la Mdimu* ni riwaya inayoelezea ugumu wa maisha ambao jamii inakabiliana nao. Ugumu huu wa maisha kwa kiasi kikubwa unatokana na hali mbaya ya uchumi wa nchi. Watu masikini ni watu ambao wameathiriwa sana na ugumu wa maisha haya. Watu hawa wamekosa fedha za kujikimu katika maisha yao ya kila siku. Wananchi wanaishi katika maisha ya kijungujiko.

Watu wa kawaida ndio wanaoumia na hali mbaya ya uchumi ambayo inatokana na siasa mbaya na uongozi mbaya, uhaba wa mafuta, mfumuko wa bei, rushwa, magendo, ufisadi na kutowajibika kwa viongozi wetu.

Kutokana na kukosekana kwa mafuta, kunasababisha tatizo la usafiri kwa watu wa kawaida na kukosa mwanga kwenye nyumba zao wakati wa usiku, msanii [anasema (uk. 1).

*"Jiji la Mindule lilikabiliwa na uhaba mkubwa mno wa petroli, dizeli na mafuta ya taa,*
*Nyumba nyingi zisizo na umeme zilibaki kiza usiku, maana mishumaa ilikuwa ghali na*
*adimu kupatikana. Usafiri ulisimama isipokuwa kwa wale wachache waliojua mbinu za*
*kupata petroli na dizeli"*

Kutokana na ugumu wa maisha, usafiri ni wa taabu na matatizo mengine mengi, watu wa tabaka la chini, hata kula kwao ni kwa taabu pia. Chakula chao kikuu ni kula mahindi ya njano kama anavyosema msanii (uk. 15 — 16)

*"Aibu hii. Miaka hamsini sasa tangu tumepata uhuru kila siku kula mahindi ya njano,"*

watu wa tabaka la chini wanaoishi mjini wanakumbana na matatizo mbalimbali yanayotokana na hali ngumu ya maisha. Kutokana na hali hii, hata kazi za kufanya


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

hawachagui mradi tu wapate pesa ya kusukuma mbele maisha yao. Mfano Tino anafanyakazi ya kusuma kwama, Jinja Maloni anafanyakazi ya kuchimba makuburi  na kupakuwa vyoo (uk. 46 — 50).

Wakulima kwa upande wao vijijini nao wanakabiliwa na hii hali ngumu ya uchumi. Mazao ya biashara wanalima lakini hayawasaidii chochote kuinua hali zao za maisha, kwani wanaofaidi jasho la wakulima ni viongozi wachache. Matokeo ya yote hayo ni wakulima kuacha kulima mazao hayo ya biashara, msanii anasema.

*"Ila kwa kifupi huko atakako watu wameacha kulima kahawa kabisa. Hawataki "*

*"Kwa nini ?"*

*"Kipato kidogo, fedha yoteyenda serikalmi. Sijui tunaelewana? "*

*"Naam !kutafutafedha za kigeni kwa ajili ya hao wakubwa"*

*"Halafu hakuna anayeziona! kulima walime wao, kufaidi wafaidi wengine "*

*"Sasa wafanya nini?"*

*"Wanalima nyanya. fedha chapu chapu "* (uk. 39 — 40)

Wakati viongozi wanafaidi matunda ya mkulima, mkulima anapata matatizo makubwa sana kiasi cha kula mahindi ya njano, huku viongozi wako kwenye ziara nchi za nje na wala hawagusi mahindi ya njano kama anavyosema msanii anasema,

*"Lakini wao ziara za nje haziishi"*

*"Na wala mahindi ya njano hawayagusi"*

*"Basi waona" (uk 40)*

Hapa msanii anaonesha kuwa wakati  viongozi wanatumia pesa nyingi kwa ziara ya nchi za nje, ziara hizo zinasababisha maumivu makubwa kwa watu wa tabaka la chini. Pesa ambazo zingetumika kuinulia uchumi wa nchi, viongozi wanazitumia kwa ziara zao za nje na mambo mengine ambayo hayana faida yoyote kwa jamii.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Hali ngumu ya maisha vilevile imesababisha ubovu wa barabara zetu. Pesa kidogo zinazopatikana, badala ya kuzipeleka kwenye matengenezo ya barabara zetu zinatumika katika shughuli nyingine. Kwa upande mwingine serikali ikawa inasingizia haina hela ya kutengeneza barabara hizo, msanii anasema (uk. 81).

*Hakuna aliyejali kuyaziba mashimo hayo madogo au kama serikali ilivyodai, haikuwa na uwezo wa kufanya hivyo. Kwa jinsi hiyo mashimo yaliendelea kuwa makubwa.*

Kwa ujumla, barabara ni nyenzo muhimu sana ya kulete maendeleao katika jamii, na ubovu wa barabara hasa unalete kero kwa watu wa kawaida ambao hutegemea barabara hizo kupata mahitaji muhimu.

Vilevile msanii anaonesha kuwa *kutokana* na hali ngumu ya maisha watu wa vijijini nyumba zao na mavazi yao ni ya kusikitisha kama asemavyo msanii,

*"Hakukuwa na nyumba za maana isipokuwa kila baada ya mwendo wa nusu saa*
*walitokea kwenye vijumba viwili, vitatu au vinne vilivyojengwa kwa suti za nyasi au udongo*
*mwekundu na kuezekwa kwa nyasi, Nje yake watoto wako uchi au kuvaa vibwende vya shuka*

*za kishingoshingo, kaptura au vishati, waliangalia gari likipita" (uk* 81).
Hii ni hali ya watu wa kijijini, na huko mjini mambo ni hayohayo kwa watu wa
tabaka la chini, maisha yao ya taabu, usafiri wa taabu watu hurundikwa kwenye
mabasi kama mizigo na wengine huenda na kurudi kutoka kazini kwa mguu kuepuka adha ya kusimama vituoni kwa muda mrefu bila ya uhakika wa kupata.
usafiri (uk. 6-7).

Kwa upande wa makazi, watu wa kawaida waliishi sehemu duni na chafu sana ukilinganisha na watu wenye pesa zao. Sehemu za makazi yao ilikuwa na uchafu ulevi, ufuska na ujambazi (uk. 26). Nyuimba zao ni mbovu na mvua ikinyesha inakuwa hatari tupu kwa watu wa tabaka la chini (uk. 29 — 30).


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Hospitalini vilevile kulikuwa na huduma mbovu kutokana na hali mbaya ya uchumi. Hakuna madawa halafu huduma zinazotolewa hazifai au zinatolewa kwa rushwa. Msanii anasema,

*"Huyu mtoto hawezi  kupona hapa"*

*Tino alisema kwa kubuhuti kikubwa"*

*"Eee!" Amani  alikaa vizuri kwanini?"*

*"Hakuna tiba ya kufaa"* (uk. 126).

Wakati wenye pesa na viongozi wanakimbilia nje ya nchi kutibiwa, watu wa tabaka la chini (masikini) wanahangaika kupata huduma kwenye hospitali zetu na ili huduma itolewe lazima utoe chochote. Masikini wasio na chochote hukosa huduma hizo na matokeo yake ni vifo vingi vya watu masikini.

Kwa ujumla, hali mbaya ya uchumi inawaandama watu wa kawaida, hawa ndio waathirika namba moja na hali hiyo mbaya ya uchumi. Watu wa kawaida wanakosa huduma muhimu kama vile chakula, sukari na vitu vingine muhimu kwa sababu ya kukosa pesa na vitu kuuzwa kwa bei ya juu. Haya yanaweza kuthibitishwa namazungumzo ya Zitto na Amani.

*"Huko vijijini mbali  Hapa vijijini sukari kilo shilingi mia tano utaweza? Zitto alibakia*

*kimya na kumwacha Amani aendelee. "Haya hata wewe fikir  viwanda  zaidi ya vitano*

*bado hakuna sukari"* (uk, 16).

Kwa viongozi ukosefu wa huduma muhimu kwa watu wa kawaida wanasingizia hawana fedha za kigeni za kununulia bidhaa muhimu. Hutumia visingizio tele, hiki

mara kile, eti dunia nzima ina matatizo ya uchumi na huu ni uongo mtupu kama asemavyo msanii,

*"Sio kweli. Tunazungumza na mabaharia kutoka nchi nyingine Afrika ambako hali simbaya. Uongo mtupu tu*"(uk. 16)


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Matokeo ya hali mbaya ya uchumi ni kuwafanya watu wa kawaida (masikini) kujiingiza katika shughuli zisizo halali ili wajipatie fedha za kujikimu. Baadhi ya shughuli hizo haramu ni wizi, umalaya, ubakaji n.k. Kwa mfano, Tino alilazimika kuiba fedha benki ili aweze kumwokoa mwanae Cheche aliyekuwa ameumia kiuno chake (uk. 147 — 148). Pia mwanamke alivamiwa na kuporwa mkufu na hereni za dhahabu kama anavyosema msanii,

*"Washenzi, wamekata mkufu wangu wa dhahabu na kuchukua hereni zangu"* (uk. 52).

Katika kuonesha zaidi athari za hali mbaya ya uchumi, mwandishi anaonesha kuwa vijana wengi walijishughulisha katika shughuli za ukuwadi ili kupata pesa. Wanawake walifanya ufuska hata ndani ya gari bila aibu msanii anasema,

*"baada ya mwendo wa dakika karibu kumi, Amani alihisi kitu kinatokea kule nyuma. Bila kugeuka alitumia kiooo cha kuona nyuma; akaona abiria wale wamelaliana. Moyo ulimwenda kasi lakini hakusimama" (uk. 24)*

Hapa msanii anaonesha kuwa kutokana na hali ngumu ya maisha utu wa mtu hupotea, binadamu tunakuwa kama wanyama. Kitendo cha kufanya mapenzi mbele ya mwenzenu ni kinyume na utu kabisa na ni kikiuka maadili ya jamii kwa ujumla.

Vilevile kutokana na ugumu wa maisha vijana wengi walijingiza katika uuzaji wabangi ili wapate pesa za kutatulia matatizo yao, msanii anasema,

*"Siku moja Amani alishuhudia kijana mmoja akimuuzia baharia mmoja kila moja ya bangi kwa dola mia tano za kimarekani".* (uk. 25).
Hali ngumu ya maisha imepoteza utu wa mwanadamu. Watu walifikia kufanya yote haya kwa sababu ya ugumu wa maisha tu. Hali mbaya ya uchumi imeathiri sanawatu wa kawaida (tabaka la chini).

**Dhamira Nyinginezo**

**(a) *Rushwa katika famii***

Rushwa ni fedha au kitu cha thamani ambacho mtu hupokea au kutoa ili kununua au kuuza huduma ya kijamii ambayo haikustahili kununuliwa kinyume na taratibu *za* utoaji wa huduma hiyo. Rushwa ni adui wa haki na

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

maendeleo katika jamii yoyote. Mwandishi katika riwaya hii ameweza kubainisha tatizo la rushwa kamakichocheo cha hali mbaya (ngumu) ya maisha. Watoto wenye matatizo mbalimbali .hulazimika kutumia raslimali zao ili kuhonga watumishi wa umma ili kupata huduma au upendeleo fulani. Raslimali hizi zingeweza kutumika katika shughuli nyingine za maendeleo kama vile elimu, biashara, kilimo ambapo vingeweza kuinua hali ya uchumi: Haya yanathibitishwa katika kitabu pale mke wa Tino anaposema, *' haya, mjini tulikaa siku mbili mpaka tukapata tiketi za hongo, moja shilingi alfu nne. "..(uk. 71)*

Msomaji anaweza kuona namna rushwa ilivyoenea hadi katika sekta ya usafiri; watu wanaingia katika gharama ambazo si za lazima. Katika kushadidia kuhusu rushwa mwandishi anamwonyesha Amani namna anavyompa ofa daktari Mikwala ili amuandikie cheti kwenda Uingereza kwa matibabu. Mwandishi anasema,

*"Mazungumzo machache yaliendelea mpaka pale Amani alipokusudia kulivunja baraza*

*kwa kusema, Daktari nashukuru sana. Ngoja nikuache: Akachomoa kitita cha noti na*

*kumkabidhi." ...(uk.* 133)

Kwa upande mwingine Brown Kwacha anapokea rushwa ili aweze kuwahudumia wageni wake. Kwanza alipokea rushwa toka kwa Bhanj kama anavyosema msanii,

*"Sikia nakwisaveka dola laki moja ndani ya akaunti yako Genea"*

(uk. 92). Kitendo cha Brown Kwacha kupokea rushwa ni kinyume na maadili ya uongozi na hawa wanarudisha nyumba maendeleo ya jamii.

Vilevile Brown Kwacha aliomba rushwa ili aweze kumwidhinishia fedha za kigeni Cheche ili akatibiwe ulaya, msanii anasema,

*"Anataka laki tatu ndipo aidhinishe kutolewa fedha za kigeni"*

*"Laki tatu?"(uk 141)*


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Kwa upande mwingine Brown Kwacha alitoa rushwa kwa maofisa wa ardhi ili apate kiwanja cha kujengea nyumba (uk. 97).

Kwa ujumla, kutoa au kupokea rushwa ni kosa la jinai: Jamii inapaswa kupiga vita rushwa kwani husababisha watu kukosa haki zao. Mbaya zaidi ni kwamba rushwa hufanya maisha ya watu kuwa duni zaidi na kurudisha nyuma maendeleo ya nchi.

**(b) *Urasimu***

Hii ni dhamira nyingine inayoelezea ugumu wa maisha katika jamii yetu. Ukiritimba wa viongozi katika kuhudumia wananchi umekuwa ukikatisha tamaa wananchi. Milolongo ya mambo ya kirasimu ndiyo chanzo cha ushawishi. Urasimu ni kikwazo kikubwa cha maendeleo na hivyo hufanya maisha ya watu kuwa magumu.

Mfano mzuri tunaweza kuuona katika riwaya hii ya *Joka la Mdimu* ambapo kijana Cheche baada ya kuumia kiuno katika kujiandaa na sherehe ya uhuru. Anashindwa kupata huduma haraka kwa sababu za urasimu. Sababu mbalimbali zinatolewa kama vile serikali haina fedha za kigeni, kwenda bila ahadi n.k. kwa mfano, Amani anamwambia Brown Kwacha,

*"Mimi nimeletwa na shida ya mtoto wa ndugu yangu ambaye amekataliwa kupewa fedha za kigeni za kwenda kutibiwa Uingereza"* (uk. 138). Brown Kwacha aliuliza,

*"Wajuaje kama amekatatiwa? . . .Siyo kakatiliwa nchi haina fedha za kigeni. ...... umechagua wakati mbaya wa kuzungumzia jambo hilo. Tafuta wakati*

*mwingine*"

Kunapokuwa na viongozi wa aina hii wanaokumbatia urasimu ni kikwazo cha maendeleo na ndiyo chanzo cha ugumu wa maisha katika jamii.

**(c) *Kutowajibika***

Hii ni dhamira ambayo inamulika viongozi wazembe ambao wamepewa dhamana na wananchi ili watumikie taifa lao. Kuna baadhi ya viongozi wameshindwa kutambua wajibu wao katika ofisi walizokabidhiwa badala


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

yake ofisi hizi za umma wamegeuza kuwa miradi yao na kushindwa kuwatumikia wananchi.

Mfano mzuri ni Brown Kwacha, Mkurugenzi wa idara ya fedha za kigeni aligeuza ofisi ya urnma kuwa sehemu ya kufanya ufuska, biashara haramu na kushindwa kuhudumia wananchi. Mwandishi anasema;

*"Broom Kwacha alikuwa kinyonga...Nyendo zake nyingi zilitiliwa shaka"* (uk. 88).

Katika kuonesha kuwa Brown Kwacha hakuweza kutumikia ofisi yake ipasavyo,

mwandishi anasema.

*"Katibu wa Brown Kwacha alimtazama mkuu wake wa kazi akastaajabu namna alivyoweza kukaidi kuwakudumia wengine na vile alivyolainika mbele ya wasichana."* (uk. 94).

Kwa ujumla viongozi wa namna hii ni wasaliti na kushindwa kuwajibika kwa jamii yao ni tatizo linalochangia wananchi wakose msaada na kuona maisha kuwa magumu bila sababu za msingi. Kama viongozi wangewajibika ipasavyo kero za wananchi zingetatuliwa na maisha ya wananchi yangekuwa bora.

**(d)** ***Nafasi ya mwanamke katika jamii***

Mwandishi anaweza kuonesha kuwa wanawake ni watu wanaoumia zaidi katika jamii. Mwandishi ameonesha kuwa wanawake wananyanyasika kutokana na mfumo mbaya wa maisha uliopo katika jamii kama ilivyo kwa watu wengine. Wanawake watabaka la chini waliathirika na ugumu wa rnaisha kama ilivyo watu wengine wa tabaka la chini.

Wanawake pia waliathirika na mfumo dume ambao uliwapa fursa zaidi wanaume na huku ukiwadidimiza wanawake. Wanawake katika mfumo dume wananafasi zifuatazo:

- Wanawake ni wazazi na walezi: Mfano mzuri ni wema (mke wa Tino) alikuwa
  mama mzazi wa watoto watatu ambao ni Cheche, Tabu na Subira. Aliwazaa na


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

kuwalea wote. (uk. 69). Vilevile mke wa Brown Kwacha alikuwa mama mzazi wa watoto watatu ambao aliwalea wakati wote (uk. 103).

- Mwanamke pia amechorwa kama chombo cha starehe. Wan awake walichukuliwa kama chombo cha kuwastarehesha wanaume pindi wanapojisikia. Mfano mzuri ni wale wanaume mabaharia walivyokuwa wakiwatumia wanawake kama chombo cha kujistarehesha. Mfano mwingine., unamhusu mkurugenzi Brown Kwacha aliyekuwa anabadilisha wanawake kama nguo kwa lengo la kujistarehesha. Mwandishi anasema,

*"Maana kadtri alivyotembea na mwanamke mmoja mzuri ndivyo ashkiyake alichochewa akitamani tena na tena. Alishafumaniwa na mkewe, nyumbani na hata ofisini, Sio hivyo tu, alikwishavunja ahadi kadhaa za wachumba. Tayari alifumaniwa na wanaume akitembea na wake zao "* (uk. 91)

- Mwanamke amechorwa kama kiumbe duni asiyeweza kutoa mchango wowote wa mawazo. Haya tunayaona kwa Brown Kwacha ambaye hakuwa akimshirlkisha mke wake katika maamuzi (uk. 97).
- Mwanamke amechorwa kama mtu jasiri na mwenye msimanio. mfano Pamela ambaye aliviruka vihunzi vyote vya Brown Kwacha na Kwacha alistajabia na tabia hiyo ya Pamela. Brown Kwacha alimtaka Pamela kimapenzi kwa vishawishi *vya* pesa lakini Pamela alionesha msimamo na ujasiri akamkataa Kwacha (uk. 96).

Kwa ujumla, mwanamke amedidimizwa sana katika riwaya hii. Amechorwa kuwa ni muhanga wa kila aina ya uonevu, unyonyaji na unyanyasaji.

### (e) *Mapenzi na Ndoa*

Hii ni dhamira ambayo mwandishi ameishughulikia katika riwaya hii. Mwandishi ameonesha (mapenzi ya aina mbili mapenzi ya kweli na mapenzi ya uongo).


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Mapenzi ya kweli ni kati ya Tino na Amani. Hawa walikuwa marafiki wa kweli na wakisaidiana katika shida na raha. Amani alimsaidia sana Tino katika harakati zake za kumtibu mtoto wake Cheche (uk 77). Vilevile Amani alimsaidia Tino kwenda kuiba pesa benki ili wampeleke mtoto wake Cheche ulaya kutibiwa (uk. 147 _ 148).

Mapenzi mengine ya kweli yako kati. ya Tino na Jinja Maloni. Hawa walipendana hasa na ndio maana Tino aliamua kuishi nyumbani kwake na Jinja kwa ajili ya kumsaidia asiathirike sana na mji.

Mapenzi kati ya Zitto , Amani na Tino yalikuwa ya kweli hawa walipendana sana na walishirikiana katika ulevi wao

Mapenzi mengine ya kweli ni ya Tino kwa watoto wake hasa Cheche. Tino pamoja na kwamba hakuwa na kitu zaidi yakusukuma kwama aliwapenda sana watoto wake. Aliwapa zawadi za kila aina hasa wakati wa sikukuu. Ni kutokana namapenzi ya kweli kwa mtoto wake, Tino alilazimika kwenda kuiba fedha benki ili akamtibu mtoto wake Cheche ulaya.

Kwa upande wa mapenzi ya uongo ni kati ya Brown Kwacha na wanawake zake kama vile Josephine, Leila na wengine wengi. Mapenzi ya hawa yaliegemea katika pesa na hayakuwa mapenzi ya kweli.

Mapenzi mengine ya uongo ni kati ya Brown Kwacha kwa watoto wake. Brown Kwacha hakuwa na mapenzi na watoto wake, ndio maana walimuogopa sana na ilifikia hatua walishindwa hata kumuomba kitu.

Kuhusu ndoa nazo msanii ameainisha aina mbili za ndoa ya kweli na ya oungo. ndoa  ya kweli ni kati ya Tino na Wema. Hawa walikuwa na mapenzi ya dhati katika ndoa yao. Walishirikiana kulea watoto wao watatu na pale wapotofautiana wajirekebisha, mwandishi anasema;

*"Tino alioa akiwa na umri ma miaka ishirini  tu, Wema alikuwa mke ndugu, yaani mtoto wa mjomba wake. Mapenzi makubwa baina yao yalikamilishwa na udugu"* (uk. 71)

Kwa upande wa ndoa ya uongo ni kati ya Brown Kwacha na mke wake. Brown Kwacha hakumpenda mke wake ndio maana alibadilisha wanawake kama nguo na bila kumjali mke wake . Nyumbani hakuwa na raha na mkewe wala watoto wake, kila siku visingizio (uk. 91). Kutokana na


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

kutokuwa na uaminifu katika ndoa yake alifikia hatua akawa anawaleta wanawake wa nje hata nyumbani kwake kama anavyosema msanii,

*"Mke wake Kwacha aliwafumania nyumbani kwake wamejibwaga kitandani kalamu ikiandika"(uk.* 94).

Ndoa za uongo au kukosa uaminifu katika ndoa huwa ni chanzo cha mateso ndani ya nyumba na kukosekana kwa amani ndani ya familia, mwandishi anasema,

*"Baina yake na mumewe palikuwa, na mkato mithiliya wembe: Vigumu kuonekana kwa macho ila kwa madhara yake, Alikonda akajipa moyo, akarudisha hali yake, akakonda tena na tena"* (uk. 104).

Kwa ujumla, kukosa uaminifu katika ndoa huvuruga amani na utulivu kati ya mke na mume na matokeo yake ni kusambaratika kwa ndoa hiyo.

***(f) Uhujumu uchumi na magendo***

Uhujumu uchumi na magendo ni dhamira nyingine inayojadiliwa katika riwaya hii ya *Joka la mdimu.* Uhujumu uchumi na magendo ni tatizo linalokwamisha maendeleo ya nchi na hali ngumu ya maisha kwa watu wa tabaka la chini. Msanii anaonesha kuwa wahujumu uchumi wa nchi wengi ni viongozi na wafanyabiashara. Uhujumu uchumi na magendo umekuwa ukisababisha taifa kukosa mapato halali na matokeo yake mapato hayo yanaangukia mikononi mwa wachache.

Katika riwaya hii, msanii anaonesha kuwa viongozi wa serikali wako mstari wa mbele katika kuhujumu uchumi wa nchi kwa kumeza nyara za serikali kwa magendo na hivyo kulikosesha taifa mapato yake. Mkurugenzi Brown Kwacha anashirikana na wafanyabiashara kusafirisha pembe za ndovu nje ya nchi kwa magendo, msanii anasema,

*"Kwacha akamnong'oneza, "Lakini safari hii nina Consignment kubwa karibu pembe mia tatu hivyo angalia sana"* (uk. 93).

Brown Kwacha kama kiongozi wa umma anaihujumu nchi yake kwa kushirikiana na wafanyabiashara. Vilevile Brown Kwacha alikuwa anawinda wanyama kwa siri na kupata pembe za ndovu na faru kwa faida yake na hivyo kuhujumu uchumi wa nchi (uk. 106).


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Vilevile Brown Kwacha alishirikiana na majangili (wawindaji haramu) kuhujumu uchumi wa nchi. Brown aliwajiri watu ambao waliwinda wanyama nakupata Pembe zake kwa ajili ya kuuza nje kwa faida yake. Brown Kwacha alinunua pembe hizo kwa wawindaji wake kama asemavyo msanii,

*"Sawa,ziko pembe ishirini za faru na sitini za ndovu "* (uk. 119).

Kutokana na kitendo hiki cha akina Brown Kwacha na wawindaji wengine, wanyama kama ndovu na faru wanapungua mno kutokana na kuwindwa kila siku na wawindandaji haramu, Vilevile Brown Kwacha aliwasaidia wawindaji haramu bunduki, risasi pamoja na darubini ili waweze kuraisisha kazi zao za uwindaji (uk. 120- 121). Huu wote ni uhujumu uchumi wa nchi na watu kama Brown Kwacha wapo katika jamii yetu. Ili tuinue uchumi wa nchi yetu lazima tuwapige vita watu kama hawa

Brown Kwacha angekuwa mfano wa viongozi wa kupiga vita biashara haramu, lakini ndiye kinara wa biashara hizo. Aliweza kukodi majangili ili kuwinda ndovu wetu ambao wangetumika katika utalii ambao ungetuingizia fedha za kigeni. Nchi inahitaji fedha hizi kwa shughuli za maendeleo

Kwa upande mwingine, msanii anaonesha kuwa watu wengi wanafanya biashara za magendo na hivyo kilikosesha taifa fedha ambazo zingetumika kuinulia uchumi wa nchi. Mfano mzuri tuna Kashogi aliyefanya biashara za magendo za kuuza mafuta na hivyo kulikosesha taifa mapato yake (uk. 17). Hata kwenye vituo vya mafuta wafanyakazi waliuza mafuta kwa magendo na kwa bei kubwa (uk. 11).

Uhujumu uchumi wa wanchi magendo ni vitu vya hatari sana katika uchumi wa nchi na maendeleo ya nchi kwa ujumla, Ni lazima vikomeshwe ili kupunguza ugumu wa maisha.

Vilevile kuungua kwa jengo la hazina ni sehemu ya uhujumu uchumi. Brown Kwacha alihusika moja kwa moja na uchomaji wa jengo hilo, kwani kuchomwa kwa jengo hilo , kulisaidia kuteketeza nyaraka muhimu ambazo zingemsababishia matatizo katika kazi yake (uk. 156 — 157) kitendo cha Brown Kwacha kwenda Ulaya baada ya kuungua jengo hilo kinadhihirisha jinsi anavyohujumu uchumi wa nchi. Hata mahesabu ya wizara yaliyotengenezwa na kupelekwa bungeni yalikuwa ni batili kwa sababu yalikuwa ya uongo mtupu.

***(g) Matabaka***

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Matabaka ni ile hali ya jamii moja ya watu kuwa na tofauti kubwa kwa misingi ya kiuchumi na kielimu. Mwandishi ameonesha kuwa mfano wa maisha ya watu wa Mindule na miji iliyoko jirani umechangia sana kutokuwepo kwa usawa. Mfumo wa maisha umepelekea kuwa katika makundi makuu mawili; Kundi la walionacho (Matajiri) ambalo linawakilishwa na watu kama Bhanj, Brown Kwacha na Mawaziri wa Serikali. Kundi la pili ni lile la watu wasiokua nacho ambacho kinawakilishwa na Tino.

Kwa ujumla mfumo wa maisha na kutowajibika kwa serikali kwa watu wake wote kumetoa mwanya kwa matajiri kama Brown Kwacha kujirimbikizia mali nyingi kwa njia za magendo, wizi na rushwa. Matajiri hawa wanaishi maisha ya kifahari kwa kujirimbikizia fedha za kifani na kujenga majumba ya kifahari: Kwa mfano katika (uk 103-104) mwandishi anasema hivi kuhusu nyumba ya Brown,

*"Ilisimama na kuzibeba nyumba zote za jirani na hapo kwa haiba yake, na bwawa lake la kuogelea".*

Wakati hiyo ndiyo hali halisi ya maisha ya watu wa tabaka la juu, Mwandishi anaonesha kuwa katika jamii hiyo kulikuwa na watu waliishi maisha ya dhiki na ufukara uliotopea mathalani, Tino aliishi katika nyumba iliyokuwa ikivuja (uk 29) na watoto hawakuwa na nguo za kuwasitiri (uk 83).

Hivyo basi ni muhimu kwa serikali kuondoa tofauti hizo kwa kutubadilisha mfano wa maisha utakaosaidia wote kuishi katika maisha bora.

**(h) *Ufisadi***

Hii ni hali ya watu walio katika nyadhifa kutumia fursa ya madaraka kujitajirisha kwa kutumia rasilimali za nchi katika miradi yao binafsi.

Mwandishi anaona kuwa ufisadi wa viongozi umefanya wananchi waendelee kubebeshwa mizigo ambayo si ya lazima na hivyo maisha kuwa magumu kwa wananchi Mfano mzuri wa viongozi ambaye ni fisadi ni Brown Kwacha. Aliweza kujenga nyumba kubwa mbili za gharama kubwa mwandishi anasema,


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

*"Gharama ya nyumba iliyokuwa ijengwe na Wafaransa ilikuwa shilingi milioni mia mbili na nusu na ile nyingine milioni mia tatu. Vifaa vyote, isipokuwa mbao na saruji vilikuwa vitoke nje."*

Hizi fedha nyingi sana. Kwa mshahara wake tu asingeweza kujenga. Biashara za magendo, pesa za kigeni katika ofisi yake na rushwa ndivyo vyanzo vikuu vya fedha. za ujenzi wa nyumba yake.

Hali hii ni hatari kwa nchi, kwani hizo fedha za kigeni wanazodai hakuna hata kupeleka wagonjwa hospitali kutibiwa ndizo zinatumika kununulia mahitaji yao. Maslahi ya taifa lazima yapewe kipaumbele. Ubinafsi wa viongozi unakwamisha maendeleo ya nchi na kufanya maisha ya watu kuzidi kuwa magumu zaidi.

**Migogoro**

Migogoro kadhaa imejitokeza katika riwaya hii.

- Mgogoro wa kwanza ni kati ya makundi wawili ambao walipigana kwa kugombania kushusha magogo katika gari (uk. 34).

- Mgogoro mwingine ni kati ya Jinja na vibaka ambao walikuwa wanambaka mama mmoja na kukwapua mkufu na hereni za mama huyo. Alipotaka kumuokoa huyo mama walikuja juu na kuanza kupigana naye. Jinja alifanikiwa kumuokoa yule mama (uk. 51- 52).

- Mgogoro wa tatu ni wa kinafsia uliokuwa ndani ya Tino. Aliwaza namna ya kupata fedha ya kumtibu mwanae Cheche. Anaposhauriwa kwenda kupora fedha alisifia. Alishindwa kuamua kama aendelee na mpango huo lakini alihofu; alipowaza namna mwanae anavyoteseka aliumia moyo. Mwisho aliamua kwenda kupora fedha benki kiasi cha milioni 20 na kufanikiwa kwenda kumtibu Uingereza mwanae. (uk. 143 -148).

- Mgogoro wa nne ni kati ya katibu mkuu wa Wizara ya Mila na Utamaduni na kijana ambao walipigana katika siku ya uzinduzi wa nyumba ya Brown Kwacha,Walikuwa wanagombania msichana aitwae Esther, (uk. 102).


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- Mgogoro mwingine ni kati ya mke wa Brown, Brown na Josephine. Mke wa Brown Kwacha alimfumania Brown Kwacha akiwa anfanya mapenzi na Josephine. Mke wa Brown Kwacha alimpiga Josephine hadi mdomo wa chini ukapasuka (uk 94).

Kwa ujumla, migogoro yote hii imetumika kusukuma riwaya mbele na kujaribu kuonesha chanzo cha matatizo ambayo yamejadiliwa kama dhamira.

Hata hivyo mwandishi anautoa masuluhisho ambayo yanaongeza uhalifu katika jamii, kwa mfano kujihusisha na dawa za kulevya, umalaya, kupigana au kuiba benki si masuluhisho bora kuna haja waandishi kutoa masuluhisho endelevu katika jamii.

**Ujumbe wa Mwandishi**

Mwandishi wa riwaya hii ametoa maadili au mafunzo kadhaa kwa jamii. Mtu anaposoma riwaya hii anapata mafunzo yafuatayo;

- Ufisadi wa viongozi ni uhalifu mkubwa ambao unamadhara makubwa katika maisha ya wananchi walio wengi. Jamii haina budi kupiga vita ufisadi ili raslimali zao ziwanufaishe wanajamii wote.
- Rushwa ni adui wa haki., penye rushwa haki hujitenga. Rushwa ni ndugu mkubwa wa ufisadi. Hivyo, jamii lazima ipambane na vitendo vyote vinavyozuia haki isitendeke katika jamii.
- Mapenzi ya dhati ndani ya jamii ni muhimu sana kwa wanandoa, marafiki na familia hawana budi kuwa na mapenzi ya dhati ili kudumisha amani miongoni mwao.
- Jamii inapaswa kubadili mfumo wa maisha unaowakandamiza wanawake ili wasiendelee kuwa chombo duni, tegemezi au chombo cha starehe.

**Mtazamo wa Mwandishi**

Mwandishi Abdalah J. Safari ana mtazamo wa kiyakinifu. Mwandishi ameweza kuainishi kero mbalimbali walizonazo wananchi. Mwandishi ameeleza uozo uliomo ndani ya jamii bila woga na namna wakubwa wanavyohusika na uozo huo. Mwandishi anaonekana anawanyoshea kidole viongozi kuwa ndiyo chanzo cha maisha magumu kwani wananchi wa kawaida wanajituma kurekebisha maisha yao duni lakini kikwazo kimekuwa ni viongozi ambao ni mafisadi na warasimu.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**Falsafa ya Mwandishi**

Mwandishi anaelekea kuamini kuwa matatizo makubwa yanayojitokeza katika jamii yanasababishwa na kutowajibika kwa viongozi, urasimu na ufisadi ndio kikwazo

**FANI**

**Muundo:**

Riwaya ya *Joka la Mdimu* ina jumla ya sura kumi (10) ambazo amezipa majina kutokana na majina ya wahusika, mahali na matukio yanayobeba kisa kizima cha hadithi hiyo katika sura husika. Kila kisa amekieleza kwa masimulizi ya msago, maisha ya kila mtu na miji kuelezea moja kwa moja visa na matukio unaweza kuandika kwa muhtasari kama ilivyooneshwa kwenye sehemu ya pitio la kitabu.

**Mtindo**

Riwaya hii ya *Joka la Mdimu* ipo katika mtindo wa masimulizi. Nafsi ya tatu ndiyo imetawala kwa kiasi kikubwa, japokuwa kuna matumizi ya nafsi ya kwanza na pili pia. Dayolojia imetumika kiasi kidogo tu. Mwandishi amefanya hivyo ili kuweka uhalisia wa mazungumzo baina ya wahusika. Mwandishi pia ameweza kutumia nyimbo katika riwaya hii. Wimbo wa Chaupele upo.

*"Chaupele mpenzi hayo usemayo*

*Kama ni maradhi yapeleke kwa daktari*

*Wanambia niliache rumba, na mimi sikuzoea*

*Sitaweza  kuliacha rumba kwa sababu yako,*

*Kama wampenda nenda kwa baba,*

*Utoe mapesa, ndipo urudi unioe"*(uk. 70 - 71).

**Wahusika**


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

1. ***Amani***

Huyu ni mhusika mkuu. Ni dereva wa taxi. Ni kijana mchapa kazi, ana huruma, ana hekima na busara. Anafaa kuigwa na jamii.

2. ***Brown Kwacha***

Huyu ni mhusika msaidizi. Ni mkurugenzi wa idara ya fedha za kigeni, Ni malaya, Si mtu adilifu, Ni fisadi, Anapenda rushwa, Anafanya biashara za magendo na Hafai kuigwa.

3. ***Tino***

Huyu ni mhusika mkuu msaidizi. Ni mvuta kwama. Ni baba wa watoto watatu. Ni jasiri. Ni mchapa kazi. Mwanamichezo. Anafaa kuigwa.

4. ***Jinja Maloni***

Ana upendo, mlevi, mkakamavu, si muoga. Hafai kuigwa.

5. ***Daktari Mikwala***

Ni daktari bingwa wa mifupa. Ni mlevi, anapenda rushwa. Hafai kuigwa.

6. ***Shiraz Bhanj***

Ni mfanyabiashara. Mtoa rushwa. Ni rafiki yake Brown Kwacha. Hafai kuigwa.

7. ***Zitto***

Ni mfanyakazi wa bandari. Ni rafiki yake Amani na Tino. Ni mtu wa kipato cha chini. Ni mwanamichezo.

8. ***Cheche***

Ni mtoto wa kiume wa Tino. Ni mvulana anayesoma. Ndiye aliyeumia kiuno wakati wa michezo ya kusherekea uhuru wa nchi. Ni mtoto mwenye tabia njema. Ni mcheshi, mdadisi na mwanamichexo. Alipendwa sana na watu.

Wahusika wengine ni Leila, Josephina, Pamela. Hawa wamejitokeza kama wahusika ambao wamekuwa marafiki wa kike wa Brown Kwacha.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**Matumiz ya lugha**

Lugha iliyotumika ni ya kawaida iliyoshehenezwa tamthilia za semi na mbinu nyingine zaKisanaa.

**(i)** ***Misemo***

*Asiye na bahati habahatishi (uk, 10).*

*Tandu kwenda  nyuma na mbele ndiyo hulka yake. (uk. 25).*

*Asiyezika hazikwi(uk. 48),*

*Mmetupajongoo na mtiwe (uk.  64)*

**(ii)** ***Methali***

*Asilolijua mtu ni usiku wa giza (uk. 77)*

*Ukiona mwenzio ananyolewa, tia maji (uk, 83)*

*Mtaka waridi sharti avumilie miiba (uk, 98)*

*Biashara haigombi (uk. 99)*

**(iii)** ***Matumiziya Lugha Nyingine***

- Mwandishi ameigiza maneno ya Kiingereza   sehemu mbalimbali. Kwa mfano:

  *- Missions to seamen please, (uk. 24). - -*

  *- Hey men will you pay extra dollars (uk. 24).*

* Matumizi ya lugha ya Kiarabu. Kwa mfano:

*"lnna Lillahi wa Inna Ilahi Rajiunna! (uk. 41).*



Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

***(iv)Tamathali za Semi***

*Tashibiha*

- Zalpher 6 ile iliunguruma kama simba dume aliyeghadhibishwa. (uk. 9).
- Wote walikimbilia kula wakiminyana kufa au kupona kama kaa wanavyogombea mavi ya mvuvi. (uk. 21).

- Maduka makubwa yalichipua mithili ya uyoga. (uk. 26).
- Miguu yake ilikazana mithili ya upinde uliotaka kufyatuliwa (uk. 33).

*Tashihisi*

Utumbo ulimlaumu (uk. 12).

Mvua ikarindima kwa kiburi na kuviadhibu vibati vibovu (uk. 27).

Lakini hata fikra nazo zilikuwa kama zimempiga chenga. (uk. 4).

*Sitiari*

Sote ni kobe (uk, 72).

Sarahange wetu mboga kweli siku hizi (uk. 15).

**Mbinu Nyingine za Kisanaa**

*Onomatopoea/ Tanakali Sauti".*

Mfano:-

(i) Saa mezani iliendelea kugonga, **"ta ta ta".**

(ii) Akazungusha ufunguo wa gari lake kutaka kuliwasha lakini ikatokea sauti kali fupi, **"ta nye nye"**.

***Takriri***


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Funga, shinda! funga, shinda ! saut za mashabiki zikalindima tena (uk. 56).

Shinda! shinda! shinda!kibanda kilitememeka tena (uk. 55).

Shetani! oyee! Shetani! oyee! Shetani chinja! (uk. 58).

**Mandhari**

Riwaya hii imejengwa katika mazingira ya mjini. Mwandishi ametumia majina ya miji ya Mindule, Sega na Boko ambayo ipo nje kidogo ya mji wa Dar es Salaam.

Mandhari haya yanaweza kugusa nchi zote zinazoendelea ambapo kuna hali ngumu ya uchumi na matatizo ya ufisadi na urasimu.

**Jina la kitabu**

*Joka la Mdimu* ni jina la kitabu ambalo linajengwa kwa lugha ya picha. Joka la Mdimu ni aina ya nyoka ambaye huishi katika miti ya kijani. Joka hili hupendelea kuishi katika minyaa na midimu. Nyoka huyu huwa na rangi ya kijani ambapo si rahisi kumuona kwa macho kwani hufanana sana na matawi ya mti aliyomo. Nyoka huyu ni hatari sana kwa maisha ya watu.

*Joka la Mdimu* limetumika kuwakilisha viongozi hatari kama nyoka huyu. Viongozi wote mafisadi kama ilivyo kwa Brown Kwacha wamelinganishwa na joka hili la mdimu.

Kwa ujumla jina *la* kitabu linasadifu yote yaliyomo ndani ya kitabu, kwani kitabu kizima kinazungumzia mafisadi na walanguzi, wahujumu uchumi, watoa rushwa na wapokea rushwa na wanaofanya magendo, Hawa ndio majoka wenyewe. Wahusika hawa wanaishi nasi na kufanana nasi lakini undani wa maisha yao ni hatari sana kama ilivyo kwa joka la mdimu.

**Kufaulu na Kutofaulu**

**Kufaulu**

Kimaudhui mwandishi amefaulu kuelezea matatizo yanayoikabili jamii. Ameeleza kwa uwazi bila kuficha namna maisha ya watu wa tabaka la chini yalivyo magumu wakati viongozi na wafanyabiashara wanafurahia maisha.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Ameeleza kwa dhati matatizo ya uhujumu uchumi, urasimu na ufisadi yanavyokuwa tatizo katika maendeleo,

Kifani mwandishi amefaulu kutumia lugha ambayo amewapa wahusika kulingana na uhusika wao. Ametumia tamathali za semi ambazo zinabeba **dhamira** ya mwandishi.

**Kutofaulu**

Mwandishi ameshindwa kuonesha masuluhisho ya matatizo husika. Hata pale anapotoa masuluhisho ya matatizo yanakuwa ni ya kihalifu zaidi. Kwa mfano, mahesabu yanapokuwa mabaya., Brown Kwacha anatatua kwa kufunga wahasibu wake watengeneze mahesabu na bunge linakubali. Au Tino anapokosa fedha za kumuuguza mwanae anaenda kupora fedha benki na hakamatwi. Mwandishi anaonekana kuhalalisha matumizi ya nguvu za kihalifu kutatua matatizo katika jamii. Lingekuwa jambo la busara kama kungekuwa na hatua za uwajibishwaji watu katika kuondoa uozo uliomo katika jamii.

## UHAKIKI WA USHAIRI

**Jina la kitabu: WASAKATONGE**
**Mwandishi: MOHAMED .S. KHATIBU**
**Wachapishaji: OUP (T) Ltd**
**Mwaka: 2003**

**Utangulizi**
*Wasakatonge* ni diwani yenye mashairi yanayotetea wavujajasho wanaonyanyaswa, kuonewa, kudharauliwa na kunyonywa na wenye navyo. Ni diwani inaoonyesha uozo wa jamii na athari zake kwa wanyonge. Diwani hii ni chachu ya kuzindua umma unaonyanyaswa ili udai haki yao dhidi ya wanasiasa madikteta wanaotumia nguvu za dola kwa maslahi yao.

**Maudhui**
**Dhamira kuu**

(i) Ujenzi wa jamii mpya

(ii) Ukombozi


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

**Ujenzi wa jamii mpya**

Mwandishi anajadili Kwa kiasi kikubwa suala la ujenzi wa jamii mpya. Jamii ambayo itatupilia mbali uonevu, unyonyaji, dhuluma unafiki, usaliti, uongozi mbaya, matabaka, ukasuku na hali ngumu ya maisha. Jamii ambayo hatamu zote za utawala, uchumi na siasa zitakuwa katika misingi ya usawa na haki.

Kama anavyoonesha kwenye diwani yake ya *Fungate ya Uhuru* kuwa suala la ujenzi wa jamii lilianza mara baada ya uhuru na kuimarishwa na kutangazwa kwa Azimio la Arusha mwaka 1967. Katika diwani hii msanii anaonyesha kuwa bado hatujafanikiwa kujenga jamii hiyo kutokana na sababu zifuatazo.

Kwanza katika jamii yetu bado kuna msuguano mkali sana wa kitabaka kati ya tabaka tawala la wenyenavyo linalonyonya na kuligandamiza tabaka la chini la makabwela. Shairi la *“Kansa”* na mengine kama vile *“Wasakatonge”, “Asali”* na *“Mumiani”* ni ushahidi wa kutosha unaobainisha vurugu katika jamii.

Pili hali ya udikteta, unafiki na usaliti uliokithiri katika nchi zetu umeoneshwa katika diwani hii. Msanii anajadili masuala haya kwa kuonesha jinsi viongozi wa nchi na dini wanavyosaliti wananchi na waumini wao. Haya yanajionesha wazi katika mashairi ya *“Wasodhambi”* (uk. 14), *“Pepo bila kifo”* (uk.14), *”Uasi”* (uk. 8). *“Madikteta”* (uk.21) na *“Nahodha”* (uk. 41).

Suala la uongozi mbaya nalo linaoneshwa na msanii katika diwani hii. Msanii anaona bado kuna uongozi mbovu katika jamii yetu katika mashairi ya *“Tonge la Ugali”* (uk. 20), *“Madikteta”* (uk.21), *“Fahali ya Dunia”* (uk. 45-46), *“Vinyago”* (uk. 49) na *“Nahodha”* (uk. 41-42).

Ni kutokana na matatizo hayo na mengineyo, ndio maana msanii anonesha kuwa tumeshindwa kujenga jamii mpya. Katika kujadili dhamira hii ya ujenzi wa jamii mpya, Mwandishi ameonesha mbinu mbalimbali zinazoweza kutumiwa na jamii katika zoezi hilo. Mbinu hizo ni kama vile:

***(i) Kupiga vita uongozi mbaya***

Msanii anaonesha kuwa oungozi mbaya ni kikwazo cha ujenzi wa jamii mpya. Suala la uongozi mbaya linaonekana kuwa tatizo sugu katika nchi nyingi za Kiafrika na kama halitatafutiwa tiba basi tutaendelea kuwa na

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

machafuko ya kisiasa na vita vya wenyewe kwa wenyewe kila siku. Mwandishi amelionesha suala hili katika shairi la *"Madikteta"* (uk. 21) na *"Unyama"* (uk . 47). Kwani viongozi wengi huongoza nchi Kwa mabavu na sio kwa kufuata sheria zilizowekwa na nchi husika. Kwa sababu ya uchu wa madaraka, wengi huingia madarakani kwa mtutu wa bunduki.

Vilevle katika shairi la *"Miamba"* (uk.27) ambalo ameonesha kwa kutumia taswira kwa kuonesha "mbugha" kama nchi na "simba na chui" kama viongozi wa nchi, anaonesha kwamba viongozi wa nchi ndio wanaomiliki vitu vya muhimu (njia kuu za uzalishaji mali) na walio wengi hawamiliki chochote na matokeo yake ni kunyonywa na viongozi hao. Pia shairi *"Mtafaruku"* (uk.36) ameonesha jinsi viongozi wanaovyowanyima watu wa kawaida uhuru wa kusema au kuzungumzia maovu yaliyomo katika jamii yao.

Katika shairi la *"Nahodha"* (uk. 41). Anaonesha kuwa baadhi ya viongozi hushindwa kuongoza nchi zao na wanapoambiwa kujiuzulu na wananchi huwa hawakubali na shairi la *"Peponi bila kifo"* (uk. 14) ameonesha tabia ya baadhi ya viongozi kuishi maisha ya raha na ya anasa wakati hawawajibiki. Ni vigumu katika uhalisia kwenda peponi bila kupitia kufa kama mshairi anavyoelezea, huwezi kupata pepo bila kupitia kifo. Hii ni lugha ya picha anayotumia msanii kuonesha kifo ni kama mapambano, ili kupitia daraja la mafanikio ambayo ni pepo kulingana na maelezo ya mwandishi.
Pia katika mashairi ya *"Tonge la ugali"* (uk. 20), *"Fahali ya Dunia"* (uk.45), *"Vinyago"* (uk. 49) yanaonesha uongozi mbaya katika jamii. Hivyo ili tuweze kujenga jamii mpya lazima tupige vita uongozi mbaya.

***(ii) Kuwa na demokrasia ya kweli na utu.***

Katika dunia yetu ya sasa, demokrasia na utu vimetoweka na kupotea kwani katika nchi nyingi zinazofuata mfumo wa kidemokrasia huwa si demokrasia ya kweli. katika nchi ya kidemokrasia wananchi wanakuwa na uwezo wa kupinga au kukataa yale yanayokuwa kinyume na watakavyo.

Katika diwani hii, msanii ameonesha kuwa katika jamii yetu hakuna demokrasia ya kweli na kunapokosekana demokrasia ya kweli hata utu hupotea. Haya yanajidhihirisha wazi katika mashairi ya *"Madikteta"* *"Saddam Hussein"* (uk. 26-27) na *"Unyama"* (uk. 47-48).


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Katika mashairi haya ameelezea juu ya viongozi ambao huongoza nchi bila bila kujali utu Kwa kuwafanyia raia wao mambo ambayo huwa ni kinyume na misingi ya ubinadamu. Kama demokrasia inavyojieleza yenyewe, hujali zaidi utu wa mtu, hivyo ni vizuri viongozi waongozapo wasijali utu wao tu, bali ajali nawale wanaowaongoza. Hivyo, ili tujenge jamii mpya lazima tuwe na demokrasia ya kweli.

***(iii) Kupiga vita ukoloni mamboleo***

Ukoloni mamboleo unaonekana ni kikwazo kikubwa cha ujenzi wa jamii hapa nchini. Mshairi ananitaka jamii kupiga vita ukoloni mamboleo Kwani unaathiri jamii nzima katika suala zima la maendeleo katika nyanja zote muhimu ambazo ni uchumi, siasa na utamaduni kwa ujmla.

Katika shairi la *"Hatua Kali"* (uk.8-9) anaonesha kuwa uchumi wa taifa letu bado una tegemea misaada toka nje, mfano mitaji, madawa, mashine na pembejeo nahii ndio inayotufanya tudumae na tuwe tegemezi. Mshairi anaonesha athari za ukoloni mamboleo katika shairi la *"Wafadhiliwa"* (uk38) kuwa viongozi wa nchi wanakuwa ni watekelezaji wa magizo kutoka wa wahisani ambao huwa wanajali maslahi yao zaidi. Matokeo yake ni kwamba nchi inafadhiliwa hukosa uhure wa kujiamulia mambo yao kutokana kulaziamishwa kutimiza yale tu yanayotakiwa na wahisani hao.

Katika shairi la *"Tiba Isiyobu"* (uk. 18), anaonesha jinsi misaada inayotolewa na wahisani inavyokuwa na masharti magumu. Masharti haya yanapelekea kutawaliwa kwa nchi hiyo kiuchumi na nchi inayotoa misaada pindi washindwapo kulipa madeni au kutimiza masharti yao, yaani kutawaliwa kwa kufuata maagizo yao. Kwa hiyo, msanii anaitaka jamii iwe makini na misaada toka kwa wahisani.

Katika shairi la *"Klabu"* (uk.50) anaonesha kuwa utegemezi na kuombaomba misaada hujenga mazingira mazuri ya nchi kwa kuvamiwa na nchi za kibepari. Hivyo msanii anaonesha kuwa ili tuondokane na ukoloni mamboleo tusiwe tegemezi, bali tuchape kazi kwa kuendeleza viwanda vyetu ili kukuza uchumi wetu, tupige vita rushwa, tuache kuombaomba hovyo.

Msanii anaendelea kuiasa jamii kuwa hakuna msaada unaotolewa bure bila ya mtoaji kujua nini atafaidika na msaada huo. Hivyo nchi inaposaidia nchi nyingine, lazima imeona faida mahali hapo ya msaada unaotolewa.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Msanii pia anasisitiza suala la elimu katika kuondoa tatizo hili la ukoloni mamboleo. Elimu lazima ipatikane ili wananchi wapate kuzindua na kuona wapi wanaelekea. Kwa kufanya hivyo tuatalinda heshima ya taifa letu na kuepuka manyanyaso kutoka kwa wahisani na matokeo yake ni kujenga jamii mpya.

***(iv) Kupiga vita matabaka***

Katika diwani hii, msanii anaonesha mivutano ya kitabaka iliyopo katika jamii yetu. Msanii ameonesha kuwa katika jamii yetu kuna matabaka mawili nayo ni tabaka tawala na tabaka la chini, yaani tabaka tawaliwa. Msanii anaendelea kuonesha kuwa, kuna uhasama mkubwa kati ya matabaka haya mawili, kwani tabaka tawala hukandamiza tabaka tawaliwa ambalo ni la wasionacho.

Katika kuonesha msuguano huo wa kitabaka, msanii ametumia shairi la “K*ansa”* (uk.5) kuonesha jinsi tatizo hilo lilivyo kubwa kama ugonjwa wa kansa, ambao huwa hauna uwezekano wa kupona. Matabaka katika jamii hayafai kwa kuigawa jamiii kulingana na hadhi na uwezo walionao, hivyo husababisha kundi moja kugandamizwa na kunyanyaswa kutokana na uwezo wao kuwa duni na kundi hili huwa ni la wale masikini wasio na chochote. Mawazo haya yanajadiliwa katika shairi la “W*asakatonge”(*uk. 5) *“Mvuja Jasho”* na “W*alala Hoi* (uk.36) katika mashairi haya msanii ameonesha kuwa watu wa tabaka la chini, hufanya kazi kwa bidii zao zote katika shughuli zao ili kujikwamua na umasikini, lakini wanashindwa kwani malipo wayapatayo huwa duni sana ukilinganisha na uzito wa kazi zao.

Katika shairi la “*Asali Lipotoja”* (uk.37-38) anaonesha jinsi tabaka la juu linavyofaidika na matunda ya uhuru, wakati wale waliopigania uhuru huo ( tabaka la chini) hawafaidi matunda ya uhuru, wakati wale waliopigania uhuru huo ( tabaka la chini) hawafaidi matunda hayo. Vilevile shairi la *“Kosa”(*uk. 3) msanii anaonesha jinsi wananchi wanavyonyanyaswa na kugandamizwa na tabaka la juu kwa kunyimwa haki zao za msingi ambazo anastahili kupata.

Katika shairi la “*Hatuna Kauli”* (uk. 8-9) msanii anaonesha jinsi nchi tajiri zinavyogandamiza nchi masikini na shairi la “*Mumiani”(*uk.34) anaonesha unyonyaji unaofanywa na watu na nyadhifa za juu katika nyanja mbalimbali za kimaisha kama vile mahakamani, watu hukoseshwa haki zao, hospitalini, vijijini wakulima hulipwa bei ndogo ya mazao yao licha ya yeye


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

kutumia pesa nyingi katika kustawisha mazao hayo.

Utabaka katika jamii ni janga sugu lisiloweza kuepukika na unapomnyonya na mumnyima mtu haki, ipo siku utazinduka na kudai haki hiyo kwa nguvu kama anavyoonesha msanii katika shairi la *"Hatukubali "* (uk. 38). Hapa msanii anaonesha jinsi watu wa tabaka la chini walivyochoshwa na kugandamizwa na kunyanyaswa na tabaka la juu, ijapokuwa inakuwa ni kosa kwao kufanya hivyo, kwani tabaka tawala hupenda kuwa juu zaidi milele na milele. Mawazo haya yanajitokeza pia katika shairi la *"Marufuku"*( uk.36)

Hivyo msanii anaonesha kwamba kuwepo kwa matabaka katika jamii hukuwamisha ujenzi wa jamii mpya hapa nchini, kwani wanaofaidi maisha mazuri ni viongozi ambao ni tabaka tawala ( wasakatonge), ili kujenga jamii mpya lazima tupige vita matabaka.

***(v) kupiga vita unafiki na usaliti***

Suala la unafiki na usaliti linajitokeza kwa viongozi wa kisiasa na udini. Msanii anaonesha unafiki na usaliti katika mashairi ya " *Waso Dhambi"* (uk.1) *"Uasi"* (uk.8) *"Sikujua"* (uk.28) *"Nahaodha"* ( uk.41-42) "W*alamba Nyayo"* ( uk.46-47), *"Pepo Bila Kifo"* (uk.14) na *Madikteta* (uk,21)

Katika shairi la "U*asi*" anaongelea unafiki na usaliti katika siasa na dini katika dini.Katika( uislam na ukristo) ambayo huwahubiria waumini wao kwa maneno makali yenye vitisho kwa kuwaonya waache uonevu wakati wao wenyewe maneno wayasemayo ni kinyume na matendo wayatendayo, vilevile katika dini, viongozi wanatenda matendo machafu kinyume na dini zao. Wakiwa mbele ya waumini wanajifanya hawatendi dhambi. Haya yanajidhihirisha wazi katika shairi la *"Vinyonga"* (uk. 49)

Viongozi wa kisiasa wanaongea maneno mengi kwa wananchi na kuahidi vitu mbalimbali hata kama viko nje ya uwezo wao ili tu waonekane wanafaa. Wanapopata uongozi husahau na kufanya maovu kama vile ubadhirifu wa fedha na kula rushwa. Haya yameoneshwa wazi katika shairi la " V*inyago" na Waramba Nyayo"(*uk. 46-47). Tatizo hili linajitokeza tena katika shairi la " A*sali Lipotoja"* hapa anaonesha jinsi watu walivyojitolea katika harakati za ukombozi wa nchi, lakini uhuru ulipopatikana nyadhifa zote za juu walishika wengine ambao hawakupigania uhuru huo na waliopigania wakaachwa na hali duni ya maisha.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Kwa ujumla, unafiki na usaliti umejadiliwa sana katika diwani hii ya W*asakatonge* na msanii anaoneshakuwa ili tuweze kujenga jamii mpya ni lazima tupige vita unafiki na usaliti wa viongozi wetu.

***(vi) Umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii***

Msanii ameonesha umuhimu wa watu kufanya kazi kwa bidii ili kuweza kujenga jamii mpya. Katika shairi la *" Klabu"* ( uk. 50) msanii anawataka watu wote katika jamii kufanya kazi kwa bidii viwandani na mashambani ili kuleta maendeleo ya nchi kwa ujumla na kujenga jamii mpya.

Vilevile katika shairi la " *Wanawake wa Afrika*" (uk.2-3) anaeleza suala hilo la kufanya kazi kwa bidii kwa kuwashauri wanawake waamke toka usingizini na wachape kazi kwa bidii na wadai haki zao za msingi. Hivyo katika diwani hii, msanii anaonesha kuwa kufanyakazi kwa bidii kutaleta maendeleo ya nchi na hivyo kufanikisha kujenga jamii mpya.

***(vii) Kupiga vita mmomonyoko wa maadili***

Katika diwani ya Wasakatonge msanii amejadili swala la mmonyoko wa maadili kulingana na wakati huu wa maendeleo ya sayansi na tekinolojia unaosababishwa na suala zima la utandawazi na kupeleka jamii kukosa mwelekeo wake uliokukwa mwema.

Mfano amejadili suala zima la wanawake wenye tabia yaa kukutana kimwili wenyewe kwa wenyewe wakiwa jinsia moja "*Wasagaji".* Amewaasa wanawake hao waachane nayo na watulie wapate wanaume wa kuwaoa na kufanya kama tendo hilo lilivyoruhusiwa kulingana na maadili ya kidini na ustaarabu wa jamii yetu na ameonesha hili katika shairi la " *Jiwe si Mchi"* (uk. 18)

Hakuishia hapo tu, pia amelijadili suala la umalaya, ambalo linawahusu wanawake wanaotembea hovyo na wanaume bila kuangalia hali mbaya iliyopo sasa katika jamii, hususani katika suala hili la ugonjwa wa UKIMWI linachongangiwa kiasi kikubwa na uasherati, hili ameelezea katika shairi la *" Wewe Jiko la Shamba"* (uk. 44-48).

Limejadiliwa pia suala la mwenendo mbovu unaoikumba jamii yetu, mfano wa hilo ni katika shairi la *"Unyama* (uk.47-48) mshairi ameonesha masuala ya ubakaji na kunajisi yanavyofanywa na binadamu kama moja ya masuala yanayopelekea maadili kuporomoka.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Hakuishia hapo, bali kuna suala zima la wanaume ambao wanatabia za kuingiliana kimwili wakiwa jinsia moja kwa mujibu wa wimbo wa "*Taarab"* uliokuwa ukiwazungumzia wanaume wa aina hiyo. Mshairi yeye,. Kwa kiasi Fulani ameonekana kuitetea tabia hii kwa kuelezea kuwa nao hupata raha zaidi wafanyavyo hivyo na wengine maumbile ndiyo huwaruhusu. Shairi la "*Jawabu la Nahodha*" (a( uk. 24-25). Kiuhalisia suala hili halipo kabisa katika mwenendo na maadili yetu ya Kitanzania. Ili tujenge jamii mpya lazima tupige vita mmomonyoko wa maadili katika jamii yetu ambao ni kinyume na taratibu za jamii zetu.

***(viii) Kupiga vita hali ngumu ya maisha***

Hali ngumu ya maisha ni moja ya dhamira ambayo imejadiliwa na mwandishi Seif Khatibu amejadili jinsi watu wa tabaka la chini wanavyoishi katika shairi la *"Walala Hoi*" ( uk. 36) mshairi ameelezea jinsi hali duni ya maisha inavyowakabili makuli wa bandarini, wakulima, wavuvi na wachimba migodi, ameelezea jinsi gani kazi ngumu wanazofanya na malipo yao kuwa duni. Wanakubaliana na kazi za jinsi hii si kwa kupenda ila ni kutokana na ugumu wa maisha ambao umesababishwa na uongozi mbaya uliopo madarakani. Katika shairi *"Mvuja Jasho*" ( uk. 12-13) , mshairi anaonesha hali ya watu wa chini maisha yao yanavyokuwa duni, kipato chao ni kidogo ukilinganisha na mahitaji waliyonayo kwani kile wakipatacho hutumika kwa siku moja tu.

Mshairi anaonesha jinsi hali ngumu ya maisha inavyolibadili bara la Afrika katika shairi la "*Afrika"* (uk. 6-8) mshairi anasema ni lini Afrika itakuwa kitalu cha shibe na sayari ya uzima. Hii inatuthibitishia kwamba bara la Afrika lipo katika hali mbaya ya maisha

Seif Khatib anaelezea jinsi tabaka hili la chini mfano katika shairi la "W*asakatonge",* "W*alala hoi",* wanavyotaabika na kukosa mwelekeo wa maisha na kuwa watu wa kkuhangaika katika shairi la "*Twende Wapi"* (uk. 20- 21).
Pia mshairi katika shairi la "Mama Ntiliye" anaonesha jinsi wanawake wanavyojitahidi kujishughulisha katika hali yao duni kwa kuuza vyakula japokuwa hawana mtaji mkubwa na nyenzo zao ni duni. Pia tukiangalia kiundani mshairi amejaribu kutumia lugha ya picha kuelezea suala hili, hapa amejaribu kumtumia Mama Ntiliye mwenye nyenzo duni kama jamii yenye hali duni lakini uduni wao haweza kusababishwa na majukumu na


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

fitina wanaozitunga na kusababisha mtafaruku unaopelekea kutokuwa na maendeleo na matokeo yake maisha ni kuwa magumu.

Na mwisho mshairi anaielimisha jamii, kuwa ni vizuri ukaanza kujikinga kuliko kusubiri tiba kwani tiba nyingine huweza isisaidie kama anavyosema katika shairi la "*Tiba Isiyotibu"* anaonesha madhara yanayopatikana kutokana na misaada inayotolewa na nchi hisani ili kuzisaidia nchi zinazoendelea. Misaada yao huwa ni ya kilaghai kwani huambatanishwa na masharti magumu yanayopelekea hali ngumu ya maisha katika nchi kuzidi kuwa mbaya. Hivyo basi, si misaada yote huweza kuwa suluhisho la tatizo la hali mbaya ya maisha katika nchi bali huweza kuleta ugumu zaidi ya awali. Hivyo, ili tujenge jamii mpya ni lazima tupige vita hali ngumu ya maisha.

**Ukombozi**

Ukombozi ni dhamira nyingine kuu anayoijadili msanii katika diwani hii ya *Wasakatonge*. Katika diwani hii, amejadili kwa kiasi kikubwa ukombozi wa wanajamii dhidi ya unyonyaji, uonevu na ugandamizwaji wa aina yoyote ile. Katika kujadili dhamira hii, msanii ameonesha ukombozi wa kisiasa kiutamaduni, kiuchumi na kifikra( kimawazo).

Katika *Ukombozi wa Kisiasa* msanii anaonesha kuwa uhuru ni njia mojawapo ya kujitoa katika utawala wa kikoloni. Katika shairi la "A*frika" (*uk.6-8) msanii anaonesha umuhimu wa nchi za Kiafrika kujikomboa kutoka mikononi mwa wakoloni ili kujiletea maendeleo. Katika shairi la "N*uru ya Tumaini"* (uk. 9-10) anaonesha nchi inavyokuwa baada yakujikomboa na analinganisha ukombozi sawa na alfajiri njema. Katika ukombozi wa kisiasa, msanii anawataka Waafrika waondoe ukoloni na vilevile wawaondoe viongozi wabovu na madikteta.

Katika *Ukombozi wa Kiutamaduni,* msanii kwa kiasi kikubwa anazungumza juu ya ukombozi wa mwanamke. Msanii anawataka wanawake wajikomboe kutoka katika lindi la uonevu na unyanyaswaji wa kijinsia, kwani wanaonekana ni viumbe dhaifu wasio na mchango wowote katika jamii, haya yanaoneshwa wazi katika shairi la "*Wanawake wa Afrika"* (uk.16).

Katika kujadili suala la ukombozi wa mwanamke, msanii ameonesha kuwa ili waweze kujikomboa lazima wapate elimu na kuzitambua haki zao za msingi. Pia lazima waungane na kuwa kitu kimoja na waachane na mambo


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

ya kifitina baina yao ili waweze kufanikiwa katika harakati zao za kujikomboa. Haya yanaoneshwa katika shairi la *" Wanawake wa Afrika" (* uk. 16).

Vile vile katika shairi la *" Mama Ntiliye"* ( uk. 17-18) msanii anaonesha kuwa ili wanawake wajikomboe kiuchumi lazima wafanyakazi kwa bidii. Msanii anaonesha kuwa mwanamke badala ya kupiga majungu wajibidiishe katika kazi ili waweze kujikomboa kiuchumi.

Katika shairi la "T*ohara"* (uk.2) msanii anaitaka jamii kuachana na mila potofu za kuendeleza tohara kwa wanawake ambazo huleta matatizo kwa wanawake sehemu zao za siri, kwa mfano kupata vidonda ambavyo huwapelekea kupata maradhi ya Pepopunda na "UKIMWI" Pale wanapochangia vifaa vya kutahiria. Msanii anataka jamii iachane na tohara kwa wanawake kwa kuwataka wanajamii kuipiga vita ili kuleta mabadiliko ya kweli katika jamii.

Kuhusu U*kombozi wa Kiuchumi*, msanii anawataka wanajamii waungane na kufanyakazi kwa bidii ili kuondoa umaskini katika nchi yetu. Anataka wanajamii waoneshe juhudi katika kazi mbalimbali viwandani, shambani nk. ili kuinua uchumi wa nchi na kuondokana na umasikini.Haya yanajionesha wazi katika shairi la "*Walala Hoi, Wasakatonge, Mvuja Jasho, Mama Ntiliye, Wanawake wa Afri*ka" n.k

*Ukombozi wa Kifikra* unajitokeza katika shairi la "*Wanawake wa Afrika"* ambapo msanii anawataka wanawake wapewe elimu ili waweze kuzifahamu haki zao na hivyo kuacha kugandamizwa na kunyanyaswa kama wanavyofanyiwa na wanaume.

**Dhamira dogondogo**

**i. Mapenzi**

Mshairi amelijadili mno suala la mapenzi katika maisha. Mwandishi ameeleza mapenzi kama kitu chenye kuwafanya wawili wapendanao kusahau karaha zote za dunia ikiwa watapendana kidhati kwani mapenzi yao yatanoga na kuzaa faraja mioyoni mwano kama mshairi anayofafanua katika shairi la " Y*eye na Mimi" (*uk.36. ). Si hivyo tu bali msanii amezidi kuelezea juu ya suala hili katika shairi la "*Mahaba*" (uk.1) ambapo ameelezea kuwa unapokuwa katika mapenzi huweza kufanya lolote lile ili kulinda penzi, pia penzi huweza kumfanya mtu kuwa tayari kujitoa mhanga

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

au kuonekana na wazimu pale anapokolea kisawasawa.

Pia mshairi anazidi kuelezea kwa kuonesha jinsi penzi linavyoweza kuwa adhabu pale mtu mmoja anapomsaliti mwenziwe ama anapofariki na kumwacha mwenziwe akihangaika au hatakuathirika kiafya haya yameonyeshwa katika shairi la *“Usiku wa Kiza"* (uk. 27)
Licha ya hiyo, mtunzi amwewatahadharisha watu kuwa makini katika mapenzi. mfano katika shairi la “S*itakujua”* (uk. 28) ambapo anamuelezea yule mtu ambaye anajuta, baada ya kumpata yle asiyemtaka maishani mwake. Na pia anataka tusiwe na pupa katika suala la mapenzi kama anavyoeleza katika shairi la “ N*ilichelewa Kupendwa”* (uk. 27)

Licha ya hiyo, mtunzi amewatahadharisha watu kuwa makini katika mapenzi mfano katika shairi la “sitakujua” ( uk.28) ambapo anamuelezea Yule mtu ambaye anajuta, baaada ya kumpata yule asiyemtaka maishani mwake. Na pia anataka tusiwe na pupa katika suala la mapenzi kama anavyoeleza katika shairi la “nilichelewa kupendwa” (uk. 41)

Mshairi amejadili mapenzi kulingana na wakati hu wa sasa. Katika wakati huu, mapenzi yamekuwa kama bidhaa sokoni ambapo unapokuwa na pesa au hali nzuri ya maisha ndipo utapa penzi, lakini kinyume na hapo utabakia na sononeko la moyo kwa kupewa ahadi zisizo za kweli na mfadhaiko wa moyo hata kujiona kutokuwa na muhimu duniani kama ilivyoonyeshwa katika shairi la *“ Nilikesha”* ( uk. 23-24).

Hivyo ni dhahiri kuwa katika hali tuliyonayo sasa na kulingana na na maelezo ya mashairi, ni vigumu kupatikana kwa upendo wa dhati. Maelezo hayo ameyatoa katika shairi la *“Pendo Tamu”* (uk.25) kitikio anaelezea ni vigumu kulipata lililotamu lenye maelewano lililoisha na lenye raha katika dunia kama hii.
Katika kuonesha mapenzi mshairi, kiasi kikubwa amejielezea mapenzi analiyonayo kati yake na Yule ampendaye, wanavyopendana kwelikweli mfano katika shairi la *“Nilinde”* (uk.15), *“Yeye na Mimi”* (uk.39,) *“Pendo Tamu”*(uk. 35), “*Tutabaki Wawili”* (uk.26) yote hayo yanaonesha upendo wa dhati kwa wawili wapendanao. Ni vizuri umpendapo mtu ukamweleza ukweli Kama mshairi katika shairi la *“Kauli Yako”* (uk.27), akimsihi mpenzi wake amdhibitishie kutoka ndani ya moyo wake kama kweli anampenda.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Pia Ni vizuri unapokuwa umempata mpenzi ukawa na heshima na ustarabu baina yenu na si vizuri kupuuzia, mara nyingine inaweza kusababisha mtafaruku baina yenu mfano katika shairi la *"Si Wewe"* (uk.21). Na unapojua mpenzi wako anakupenda kwa dhati basi ni vizuri ukazienzi hisia zake. Si vizuri ukamdhihaki kwa kuchezea upendo alionao kwako kama anavyosema katika shairi la"*Wewe Wajua"* (uk.29.) Na si kumkosesha mtu mwelekeo wake wa maisha, mfano wa hilo ni katika shairi la "*Machozi ya Dhiki"* (uk. 28), msahiri anaelezea jinsi dhuluma ya mapenzi inavyoweza kumtesa mtu na kumsababishia maumivu mithili ya kisicho na dawa.

**(ii) Nafasi ya mwanamke katika jamii.**

Mshairi amemchora mwanamke kama kiumbe dhaifu asiyeweza kujitetea dhidi ya mila potofu zinazomkandamiza na kumuumiza. Mwandishi amelionesha suala hili kama ifuatavyo;

Ameonesha jinsi mila na tamaduni ambazo humuathiri mwanamke kama inavyooneshwa katika shairi la *"Tohara"* (uk. 2). khatib anonesha jinsi wanawake wanavyoathirika na suala hili la tohara kwa kuonesha athari wazipatazo kama kuambukizwa magonjwa mfano UKIMWI. Kutokana na kutumia chombo kimoja wakati wa kutahiriwa/ kukeketwa, kuharibika sehemu za siri, kupatwa na shida wakati wa kujifungua ambapo hupata maumivu makali kupita kiasi.

Vilevile ameoneshwa mwanamke kama mtu fitini asiyependa maendeleo. Hutumia muda wake mwingi katika kuchonganisha watu kwa kupika uongo kuusambaza na ametumia taswira ya shairi la *"Mama Ntiliye" (*uk.17-18) kufikisha maudhui haya na hakuishia hapo tu bali amewaasa wanawake kuacha tabia hiyo mbaya kwani za mwizi ni arobaini na ipo siku watakuja kuadhirika watakapokamatwa na watu wenye kukerwa na tabia zao.

Mwanamke amechorwa kama chombo cha kazi. Katika jamii nyingi hasa za kiafrika mwanamke huwa ndiye mfanyashughuli zote za nyumbani na hata zile za shambani. Licha ya majukumu hayo pia, mwanamke ndio mlezi wa familia kama inavyoelezwa katika shairi la *"Mwanamke" (*uk.16).

Pia mwanamke amechorwa kama chombo cha starehe, ameonyeshwa

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

kama chombo cha kuliwaza/ kuburudisha wanaume pale watokapo katika shughuli zao. Na pia huwa hana thamani katika jamii yake kama inavyoelezwa katika shairi hilohilo la *"Mwanamke".*

Mshairi amemweleza mwanamke kama kiumbe asiye na maadili katika shairi la *" Wewe Jiko la Shamba"* (uk. 44) ambapo amemwonesha mwanamke kama mtu Malaya, ambaye hutembea hovyo na wanaume bila kuangalia madhara yake ambayo huwa ni magonjwa ya zinaa, hasa tatizo kubwa la ugonjwa wa UKIMWI ambao hauna tiba. Mshairi anaelezea zaidi katika shairi la *"Vitamu*" (uk.44) kwa wale wenye tabia mbaya kama hizo waache kwani wanaume huvutiwa mno na wanawake waliolelewa kutunzwa kwa maadili mema, ambao ndio hasa wanaume huwakimbilia nah hivyo basi ni vizuri mtu kujiheshimu ili kulinda hadhi yako.

Mwisho, mshairi anawasa zaidi na kuwashauri wanawake wote wa Afrika kwa ujumla, kwa kuwapa njia mbadala za kuweza kujukwamua dhidi ya matatizo yanayowakabili. Amewaonesha njia za kufuata ambazo ni kuungana, kushirikiana na wajitahidi katika suala zima la taaluma / elimu ili wajielimishe na kuweza kuzitetea kwa umoja haki zao bila kubaguana na kuachana na mambo ya umbea , majungu na fitina; vitu ambavyo vitarudisha nyuma katika harakati za kukwamua, katika shairi la "*Wanawake wa Afrika" (uk10-11).*

**Ujumbe**

- Ukiteta ni kikwazo kikubwa cha maendeleo. Jamii haina budi kung'oa utawala wa kidikteta katika jamii zao.
- Mapenzi ya dhati katika jamii ni suala la muhimu katika jamii.
- Heshima kwa jinsia zote ni muhimu kuzingatiwa ili kuletea usawa wa kijinsia katika jamii.
- Ukoloni mamboleo  na aina zote za unyonyaji ni lazima zipigwe vita katika ujenzi wa jamii mpya

**Falsafa**

Mwandishi anelekea kuamini kuwa jamii yoyote haiwezi kuendelea kama hakuna usawa katika jamii husika.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**Msimamo wa mwandishi**

Mwandishi ana msimamo wa kimapinduzi. Mwandishi ameweza kuonesha matatizo mbalimbali yanayoikabili jamii bila woga. Mwandishi pia amependekeza mbinu za kuondokana na matatizo hayo. Miongoni mwa matatizo yanayotajwa na mwandishi kuwa ni kikwazo cha ujenzi wa jamii mpya ni haya.

- Uongozi mbaya.
- Matabaka
- Unafiki
- Dhuluma
- Unyonyaji

**FANI**

Mwandishi ametumia miundo ya aina mbalimbali. Anaweza kutumia muundo wa tarbia, tathlitha na sabilia. Mifano ya mashairi na aina ya miundo iliyotumika ni kama ifuatavyo.

**(i) *Sabilia*:** Huu ni muundo unaohusisha mashairi yenye mistari mitano na zaidi. Mfano wa mashairi yenye muundo wa Sabitia ni *"Kosa"* (uk.3), *"Nilikesha"* (uk.23), *"Walala Hoi"* (uk.36 -37), "*Nahodha" (uk. 41 -42)* na *"Unyama" (uk.47)*

***(ii) Tarbia:*** Huu ni muundo unaohusu mashairi yanayoundwa na ubeti wenye mistari mine (4) tu. Mfano wa mashairi yenye muundo wa tarbia ni "*Mcheza Hawi Kiwete"* (uk.32) *"Siwi Maji Mafu"* (uk.33), na *"Pendo Tamu"* (uk.35).

**(iii) Tathilitha** : Huu ni muundo unaohusu mashairi yanayoundwa na mistari mitatu (3) katika kila ubeti: Mfano wa mashairi hayo ni *"Hatuna Kauli*" (uk.8), *"Sikujua"* (uk.28) na "*Kansa"* (uk 4).

**Mtindo :**

Mshairi ametuamia mtindo wa aina mbili;

a. Mtindo wa kimapokeo unaofuata urari, vina na mizani. Mfano wa mashairi yanayofuata mtindo wa kimapokeo :

(i) *Buzi Lisilochunika (uk27)*


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

(ii) *Wewe Jiko la Shamba (uk.27)*

(iii) *Siwi Maji Mafu ( uk 33)*

(iv) *Mcheza hawi Kiwete (uk 32)*

b. Mtindo huria (mavue) ni mtindo ambao haufungwi na kanuni za urari wa vina na mizani

(i) *Si wewe (uk.21)*

(ii) *Sikuliwa Sikuzama (uk.22)*

(iii) *Miamba (uk.29)*

(iv) *Marufuku (uk.36)*

(v) *Vinyago (uk. 49)*

Hata hivyo, mashairi mengi ni yale ya kisasa ambayo hayafuati urari wa vina na mizani.

**Matumizi ya lugha**

*Wasakatonge* ni diwani ambayo imeandikwa kwa kutumia lugha inayoeleweka kwa wasomaji wa diwani hii. Imeshehenezwa kwa tamathali za semi na mbinu nyingine za kisanaa.

**Tamathali za semi**

*Tashihisa.* Hii ni tamathali ya semi yenye kuvipa vitu uwezo wa kutenda kama binadamu.

Kwa mfano:

- "*Radi yenye chereko" katika shaiti la "Afrika"*
- "*Pendo lenye tabasamu" katika shairi la "Pendo Tamu"*
- "*Inaumwa Afrika" Katika shairi la "Tiba isiyotibu"*
- "*Kazi kikajitajirisha" katika shairi la "Twende wapi"*

***Sitiari :*** Hii ni tamathali ya mlinganisho. Vitu viwili hulinganishwa moja kwa moja bila kutumia viunganishi vya mlinganisho.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- “*Ndwele ni maskini” katika shairi la “Tiba isiyotibu.*
- “*Uchoyo ni sumu” katika shairi la “Pendo tamu”*
- “*Mate si baragumu” katika shairi la “Mtemea mate mbinguni”*

***Tashibiha*** *:* Hii ni tamathali ya mlinganisho wa vitu viwili tofauti kwa kutumai viunganishi kama vile; kama, mfano wa, mithili ya, sawa na, n.k.

Kwa mfano:

- “*Lanuka kama ng'onda” katika shairi la “Kansa”*
- “*Hubakia kama wanga” katika shairi la “ Nilichelewa kupendwa”*

**Mbinu Nyingine za Kisanaa.**

***Takriri :*** Hii ni mbinu ya kurudiarudia tungo. Katika diwani hi mbinu hii imejitokeza katika mashairi yafuatayo:

- “*Buzi lisilochunika” mshairi anasema* “*Hili buzi, buzi gani lisiloelimika*

Neno “buzi” limejirudiarudia katika mstari mzima.

Takriri nyingine zimejitokeza uk 4 mshairi anaposema, jamii imeoza imeoza ya nuka” (neno oza) uchafu wachomoza, wachomoza, wafuka. (Neno chomoza).

**Ujenzi wa picha na taswira**

Mashairi ametumia yugha ya picha kueleza hisia zake baadhi ya taswira hizo ni pamoja na hizi zifuatazo

i. Nahodha: imetumika kueleza kiongozi

ii. Jahazi : imetumika kueleza nchi

iii. Jiwe si mchi: imetumika kueleza wanawake wasagaji

iv. Tonge la ugali: uchu wa madaraka

vi. Vinyago: wasaliti

**Jina la Kitabu**


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Jina la kitabu *Wasakatonge* linasadifu yale yanaelezwa ndani ya kitabu. Wasakatonge ni watu ambao wanapigania maisha yao ili kupata chakula chao cha kila siku (watu maskini). Jina la kitabu linasadifu yaliyomo ndani kwa sababu mashairi mengi yaneleza matatizo wanayokumbuna nayo watu wa tabaka la chini.

Vilevile kuna shairi pia ndani ya kitabu hiki ambalo ameliita *"Wasakatonge"* ambapo mshairi anaeleza fani na maudhui ya mashairi yake kuwa yatahusu Wasakatonge.

Hivyo basi *Wasakatonge* kama jina la kitabu linasadifu yaliyo ndani ya kitabu kama ambavyo imeelezwa hapo juu kuwa mashairi mengi yanazungumzia matatizo ya watu wa tabaka la chini na pia kuna shairi la *Wasakatonge* ndani ya kitabu hiki.

**KUFAULU NA KUTOFAULU KWA MWANDISHI**

**Kufaulu**

Mwandishi amefaulu kimudhui kwani amewaza kueleza matatizo sugu yanayoigusa jamii yake na kuweza kuonesha mbinu mbalimbali za kuondokana na matatizo hayo.

Mwandishi ameweza kuonesha ufundi wake katika kuandika mashairi mengi kwa kutumia mitindo yote, miundo ya ushairi mbalimbali na lugha iliyojaa lugha za picha (taswira) tamathali za semi na mbinu nyingine za kisanaa.

**Kutofaulu**

Mwandishi ameshindwa kutumia Kiswahili sanifu na badala yake lahaja ya Kiunguja imetawala sana katika mashairi yake. Hili ni tatizo kwani wasomaji wengi wanaweza wasiwe na ujuzi wa kuelewa lahaja mbalimbali.

**Jina la Kitabu: - MASHAIRI YA CHEKACHEKA**

**Mwandishi: - THEOBALD MVUNGI**

**Wachapishaji: - EDP**


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**Utangulizi**

Theobald Mvungi ni miongoni mwa waandishi na wahikiki mashuhuri wa fasihi ya Kiswahili. Miongoni mwa kazi zake ambazo zimetokea kuwa kisima cha hazina ya mali za kijamii ni pamoja na diwani ya *raha karaha* (1978) na *chungu Tamu* (1980). Mwandishi ni mkuza mitaala katika Taasisi ya Elimu Tanzania

**Fani**

Fani ni kipengele muhimu katika kazi yoyote ya fasihi. Hakuna kazi yoyote inayoweza kuitwa ya fasihi bila kuwa na kipengele cha fani. Hizi ni njia atumiazo mwandishi wa kazi ya fasihi ili kufikisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa. Kwa hiyo fani ni mbebaji wa maudhui. Vipengele kadha wa kadha vinavyounda fani vimejidhirisha waziwazi katika kazi ya mashairi ya chekacheka kama ifuatavyo:

**Muundo**

Kitabu cha mashairi ya Chekacheka ina jumla ya mashairi 29. Mashairi yote yana muundo wa tarbia. Kila shairi lina ubeti wenye ubeti wenye mistari mine. Hakuna hata ubeti mmoja amboa una mistari zaidi ya mine au pungufu ya mistari mine. Hivyo basi, muundao uliotumika ni tarbia.

**Mtindo**

Mwandishi wa mashairi ya Chekacheka amejitahidi kutung a mashairi yake kwa muundo wa kimapokeo. Mtindo wenye kufuata kanuni za urari wa vina na mizani na mpangilio wa vina vya mwishoi na /au vya kati.

Hii ina maana kwamba mashairi yote katika diwani hii yana ulinganifu wa idadi ya silabi na vina vya mwihso na /au vya kati kwa kila mstari. Ametunga mashairi na tenzi. Kimuundo, mashairi yana mishororo(mistari) minne kwa kila ubeti. Kila mshororo una mizani 16 na umegawanyika katika vipande viwili vyenye mizani 8 kwa kila kipande kama inavyoonekana katika ubeti huu wa shairi la *"Niwa kaombe Mtini"* (uk 12)

*"Nimejaribu kuongea, ndege awe mkononi,*

*Yeye juu hurukia, namuomba samahani,*

*Nyimbo ananiimbia, nyimbo zachoma moyoni*


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

*Basi mie taabaani, njiwa akitabasamu"*

Kwa upande wa tenzi, mwandishi ametunga tenzi zenye mizani kwa kila mistari. Zina urari wa vina vya mwisho. Maana yake ni kwamba kuna ulinganifu wa silabi za mwisho kwa kila msitari kama tuonavyo katika ubeti huu wa shairii la "sengenge"(uk 19)

"*nipitshe wewe sengenge,*

*Nipishe kando jitenge*

*Nipishe usinifunge*

*Usiwe haambiliki'*

Takribani katika mashairi yote ya diwani hii, kila ubeti una kiitio chake tofauti. Hakuna kibwagizo kinachorudiwarudiwa kama tulivyozoea katika mashairi mengi.

***Matumizi ya lugha***

Lugha ndiyo malighafi ya mshairi yeyote. Mtunzi mzuri wa shairi ni Yule anayeweza kuchagua na kupanga maneno yake kwa ustadi ili yaweze kuleta ile athari iliyokusudiwa. Kinyeme chake shairi huwa chapwa na lenye kuchusa.

Theobald mvungi amefanikiwa katika matumizi ya lugha. Ametumia lugha nyepesi na yenye kueleweka kiurahisi. Aisha ameweza kuteua maneno ya kutumia katika mashairi yake kwa kuzingatia kile alichotaka kusema. Mashairi yake ni ya kimapokeo yanayozingatia urari wa vina na mizani. Lakini bado kafanikiwa kuteua maneno yanayoweza kuingia katika mfumo huu bila kuathiri maudhui ya mashairi yake. Hapa na pale katika kazi yake mwandishi katumia mkato wa maneno, bila shaka hii ni katika kuhakikisha anatunza dhima yake ya kuwa na mashairi yenye muundo wa kimapokeo

*Mfanowa mkato wa maneno ni:-*

*"mejaribu" badala ya "nimejaribu" (uk.12)*

*"…………siniguse" m badala ya "usiniguse"(uk.20)*



Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

*"………...tayafumba" badala ya "utayafumba" (uk.20_*

*"……….tayapata" badala ya "utayapata" (uk.10)*

**Matumizi ya tamathali za semi**

Tamathali za semi zimetumika kwa wingi katika mashairi ya Chekacheka. Baadhi ya tamathali za semi ambazo zinajibainisha waziwazi ni pamoja na:-

***Tashibiha***

*Kwa mfano,*

*"watu sawa na kamasi" (uk. 2)*

*"mlevi akakolea kama tumbaku ya tozo" (uk.2)*

*"mfanowe kama radi" (uk. 13*

*"hotuba zamiminika mfano maji bombani"(uk. 2)*

**Tashihisi**
Hapa vitu visivyo binadamu vinatenda kama binadamu. Katika shairila *'Njiwa kiumbe mtini'* (uk.12) njiwa anapewa uwezo wa kuimba nyimbo zinazochoma moyoni na pia kutoa tabasamu linalomuacha hoi mshairi. Tashihisi inajitokeza pia katika shairi la *'moyo'*(uk.13) moyo unasemekana kuwa una kiburi unashauriwa lakini unakaidi ( ubeti wa pili) katika ubeti wa tatu moyo unaambiea ujifunze busara ili uwe ndiyo taa yake. Katika ubeti wan ne, moyo unaaswa usiwe jeuri. Hapa moyo unapewa sifa ya kufanya kama binadamu (uk. 13)

**Sitiari**
Kwa mfano

*'……….maisha ni safari' (uk13)*

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

*'………..sisi ni miamba gogo*" (uk. 5)

**Mbinu nyingine za kisanaa**

**Tashtiti**

Tamathali hii nayoimetumiwa na mshairi katika diwanni yake. Mashairi mbalimbali ni ya ki-tashtiti kwa namna Fulani kwa mfano. Shairi la *'mtoto aso riziki ( uk.26)* ni tashtiti kwa wale walioko madarakani

**Takriri**

Katika ushairi, takriri huwa ni kurudia rudia kwa silabi ( vina ) neon au mstari. Aina ya takriri inayopatikana kwa wingi katika *Mashairi ya Cheka cheka* ni takriri vina na takriri neno

**Takriri vina**

Takriri vina inajidhihirisha wazi katika diwani hii. Hii ni kwa sababu mashairi yote katika diwani hii yana ulinganifu wa vina vyakati na/au vya mwisho kwa kila mstari. Mfano mzuri tunaweza kuupata katika shairi la *'moyo'* (uk.13) katika ubeti wa kwanza silabi ri na di nitakriri kama unavyoonekana hapa chini:

*"moyo nimeushauri, lakini umekaidi,*

*Moyo kiburi hatari, mfanowe kama radi,*

*Moyo mefumbata shari, unayakwepa marudi,*

*Moyo u mwilini mwangu, jirudi tuwe pamoja*"

**Takriri neno**

Mvungi ametumia pia mbinu ya kurudiarudia neno kwa lengo la kusisitiza jambo Fulani. Kwa mfano, katika ubeti wa shairi la *'moyo'* tulioudondoa hapo juu, amerudiarudia neno*'moyo'* ili kutia msisitizo.

Takriri neno inapatikana pia katiak shairi la *'mashairi ya Ngulu'*(uk.27) katiak ubeti wa kwanza wa shairi hili, neno '*ngulu*' limerudiwa mara kadhaa kwa lengo la kusisitiza jambo

**Ujenzi wa taswira**

Mshairi anadhihirisha ufundi wake wa kuunda picha za mambo mbalimbali


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

katika mawazo ya hadhira yake kwa kutumia maneno. Anaweza kutuchorea picha zinazotufanya tuhisi, tuone na hata kunusa na kusikia kile kinachozungumzwa. Ubingwa wake katika matumizi ya taswira unadhirihishwa na sehemu za beti hizo za shairi la *Tuambae ukasuku'*(uk.3)

*"Hakuna athubutuye,ati nyani kumtuma,*

*Aibebe mizigoye, au chuchu kumkama,*

*Na sogi amjaziye ampandishe kilima,*

*Nyani si mkubalifu, mfugaji atazikwa"*

*"kadhalika tafakari, mshairi uwe nyati,*

*….. Ati ukweli ni shar, mshairi uwe nyati,*

*…..mshairi jihadharini, isishikwe kama fimbo"*

*"….. usiwe kama kunguru, woga umejaa tumbo" (uk. 3)*

Tunaziona taswira za kimaumbile katika beti za shairi hili. Mwandishi amechora taswira ya nyati aliye mkali kupindukia kiasi kwamba mtu hathubutu kumtuma kitu. Aidha mwandishi amefaulu kuelezea namna washairi wanavyopaswa kuwa wakali kwa kutumia picha ya nyati asiyeweza kukamuliwa wala kubebeshwa mzigo

Kwa upande mwingine, mwandishi anajenga taswira ya kunguru aliye mwoga na akafaulu kuitumia picha hiyo kuelezea woga walionao washairi wengi. Mwandishi pia amejenga taswira za hisi. Kwa mfano katika shairi la *'Kuna nini huko ndani?*' (uk4) mshairi anajenga taswira ya harufu ya kunukia. Taswira hii inawajengea hadhira hisia zaidi za tama. Hebu tuchunguze ubeti huu;

*"kuna nini huko ndani, mbona jiko lanukia,*

*Rihi yajaa puani, na muda wajiendea,*

*Kisoiva kitu gani, mbona mate mwatutoa,*


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

*Naona mwajigawia, wapishi ninawahofu*

Aidha, mwandishi amejenga pia taswira za mawazoni katika shairi la *'kimoyo'*( uk.12), kwa mfano, mshairi anaongea na moyo wake jambo ambalo ni la mawazoni tu.

**Jina la kitabu**

Jina la kitabu *Mashairi ya Chekacheka* yananawiana na yale yaliyomo ndani ya kitabu hiki. Mwandishi kwa kutumia mbinu ya kisanii ameweza kueleza mambo ambayo si rahisi kuelezwa kwa lugha ya kawaida. Neno chekacheka huonesha furaha au raha wakati yanayoongelewa ndani ya kitabu hiki hayafurahishi wala hayaleti raha kwa wasomaji ila yanaleta karaha, huzuni, majonzi hasira na chuki. Kitabu kizima kinajadiliwa maovu mbalimbali yanayotendwa na viongozi wetu ambayo ni kinyume na taratibu au maadili ya uongozi. Mambo hayo ni kama vile rushwa, ulaghai wa kisiasa, uongozi mbaya, matumizi mabaya ya mali ya umma, wizi wa mali ya umma, ukasuku na usaliti.

**Maudhui**

*Mashairi ya Chekacheka* ni diwani yenye kubeba maudhui yenye kusawiri kikamilifu mambo ambayo yanajitokeza hapa Tanzania na hata kwingineko duniani. Ni diwani yenye dhamira nzito na ujumbe mpana kwa hadhira lengwa.

**Dhamira**

Dhamira au mawazo yanayomchochea mwandishi kuandika *mashairi ya Chekacheka* nyingi za zinafaa kujadiliwa kwa jicho la ukomavu. Hata hivyo baadhi yake zimejitokeza na kujadiliwa sana katika kazi hii. Hizi ni pamoja na dhamira ya *ukweli, siasa, mapenzi, dini, uhusiano wa kimataifa na maisha*

**Dhamira ya ukweli**

Theobald Mvungi anajenga dhamira ya ukweli bila woga. Hii inajionyesha katika shairi lake anapomsifu mwandishi Penina Muhando kwa kazi yake nzuri ya*Lina ubani.* Mwandishi anasema muhando kasema ukweli kuhusiana na walaji majahili bila kuwapaka mafuta kwa mgongo wa chupa. Hivi ndivyo inavyostahili kwa msanii aliye makini. Katika shairi lake la *'kazi yetu harakati'*(uk.21) tunasikia sauti ya mshairi ikisema.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

*Ameweka dawa kali, kidonda kipate hali,*

*Mhando kasema kweli, ile kweli ilo kali,*

*Kwa walaji majahili, dawa yao ni ukali,*

*Kwa kiziwei aelewe, ni vitendo umwonyeshe*

Ubeti huu unatuonyesha fika kwamba mwandishi anapenda na kuthamini ukweli, nah ii huenda ndiyo sababu akaamua kuzungumzia katia mashairi yake, kwa mfano, siasa bila woga wala kificho

**Dhamira ya siasa**

Dhamira ya siasa kama ilivyo katika diwani zake nyingine imejadiliwa vilivyokatika diwani hii. Mvungi analichora suala la siasa kwa jicho pevu mara kwa mara. Mshairi anaonekana kuyajadili masuala ya siasa kwa ukali. Chini ya mwavuli wa siasa mwandishi anajadili masuala yafuatayo:

**(i) Mfumo wa siasa ya chama kimoja**

Mwandishi anaijadii vilivyo siasa ya mfumo wa chama kimoja. Kwa maoni yake ni kwamba mfumo huu uliwanyima watu uhuru wa kushiriki ipasavyo katika siasa ya nchi yao. Katika ubeti wa 7 wa shairi la *'Taifa wamelizika'* (uk.2), mwandishi anasema;

'*mezikwa demokrasia, chama kimoja ndo 'o ngao,*

*Watu hawana nafasi, kutetea nchi yao,*

*Mawazo ya ukakasi, mawazo ya mtitio,*

*Wapenda jibu mkato, wale waoga wa hoja*

Mvungi pia anawaponda wale wote waliokuwa wnaogopa mfumo wa siasa wa vyama vingi. Anaona kwamba hao hawana lolote isipokuwa tu wanaogopa kuumbuliwa mara tu vyama vingine vitakapokuwa vimechukua madaraka. Tunasikia sauti ya mshairi ikisema:


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

*Waogopao vingi vyama, ni hofu ya kuumbuka,*

*Maovu wanayafuma, kwa dharau na dhihaka;*

*Vyama vingi vingesema, na kutwaa madaraka,*

*Pasipo uhuru huo, utu upo mashakani.( uk.2)*

Inaelekea shairi hili lillitungwa wakati Tanzania ikiwa bado chini ya mfumo wa chama kimoja cha siasa. Ndiyo sababu mwandishi anaelezea kutoridhishwa kwake na hali iliyokuwepo nchini ambapo viongozi na hata raia walikuwa wanag'ang'ania mfumo wa siasa ya chama kimoja kwa visingizio kedekede. Lengo hasa la mfumo wa chama kimoja kama alivyoeleza mwandishi katika ubeti wa mwisho wa shairi hili ni kuwafanya wananchi wawe wavivu wa kufikiri na hivyo kuwawezesha watawala kufanya mambo yao watakavyo huku wananchi wakibaki kupiga makofi tu.

Tangu shairi hili litungwe, leo tuna zaidi ya miaka kumi tngu mfumo huu uruhusiwe rasmi nchini. Mazuri tunayaona na pia mabaya yake tumeyaona. Ukweli ni kwamba kila jambo zuri pia lina ubaya wake. Hata hivyo, pamoja na kasro zilizojitokeza katika kipindi hiki ikiwa ni pamoja na mauaji ya Zanzibar ya tarehe 26 na 27 Januari 2002, bado mfumo wa siasa ya vyama vingi umeonyesha manufaa makubwa

**(ii) Demokrasia**

Licha ya kujadili siasa ya mfumo wa chama kimoja katika shairila *'Taifa Wamelizika'*(uk.2) Pia amejadili suala la demokrasia. Mwandishi anaanza kwa kuwaomba wabunge wa CCM (chama tawala kwa sasa) na wajumbe wa mikutano mbalimbali ya chama kutopiga blaa blaa wakiwa viakoni. Hii ni kwa sababu demokrasia haina maana ya kuongea kwa nguvu na kwa kelele bila vitendo. Dhamira hii inasawiri barabara hoja za watu mbalimbali ambao wamekuwa wakiwalalamikia wabunge kwa tabia yao ya kulalamika kidogo kusifu sana na kuunga mkono hoja zote zinazoletwa bungeni na Serikali. Hawa ni bendera fuata upepo kwani wao binafsi hawaoneshi kuyaangalia masuala wanayoyajadili kwa jicho pevu kabla ya kuchukua jukumu la kuunga mkono



Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Mwandishi anaona kwamba wabunge na wajumbe wa aina hii hawawakilishi raia waliowachagua bali wanawakilisha nafsi zao. Wanachojali ni utukufu na furaha zao na sio shida za wapiga kura wao.

Aidha mwandishi pia analijadili suala la maduka ya ushirika na vijiji. Haya yalikuwa hayana bidhaa nyingi muhimu ingwa ndiyo yaliyokuwa tegemeo la wananchi wa kawaida katika miaka ya 1979-1988. Watawala hawakujali kitu wananchi walipokuwa wanataabika.

**(iii) Suala la kutetea haki**

Mwandishi anamwomba Rais Mwinyi, aliyekuwa madarakani wakati huo kuwa imara na kkulind moto aliouwasha ili usizimwe( *shairi la mwinyi umewasha moto! Angalia Usizimwe(uk.1)* inaelekea moto anaozungumzia mwandishi katika shairi hili ni haki. Hivyo anaombwa awe mkali ili kuhakikisha kwamba haki inatendeka katika jamii. Tunaisikia sauti ya mwandishi ikisema;

*Tumaini la wanyonge, kwamba ipo serikali,*

*Ile nchi ya mazonge, ya wenye meno makali,*

*Wanyanganyao matonge, wanyonge hawana hali,*

*Mwinyi ukiwa mkali, ndio raha ya raia(uk. 1)*

Tunaona katika ubeti huumshairi anamhimiza Rais Ali Hassan Mwinyi kuwa mkali kwani nchi anayoiongoza inaonekana kuwa ina mizengwe. Mwandishi pia amejadili suala la wale ambao Rais Mwiyi atawaondoa katika utawala. Wale ambao atawaondolea madaraka bila shaka hawatafurahia kuondolewa kwao madarakani. Mwandishi ana haya ya kusema kuwahusu;

*" …. Wale unaokusudia kuwatoa kwenye viti,*

*Kwa kweli wanachukia sasa wanajizatiti (uk.1:ubeti 2)*


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Akisha mtahadharisha Rais Mwinyi kuhusiana na wale anaotegemea kuwaondoa, madarakani, ndipoanamkubusha atazame nyuma alikotoka. Aende mitaani, azungumze na watu ili aweze kupata kero zao na kuzishughulikia. Mshairi anasema:

*Tazama kila konani, kumbuka vita ni vita;*

*Jambo la mwisho adili, kweli ibaki ni kweli,*

*(Shairi la 'Mwinyi Umewasha moto' ubeti wa 6*

**(iv) Uzembe na ukasuku**

Mvungi katika shairi lake la '*Tuambae Ukasuku'* anatoa wito tusiwe makasuku. Kasuku hana jipya bali kurudiarudia tu yale yaliyosemwa. Anawashauri wasanii wasiwe makasuku pia. Maana yake ni kwamba wasiwe tu vipazasauti vya walio madarakani, bali wawe wakali kama nyati ambaye hakuna anayeweza kumchezeachezea. Zaidi mshairi anawaonya wasanii wasirambishwe sukari wakasahau wajibu wao, wajibu wa kuikosoa jamii. Hebu tuisikie sauti yake;

"*mshairi jihadhari, usishikwe kama fimbo,*

*Kwa kulambishwa sukari, ukaimba zao nyimbo,*

*Ukafikiri fahari, unakuwa chao chombo,*

*Kuwabeba huna budi, na vutalamba" ( ubeti wa 6, Uk.3)*

Mwandishi pia anakemea suala la uzembe. Kwa mawazo yake, uzembe unasababisha mazo ya wakulima kutosafirishwa nje kwa ajili ya mauzo. Anataja mifano michache ya pamba, mahindi na ufuta katika kuthibitisha


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

hili. Tatizo ni kwamba kila mtu anasubiri asukumwe ndiyo atimize wajibu wake, na hili ni hatari. Shairi la "Ni wa wapi Ushauri", (uk.23)

**(v) Rushwa na ulanguzi**

Tatizo la rushwa na ulanguzi linajadiliwa kwa undani katika diwani hii ya *mashairi ya Chekacheka.* Imedhihirika wazi kwamba ni watu wenye dhamana serikalini na katika mashirika ya umma walio vinara vya rushwa na ulanguzi ( Shairi la 'Mwinyi Umewasha Moto; uk.1) Ni hiyo hiyo fedha ya rushwa na ulanguzi waitumiayo kununulia magari ya kifahari na kujenga majumba yenye thamani kubwa ikiwa ni pamoja na kuendesha maisha ya anasa. Mwandishi anamshauri Rais Mwinyi

( hapa yeyote mwenye madaraka juu ya hao wala rushwa na walanguzi ) kuwachukulia hatua. Mwandhishi anasema:

*"…………walaji hupendwa sana, na tuhuma zikizidi,*

*Ahamishiwa kwa jana, na akale kwa juhudi, walaji wanajuana, hawa dawa ya rudi"(uk.1)*

Ni ka bahati mbaya kwamba ushauri na mapenzi ya mshairi hayakutekelezwa kwani mashirika ya umma hayapo tena. Walaji walishafafilisi kabisa. Sasa ni enzi za wawekezaji kutoka nje. Huenda hili la wawekezaji likalinufaisha taifa kwani matunda yameanza kuonekana, ingawa pia kuna matatizo kedekede.

**(vi) Ufujaji wa fedha za umma**

Mshairi anayamulika mashirika ya umma na kugundua kwamba kuna ufujaji wa fedha za umma kwa kiwango cha juu sana. Fedha za serikali au za mashirika ya serikali zinatumika isivyopaswa. Baadhi ya viongozi wanajikopesha na wengine wanajiipa mishahara na masurufu mazuri wanapokuwa kwenye shughuli za kiofisi nje ya vituo vyao vya kazi. Baadhi ya shughuli wanazojipangia nje ya vituo vyao vya kazi zinakuwa sio muhimu. Wanafanya hivyo tu ili waweze kupata njia ya kuzifafuna fedha za umma. Ndipo Theobald Mvungi anasema:

"*sherehe zenu utamu, raha za wachache,*

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

*Ni mateso ya kaumu, wasoweza kujikimu,*

*Mikoa yafanya zamu, kuziandaa karamu,*

*( shairi la "Gunia la Mikutano", uk.25)*

Hapa msanii anataka kutueleza kwamba wananchi wanaandaa sherehe za kuadhimisha kumbukumbu mbalimbali kama za muungano, Uhuru, nk lakini wanaofaidi ni wakubwa. Walalahoi hawaambulii chochote/

**Mapenzi**

Mashairi yanayobeba dhamira hii ni pamoja na shairi la *"njiwa kiumbe mtini*"( uk.12). "kimoyo" (uk.12) na "penzi lisiloheshima" (uk.14) katika shairi la *" Njiwa Kiumbe mtini" mathalani, tunamwona mshairi akitoa hisia zake kali hasa kuhusu huyu "njiwa" aliye mtini.* Hii ni tashtiti inayowajengea wasomaji taswira ya aina Fulani Mwandishi anatuonyesha hamu ya kumtia viganjani "njiwa" huyo ili awe wake. Hata hivyo mwandishi anatueleza:

*"…. Yeye juu aliruka, namuomba samahani,*

*Nyimbo ananiimbia, nyimbo zachoma moyoni,*

*Basi mie taabani,njiwa akitabasamu (uk. 12)*

Hapa, inaelekea mshairi analalamikia mpenzi wake ambaye anaitesa sana roho yake. Anajaribu kumchukua lakini wapi. Msanii anajenga taswira ya "*njiwa*" arukaye hapa na pale, matawini, ili kumjaribu mshairi. Yeye mwenyewe mshairi anatwambia:

"*Si kwamba anikimbia, ni mbinu zake teule,*

*Tabu kuniongezea, hata chakula nisile,*

*Njiwa kushuka hashuki, na mtini haondoki (uk.12)*

Tunamwona mshairi akisononeka kwa hili. Pia tunamwona "*Njiwa*" wa mshairi aking'ang'ania mtini. Ni mzuri kupindukia. Tunamwona mshairi akiwa chini ya mti macho juu huku tama yakumpata Yule "*njiwa*" ikiwa imemtawala.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Kwa lugha ya kawaida, mshairi ana mpenzi wake anayempenda sana lakini kila akitaka akamilishe mipango ili waoane, mpenzi wake huyo hatoi msimamo na uamuzi wa moja kwa moja. Ndipo tunamsikia akisema:

*"Unayofanya si kweli, njiwa wacha tafrani,*

*Moyo waunyima hali, kwanini unauhini?*

*Rudi usiende mbali, moyo uwe afueni*

*Njiwa hebu baini, moyo unavyoteseka" (uk. 12)*

Aidha, katika shairi la *"penzi' Lisilo Heshima"* (uk. 14)mshairi anatutanabaisha maana ya mapenzi. Analijadili suala la mapenzi ya kweli . kwa maoni yake, penzi la kweli ni lile lisiloathiriwa na vitu kama vile pesa, nguo, gari na kadhalika. Hata hivyo, kama asemavyo mwandishi, mambo yako kinyume. Siku hizi kuna msemo kwamba *"hapendwi mtu bali pochi lake"*Mvungi alishayaona haya zamani, naye anasema

"Penzi la umasikini, kwa hii dunia,

Ni penzi la nukusani, mpendwa hatopokea,

Mpendwa hamuelewani, ka maneno kumwambia,

Mfuko huna kitu, mpenda wahangaika'

( Shairi la "*penzi lisilo Heshima*". UK. 14)

Ni kwa bahati mbaya kwamba ushauri na mapenzi ya mshairi hayakutekelezwa kani mashirika ya umma hayapo tena. Walaji walishayafilisi kabisa. Sasa ni enzi za wawekezaji kutoka nje. Huenda hii la wawekezaji likalinufaisha taifa kwani matunda yemeanza kuonekana, ingawa pia kuna matatizo kudekede.

**(vi) Ufujaji wa fedha za umma**

Mshairi anayamulika mashirika ya umma na kugundua kwamba kuna ufujaji wa fedha za umma kwa kiwango cha juu sana. Fedha za serikali au za mashirika ya serikali zinatumika isivyopaswa. Baadhiya viongozi


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

wanajikopesha na wengine wanajilipa mishahara na masurufu mazuri wanapokuwa kwenye shughuli za kiofisi, nje ya vituo vyao vya kazi. Baadhi ya shughuli wanazojipangia nje ya vituo vyao vy kazi zinakuwa sio muhimu. Wanafanya hivyo tu ili waweze kupata njia ya kuzitafuna fedha za umma. Ndipo Theobald Mvungi anasema:

*"sherehe zenu utamu, raha za wachache,*

*Ni mateso ya kaumu, wasoweza kujikimu,*

*Mikoa yafanya zamu, kuziandaa kaamu,*

*(Shairi la "Gunia la Mikutano", uk.25)*

Hapa msanii anataka kutueleza kwamba wananchi wanaandaa sherehe za kuadhimisha kumbukumbu mbalimbali kama za Muungano, Uhuru, nk. Lakini wanaofaidi ni wakubwa. Walalahoi hawaambulii chochote.

Mapenzi

Mashairi yanayobeba dhamira hii ni pamoja na shairi la "*Njiwa kiumbe Mtini"* (uk.12), *"kimoyo"* (uk.12) na "Penzi lisiloheshima" (uk.14) katika shairi la *"Njiwa kiumbe Mtini"* mathalani , tunamwona mshairi akitoa hisia zake kali hasa kuhusu huyu "*Njiwa"* aliye mtini. Hii ni tashtiti inayowajengea wasomaji taswira ya aina Fulani. Mwandishi anatuonyesha hamu ya kumtia viganjani "njiwa" huyo ili awe wake.

Hata hivyo mwandishi anatueleza:

*"………….. Yeye juu aliruka, namuomba samahani,*

*Nyimbo ananiimbia, nyimbo zachoma moyoni,*

*Basi mie taabani, njiwa akitabasamu (uk. 12)*

Hapa, inaelekea mshairi anamlalamikia mpenzi wake ambaye anaitesa sana roho yake. Anajaribu kumchukua lakini wapi. Msanii anajenga taswira ya *"njiwa"* arukaye hapa na pale, matawini, ili kumjaribu mshairi. Yeye mwenyewe mshairi anatwambia:

*"….. Yeye juu aliruka, namuomba samahani,*


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

*Nyimbo ananiimbia, nyimbo zachoma moyoni,*

*Basi mie taagbani, njiwa akitabasamu (uk. 12)*

Tunamwona mshairi akisononeka kwa hili. Pia tunamwona "njiwa" wa mshairi aking'ang'ania mtini. Ni mzuri kupindukia. Tunamwona mshairi akiwa chini ya mti macho juu huku tama ya kumpata yele *"njiwa"* ikiwa imemtawala. Kwa lugha ya kawaida, mshairi ana mpenzi wake anayempenda sana lakini kila akitaka akamilishe mipango ili waoane, mpenzi wake huyo hatoi msimamo na uamuzi wa moja kwa moja. Ndipo tunamsikia mshairi akisema:

*"Unayofanya si kweli, njiwa wacha tafrani,*

*Moyo waunyima hali, kwaninii unauhini?*

*Rudi usiende mbali, moyo uwe afueni,*

*Njiwa hebu baini, moyo unavyoteseka"* (uk. 12)

Aidha , katika shairi la "penzi Lisilo Heshima" (uk. 14), mshairi anatutanabaisha maana ya mapenzi. Analijadili suala la mapenzi ya kweli. Kwa maoni yake, penzila kweli ni lile lisiloathiriwa na vitu kama vile pesa, nguo, gari na kadhalika. Hata hivyo, kama asemavyo mwandishi , mambo yako kinyume. Siku hizi kuna msemo kwamba " *hapendwi mtu bali pochi yake"* Mvungi alishayaona haya zamani, naye anasema:

*"penzi la umasikini, kwa hii dunia,*

*Ni penzi la nukusani, mpendwa hatapokea,*

*Mpendwa hamuelewani,kwa maneno kumwambia,*

*Mfukoni huna kitu, mpendwa wahangaika"*

*(shairila "penzi Lisilo Heshima",* uk.14)


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Kutokana na mapenzi ya siku hizi kutawaliwa na vitu ( mali) ndiyo sababu ndoa nyingi za siku hizi zinayumba sana. Watu wakipendana kwa sababu ya vitu ni lazima hawataendelea kupendana iwapo vitu vilivyosababisha wapendane havitakuwepo au iwapo vitapungua. Kwa ujumla, kama asemavyo mshairi, penzi litakalotanguliza pesa, hilo si penzi bali ni chuki. Ni penzi la uzandiki na jamii haina budi kulipiga vita penzi la namna hii( rejea ubeti wa 3 na 4 wa shairi la "penzi Lisilo Heshima" uk. 14) Msanii anataka yawepo mapenzi ya kweli. Watu waambizane ukweli mtupu. Wasidanganyane kwa lengo la kuvutana.

**Dini**

Suala la dini linajitokeza katika shairi la "Chanzo cha Huo Uozo" (uk.24) mwandishi anajadili uozo katika dini ya kikristo, kwa maneno yake anasema:

*"Nimeona upotofu, humu ukristoni,*

*Upotofu wenye hofu, wahubiri mu kundini,*

*Mlei na Askofu, nyote mfanye makini,*

*Dini iwe maadili, msisitizo si fedha"( uk.24)*

Hapa mshairi anazungumzia suala la michango kanisani. Ni kweli kwamba katika baadhi ya madhehebu ya kikristo pesa inawekwa mbele sana. Wakristo ni kama wanalazimishwa kutoa badala ya kusisitiza suala la kuacha dhambi na kumrudia mmungu ambalo ndilo kusudi kubwa la dini ya kikristo. Suala hili alishaliona hata msanii wa nyimbo za dini, Faustine Munishi aliposema kwamba whubiri wengi wanahubiri kutoa kila siku. Hivyo ni katika albamu yake ya " Malebo" Baadhi ya kuishuhudia hali hiyo, msanii ndipo akasema:

"Ninalaani mkazo, huu mkazo wa mali,

Mkazo una mzozo, unikumbushao mbali,

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Chanzo cha huo uozo, kusahau maadili,

Padri punguza hamu ya shilingi kuzipenda

( ubeti wa sita wa shairi "chanzo cha Huo uozo uk.24)

**Uhusiano wa Kimataifa**

Tunasikia sauti ya mshairi akitoa kilio kikubwa ka kiongozi shupavu wa India, Indira Gandhi. Hii ni katika shairi la "Indira" (UK. 17) kiongozi huyu alikuwa ameuawa miaka michache nyuma. Katika shairi hili, mwandishi hasiti kuonesha uhusiano uliokuwepo kati ya Tanzania na kiongozi huyo. Kisha mshairi anamlilia akisema:

*"Wengi tumesononeka,*

*Oktoba Kutokana,*

*Umeondoka haraka,*

*Kwa kweli ulitukuka" (uk.17)*

Mvungi anamwelezea shujaa Indira Gandhi anaposema:

*"Haki ulipigania,*

*Pia demokrasia,*

*Ujamaa ulizingatia,*

*Ndiyo msingi imara"* (uk. 17)

Mwandishi pia anaelezea uhusiano mchafu uliokuwepo miongon mwa weupe na weusi huko Afrika ya Kusini. Hapo ilikuwa ni enzi zile za ubaguzi wa rangi. Ndipo anapojadili katika shairi lake la " *utumwa Huru"* (uk. 22)

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

kwamba uhusiano huo utaleta madhara kwani utulivu hauwezi kuwepo. Hebu tumwone mshairi anamwonaje kaburu:

*" Kaburu atenga rangi, mnyama Yule katili*

*Tena ana kwa wingi, katili hana akili,*

*Weupe ndio making, Mwafrika hatawahi*

*Ni uovu wa kaburu, aibu barani kwetu"* (uk. 22)

Hapo ilikua ni enzi zile. Je msanii bado anamwona kaburu kuwa ni mnyama wakati ndiye mwekezaji mkubwa hapa Tanzania? Hata hivyo, mambo yalishakuwa mazuri nchini Afrika ya Kusini baada ya kupatikana kwa utawala wa wengi hapo mwaka 1994.

**Maisha**

Baadhi ya mashiri katika diwani hii yana mawazo ya jumla kuhusu maisha, kwa mfano, mashairi ya "utu umekuwa kima" (uk.18) na "*Dhahabu ya Fahari"* (UK.18). katika shairi la "utu umekuwa kima" mshairi anatoa onyo kwa wale wenye tabia ya kudharau utu. Aidha, katika shairi la *"Fahari ya Dhahabu"* mshairi anatufumbua macho kwamba si kila king'aacho ni dhahabu. Watu wanaweza kulikubalia jambo baya kwa lengo la kujionesha tu kwa jamii.

Shairi linguine lenye kuzungumzia kuhusu maisha ni lile la *" utaliwa kama pumba"* (uk. 20) mshairi anaonesha kutishika na mauti. Kufuatia tishio la mauti, ndipo tunamsikia akisema:

*" mauti nipishe mbali, ujiitaye umoja,*

*Mauti usio akili, kila uchao viroja,*


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

*Mauti mwana katili, wewe usojali hoja,*

*Mimi wewe shirikani, mwisho haiwezekani"*

(uk. 20)

## KUFAULU NA KUTOFAULU KWA MWANDISHI

### Kufaulu kwa mwandishi

- Mshairi wa diwani hii amefaulu kwa kiasi kikubwa katika kuonesha mambo mbalimbali yanayoikumba jamii yake. Baadhi ya mambo hayo ni uongozi mbaya, usaliti, unyonyaji n.k. msanii anasema kuwa matendo mengi maovu hufanywa na tabaka tawala na baadhi ya watu wa tabaka la chini ambao ni vibaraka wao. Hata hivyo, msanii anasema kuwa ili kukomesha watu hawa sharti wananchi wa kawaida waungane na kuanzisha vita dhidi ya watu hao.
- Mshairi amefaulu kuonesha mambo mbalimbali yaliyoikumba nchi yetu mwishoni mwa miaka ya 1970 na mwanzoni mwa miaka ya 1980. Mambo hayo ni kama vile hali mbaya ya uchumi.
- Kwa upande wa fani, msanii amefanikiwa kuktumia lugha ya kishairi ambayo imefanikiwa kuibua maudhi yaliyokusudiwa. Vilevile, mtindo wake wa kimapokeo umempatia umaarufu hasa kwa wanamapokea.

### Kutofaulu kwa mwandishi

- Kifani mwandishi hajafaulu hasa katika hatua yake ya kuamua kutumia ushairi wa aina moja tu, ushairi wa kimapokeo. Hali hii inafanya taaluma hii kkuonekana kama kitu kisichobadilika kulingana na mabadiliko yanayotokea. Baadhiya washairi wanayaona mabadiliko kulingana na mabadiliko yanayotokea. Baadhiya washairi wanayaona mabadiliko hayo kama upuuzi mtupu kitu ambacho si kweli. Kilichotakiwa kwa malenga huyu ni kutumia aina zote za ushairi sit u kwa lengo la kukuza ushairi wa Kiswahili bali pia kuonesha usomi wake katika kupokea mabadiliko yeneye manufaa kwa jamii yake.
- Vile vile mashairi mengi yamejaa falsafa ya Kimax inayosisitiza mapinduzi ya kumwaga damu kama njia pekee ya kuleta mabadiliko. Jambo hili si la kweli kwa asilimia mia kwani falsafa hiyo haijawahi kuleta utulivu wa muda mrefu katika dunia hii. Imekuwa ikichochea

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

mapinduzi yasiyoisha. Jambo alilotakiwa kufanya mshairi ni kuangalia aina ya tatizo na kulitafutia ufumbuzi wake kwani si kila tatzizo linaweza kutatuliwa kwa njia ya kumwaga damu.

## MASWALI YANAYOHUSU USHAIRI

1. "Washairi ni Walimu*"* jadili kauli hii ukizingatia dhamira za vitabu viwii, kati ya *malenga wapya, Mashairi ya Chekacheka* na *Wasakatonge*
2. Waandishi *wa Malenga Wapya, Wasakatonge na Mashairi ya Chekacheka* wamefanikiwa kuielimisha jamii katika masuala ya siasa na uchumi. Jadili kauli hii ukizingatia vitabu viwili ulivyosoma.
3. Kwa kuzingatia dhamira za vitabu viwili kati *ya Wasakatonge, malenga wapya na Mashairi ya Chekacheka,* fafanua maan a ya ushairi na matumizi yake katika jamii.
4. *Linganisha mafanikio ya vitabu viwili kati ya wasakatonge na mashairi ya Chekacheka* na *Malenga wapya* kimaudhui
5. Jadiil uhalisi wwa dhamira za vitabu viwili katiya *Wasakatonge*, *malenga wapya* na *Mashairi* ya *Chekacheka*
6. Ujenzi wa taswira ni kipengele muhimu sana katika kuipamba lugha ya ushairi na kufikisha ujumbe kwa jamii. Jadili ukweli wa kauli hii kwa kuonesha taswira mbalimbali zinazojitokeza katika vitbu viwili kati ya *Malenga Wapya*, *Wasakatonge* na *Mashairi ya Chekacheka*
7. "Fani ni muhimu sana katika kuifanya kazi ya fasihi ikubalike kuwa kazi ya sanaa' chagua vitabu viwili kati ya *Wasakatonge*, *Malenga Wapya* na *Mashairi ya Chekacheka* ujadili vipengele muhimu vya kisanaa vinavyojenga kazi hizo
8. Fasihi hujengwa na fani na maudhui. Ijadili kauli hii ukitumia vitbu viwili kati ya *Malenga Wapya*, *Wasakatonge* na *Mashairi ya Chekacheka* huku ukizingatia matumiz ya lugha
9. Kwa kutumia washairi wawili jadili jinsi wanavyofanana na/au kutofautiana katika miundo ya mashairi yao
10. Chagua dhamira tatu zilizoshughulikiwa na washairi wawili kati ya T. Mvungi wa *Mashairi ya Chekacheka*, TAKILUKI wa *Malenga Wapya* na M.S. Khatib wa *Wasakatonge* kasha ueleze kufanikiwa au kutofanikiwa kwa washairi hao katika kuziibua dhamira hizo.
11. Ushairi wa Kiswahili kama tunzu nyingine za fasihi una kazi ya kuadiisha na kuelimisha jamii inayoandikiwa. Jadili usemi huu kwa kkutumia vitabu viwili kati ya na


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

12. Ujumbe wa *Malenga Wapya*, *Mashairi ya Chekacheka* na *Wasakatong*e una umuhimu mkubwa katika Tanzania ya Leo jadili kauli hii kwa kutumia vitabu viwili kati ya vilivyotajwa
13. Jadili kufaa au kutofaa kwa dhamira zillizoshughulikiwa na T.A. Mvungi wa *Mashairi ya Chekacheka,* TAKILUKI wa *Malenga Wapya* na M.S Khatib wa *Wasakatonge*
14. Aghalabu, washairi wawili kati ya TAKILUKI *wa Malenga Wapya*, Theobald Mvungi wa *Mashairi ya Chekacheka* na M.S. Khatib wa *Wasakatonge* wanavyozingatia kauli hii
15. Inasemekana kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa, lakini ya mkulima hathaminiwi. Jadili jinsi waandishi wa vitabu viwili vya mashairi kati ya *Wasakatonge*, *Mashairi ya Chekacheka* na *Malenga Wapya* wanavyolizungumzia suala hili
16. Eleza namna matumizi ya vipengele vya lugha yaliyoboresha au kufifisha diwani mbili kati ya *Mshairi ya Chekacheka, Malenga Wapya* na *Wasakatonge*
17. Miundo ya *mashairi ya Chekacheka*, *Wasakatonge* na *Malenga Wapya* ni tofauti chagua vitabu viwili kasha uelezee utofauti huo kama upo
18. "Mwanafasihi ni askari katika mapambano dhidi ya masuala kadha wa kadha yanayohusu jamii yake" Hakiki kauli hii ukihusisha vitabu viwili kati ya *Wasakatonge, Mashairi ya Chekacheka* na *Malenga Wapya.*
19. *Suala la ukombozi wa mwanamke ni suala ambalo limetiliwa mkazo sana hasa baada ya mkutano wa wanawake duniana uliofanyika mjini Beijing-China. Je washairi wnazungumziwa vipi. Chagua washairi mawili kati ya washairi wa Malenga Wapya, Wasakatonge na Mashairi ya Chekacheka?*
20. Fafanua jinsi waandishi wawili kati yaTAKILUKI, M.S Khatibna T. Mvungi walivyosaidia kujenga jamii mpya ya watanzania.
21. *"*Waandishi wa *Malenga Wapya, Wasakatonge* na *Mashairi ya Chekacheka* ni watatuzi wa matatizo ya jamii kwa vile wamegundua matatizo hayo na kuyatafutia utatuzi" Jadili kauli hiyo kuzingatia vitabu viwili kati ya vitatu ulivyosoma.

---

# UHAKIKI WA KAZI ZA FASIHI ANDISHI


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

MAANA YA KUHAKIKI

Kuhakiki kwa mujibu wa Njogo na Chimerah (1999) ni kupata hakika na ukweli wa jambo. Wanaoendelea kusema kuwa, uhakiki ni uchambuzi wenye kina wamepata kutumia tu ya baadhi mtaalamu wa fasihi wamepata kutumia istilahi kama vile kupembua kukosoa, kuvunjavunja n.k. Istilahi hizi zinazojaribu kueleza dhana ya uhakiki katika ulimwengu wa fasihi.

KUHAKIKI NI NINI SASA?

Kwa ujumla (kuhakiki ni kitendo cha kucHAmbua na kufafanua vipengele vya fani na maudhui katika kazi ya fasihi. Vipengele vya fani ni kama vile muundo, mtindo, wahusika, lugha na mandhari. Na vipengele vya kimaudhui ni kama dhamira , ujumbe falsafa, migogoro, itikadi na msimamo.

ZINGATIA

1. Kuhakiki ni kitendo cha kuchambua kazi ya fasihi na uhakiki ni ile hali ya kuchambua kazi ya fasihi.

2. Mtu anayetenda kitendo cha kuchambua kazi ya fasihi anaitwa mhakiki

3. Kitabukilichoandikwa na mhakiki ambapo ndani yake kuna uchambuzi wa kazi ya fasihi kinaitwa tahakiki.

4. Kuhakiki kunagusa / kubainisha vipengele vya fani na maudhui. Hivyo mtu anayetaka kuhakiki kazi za fasihi anapaswa kujua nadharia mbalimbali na istilahi zinazotumika katika fasihi.

MSINGI WA UHAKIKI WA KAZI ZA FASIHI

Kuhakiki kazi za fasihi ni taaluma inayopaswa kufuata taratibu na misingi ya kiuhakiki. Misingi inagusa maeneo matatu nayo ni,

(a) Mhakiki

(b) Kazi ya fasihi inayohakikiwa

(c) Mwandishi asilia na nhadhira iliyokusudiwa

(a) MHAKIKI

Mhakiki ni mtu anayechambua kazi ya fasihi. Si kila mtu anaweza kufanya kazi hii. Mtu anayepaswa kuwa mhakiki lazima awe na sifa zinazokubalika ili apate kufanya kazi hiyo kwa ubora.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

SIFA ZA MHAKIKI BORA

1. Awe anafahamu nadharia mbalimbali za kifasihi mhakiki anapaswa kujua kwa undani kuhusu fani fani na maudhui na vipengele vilivyomo katika kila kimoja.
2. Awe anafahamu vyema histoiria ya maisha ya mwandishi asilia wa kitabu hich. Na historia ya maisha ya jamii anayotoka na anayoiandikia.
3. Awe amesoma tahakiki za watu wengine waliochambua kazi anayotaka kuifanyia uhakiki. Hii itamsaidia kutoa tahakiki bora zaidi kwani atakuwa amejifunza yaliyo mazuri na kuepuka waliofanya wengine.
4. Asiwe mtu wa kuyumbishwa na maandishi au maneno ya wahakiki na watu wengine. Mahusiano ya mhakiki na waandishi yasiathiri uhakiki.
5. Awe na uwezo wa kutumia mkabala sahihi kulingana na kazi anayoifanya uhakiki. Mikabala humwongoza nhakiki kuchambua vyema kazi za fasihi.

DHIMA ZA MHAKIKI

Mhakiki wa kazi za fasihi anajua wazi kuwa kalamu ni chombo kinachoweza. Kuleta faida na hasara kwa jamii. Hivyo basi anatambua kuwa yeye anayodhamana kubwa itakayomwezesha mwandishi asilia kufikisha ujumbe kwa hadhira yake.

Mhakiki ana wajibu wa kuieleza hadhira juu ya watu waliolengwa na kazi hiyo ya fasihi. Mhakiki ni lazima aifahamu barabara jumuia ambayo mwandishi asilia aliandika juu yake aweze kufikisha ujumbe kwa hadhira yake.

Mhakiki anapaswa kuelewa historia ya watu ambao maandhishi yao yanayowahusu , bila kuifahamu historia yao, itakuwa vigumu kwake kueleza bayana ya mabo ambayo mwandishi asilia alimwandikia na kwa nini aliandika hivyo.

Ni wajibu wa mhakiki kuileza hadhira maandishi ya mwandishi ni kiwango gani? Maandishi ni sehemu ya utamaduni , na hakuna taifa linalopenda kuona utamaduni wake unamomonyolewa. Mhakiki huyapitia maandishi asilia na kujaribu kupembua bna kuchanganua kuwa ni kwa kiwango gani, maandishi hayo yanawazindua na kuwapevusha msomaji. Mhakiki huwasaidia wasomaji kuona baina ya maandishi yaliyo na somo kwa jamii na atawasaidia hasa iwapo yeye mwenyewe ni sehemu ya wale wanaopambana na kupigania haki zao. Mhakiki sharti aseme wazi , ayafichue maandishi ya namna hiyo. Mhakiki bora huijenga jamii ya kimawazo.

Mhakiki hodari hupiga vita uandishi wa lugha unaoleta sera mbovu za viongezi ambayo udikteta ni aina ya unyonyaji , maandishi yanaweza kuwa zana imara ya maguzi ya kweli. Mhakiki wapige vita waandishi asilia wanaowatetea wanasiasa wanaopiga kelele jukwaani lakini hawana vitendo. Hana budi kupigania ushindi wa demokrasia ya kweli.

Mhakiki ni lazima awaonye waandishis asilia wanaopenda kuandika habari za uongo, kuwa maandishi sipambo au kitu cha anasa , bali ni zana maalumu katika malezi na makuzi ya watu.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Mhakiki ni kiungo na ni rafiki wa waandishi asilia na wasomaji. Mhakiki anapaswa kujua na kuwanasa wasomaji kuwa uwezo wa kuchambua mambo ya kisayansi bila kutonesha hisia za wasomaji. Asiwe na majivuno bali awaheshimu anaowahakiki na anaotaka wasome uhakiki wake, yani mhakiki wa leo sharti aviangalie vitabu vya wanadhisi wetu na avichambue , aone kama vinahusu maisha yetu.

Mhakiki ana kazi muhimu ya kutoa ufafanuzi kuhusu vipengele kadhaa vya kisanaa kama vile matumizi ya tamathali za semi, ishara na taswira mbalimbali. Mbinu hizo zinaweza kumdanganya msomaji ambao hajapata utaalamu mkubwa kufichua ishara Fulani kwa vile mbuyu, jahazi , chewa na kisu katika kitabu cha “mashetani” (1971) ana msaidia msomaji kupata ujumbe kikamilifu.kazi ya fasihi inayohakikiwa

B) Kazi yoyote ya fasihi ni lazima iwe na fani na maudhui.

UHAKIKI WA FANI

Fani ni jumla ya mbinu , ufundi , mtindo wa vipengele vingine vinavyotumika kusawilisha maudhui . hivyo fani ni ufundi wa kisanaa anautumia msanii katika kazi yake.

Vipengele muhimu vinavyounda fani ni kama vile;

1. Muundo
2. Mtindo
3. Lugha
4. Wahusika
5. Mandhari

1. MUUNDO

Ni mpangilio wa visa na matukio katika kazi ya fasihi. Kwa ujumla , muundo hugusa mambo yafuatayo;

i. Umbo la kazi ya fasihi kama hadithi, tamthiliya au ushairi.

ii. Idadi ya sura , maonesho, mistari na beti.

a. Sura – mara nyingi huwa kwenye riwaya

b. Maonesho- hujitokeza kwenye tamthiliya

c. Mistari na beti kwenye ushairi kwa mfano;

Ubeti kuwa na mistari:-

- Moja – tamolitha
- Miwili- tamthnis
- Mitatu- tathilitha


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- Minne- tarbia
- Mifano – takhimisa
- Sita na kuendelea – salabia

iii. Msuko

Msuko wa visa na matukio huweza

a. Msago (moja kwa moja) – msuko sahihi

b. Urejeshi (kioo) kuvukia matukio

c. Changamano : urejeshi na msago

2. MTINDO

Ni namna mwandishi alivyotumia mbinu mbalimbali ili kubaini vionjo vya kazi na mwandishi mwenyewe kutokana na mazoea. Ni kiungo muhimu cha fani na maudhui mtindo huhusisha vipengele vifuatavyo;

a. Matumizi ya nafsi : hapa pana nafsi tatu

i. Nafsi ya I- mwandishi ndiye mjuvi wa matukio

ii. Ya II – watu wawili au zaidi wanajibizana

iii. Nafsi ya III- mtu wa tatu anatusimulia mimi na wewe

b. Matumizi ya tanzu nyingine ndani ya kazi ya fasihi kwa mfano , ndani ya hadithi kunaweza kuwa na nyimbo, barua , mchezo wa kuigiza n.k.

c. Mtindo wa utanzu huweza kuwa mtindo mono/majibizano (dayolojia) au masimulizi.

d. Uteuzi wa maneno

3. WAHUSIKA

Huwa ni viumbe hai , au si hai , ambao hutumika kuwakilisha matendo , mwenendo au tabia za kibinadamu wa kweli katika jamii. Viumbe hai ni wale wanaopatikana katika kazi ya fasihi. Mfano fisi anawezahusika katika kazi ya nafsi huyo huweza kuwakilisha binadamu wajinga na waroho.

WASIFU WA WAHUSIKA

Wasifu wa wahusika ni muonekano wa mhusika kimaumbile , kitabia , matendo na hulka zake zote ndani na nje ambazo humpambanua kwa udhati. Kwa ujumla , wasifu wa unaweza kuwekwa katika aina kuu mbili nazo.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

a. Wasifu wa nje wa mhusika

Huu hutokana na maumbile na muonekano wa nje wa mhusika

b. Wasifu wa ndani

Hujibainisha kwa kuangalia tabia na matendo ya wahusika.

- Wasifu wa wahusika kupatikana kwa kuangalia vitu vifuatavyo.

i. Majina yao

Wakati mwingine majina ya wahusika hubeba wasifu wao hususani, wahusika wa fasihi simulizi kwa mfano. Sungura , fisi , kobe , majivuno, n.k

ii. Kauli zao

Namna wanavyoongea na yale wanayoongea hutufanya wasomaji au wasikilizaji wa fasihi kuelewa wasifu wa wahusika.

iii. Matendo yao

Matendo atendayo mhusika humfanya msomaji ahukumu tabia na mwenendo wa mhusika . mathalani kupiga , kumpapasa , kukutana huweza mhusika huyo aonekane kama kiumbe kamili.

iv. Uhusika wao

Nafasi aliyopewa mhusika huweza kufanya wasomaji waweze kutoa hukumu juu ya wasifu wa mhusika kwa mfano kama mhusika anafanya kazi ya ukuli, tunategemea kuwa mtu huyo si msomi.

AINA ZA WAHUSIKA

Katika kazi ya fasihi kuna aina kuu tatu za wahusika kama ifuatavyo;

a) Wahusika wakuu

b) Wahusika wasaidizi

c) Wahusika wajenzi

a) WAHUSIKA WAKUU


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Hii ni aina ya wahusika , ambao huweza kubebeshwa wazo kuu lililomfanya mwandishi kuandika kitabu mhusika mkuu huyo mara nyingi hujitokeza kutoka mwanzo wa kitabu hadi mwisho wa kitabu. Kwa mujibu wa Njogou na Chimerah (1999) wanasema kuwa wahusika wakuu ndiyo nguzo ya kazi ya fasihi kwa wahusika hawa ndio wanaosheheni hadithi nzima.

b) WAHUSIKA WASAIDIZI

Hawa ni wahusika ambao hutumiwa ili kumsadidia msomaji aelewe zaidi kuhusu uhusika wa wahusika.

c) WAHUSIKA WAJENZI

Hawa ni wahusika ambao huibuka katika kazi ya fasihi kwa ajili ya kuibua dhamira Fulani. Kimsingi hutumika pia kujenga wahusika wakuu na wasaidizi . wahusika hawa hawajitokezi toka mwanzo hadi mwisho . mara nyingi wahusika huibuka na kutoweka baada ya kuibua dhamira au baada ya kuwajenga wahusika kadhaa.

MTAZAMO WA JUMLA KUHUSU UUMBAJI WA WAHUSIKA KATIKA KAZI ZA FASIHI.

Wahusika wakuu , wasaidizi na wadogo wanaweza kugawanywa katika makundi makuu matatu ambayo wao toka mwanzo hadi mwisho wa kazi ya fasihi. Makundi hayo ni kama vile;

a) Wahusika duara

b) Wahusika bapa

c) Wahusika shinda/foili

a) WAHUSIKA DUARA

Hawa ni wahusika ambao huumbwa wakiwa na tabia ya kubadilika. Ni wahusika ambao hushinda wakati Fulani katika maisha yao, lakini pia hukumbwa na anguko kutokana na kuwa na hulka za kibinadamu. Ni wahusika ambao huumbwa na sura zote mbili;

i. Ubaya na uzuri

ii. Wema na ubaya

iii. Ushindi na anguko n.k

b) WAHUSIKA BAPA

Wahusika bapa nia aina ya wahusika ambao wanajengwa na aina moja ya tabia na toka mwanzo hadi mwisho. Kama ni mbaya basi huwa mbaya mwanzo hadi mwisho na


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

kama ni nzuri huwa nzuri mwanzo hadi mwisho.wahusika hawa hata majina yao huweza kumtambulisha msomaji tabia ya mhusika huyo mfano.

i. Majivuno

ii. Mfalme jua

iii. Adili

iv. Shinda n.k

c) WAHUSIKA SHINDA/FOILI

Hawa ni wahusika ambao hawajitegemei kimawazo na huwa hawana msimamo, wahusika hawa huyumbishwa kwa urahisi na wahusika wengine kundi hili la wahusika ndio hutufanya tuelewe tabia na sifa za wahusika wengine.

4. MANDHARI/MAZINGIRA

Ni sehemu ambayo matukio ya hadithi au masimulixzi yanafanyika. Mandhari haya yanaweza kuwa ya kuubwa au halisi (ya kweli) katika fasihi mazingira yanaweza kuwa halisi au yakubuni (dhamira)

a) MANDHARI YA KUBUNI

Haya ni mandhari ambayo mwandishi ametumia tu, lakini katika hali halisi . mfano Shaaban Robert – riwaya ya kusadikika anatumia nchi inayoelea.

b) Mandhari halisi

Haya ni mazingira ya kweli ambayo yapo kweli na mwandishi huamua kutumia ili kuelezeana visa mbvalimbali . mfano ,Shaaban Robert –" Wasifu wa siti binti Saad" (1958)

5. MATUMIZI YA LUGHA

Lugha ndiyo nyenzo kuu ya fasihi. Ndiyo hutofautisha kazi ya fasihi na kazi isiyo ya kifasihi , lugha ndiyo huipambanua kazi ya fasihi na aina nyingine za kisanaa.

MAMBO YA KUZINGATIA WAKATI WA KUHAKIKI MATUMIZI YA LUGHA

a) Ufasaha / usanifu wa lugha

Mhakiki anapojaribu kutathimini ufasaha wa lugha,

Hujiuliza mswali yafuatayo.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Je lugh iliyotumika ni sanifu / fasaha? Kuna matumizi ya lahaja nyingine za lugha hiyo?

b) Matumizi ya semi

- Methali:

Ni aina ya semi ambayo ianweza kufafanishwa na kiungo na kitoweo cha lugha . hutumika kuyapima maisha, kufunzia jumuiya na kutawala jamii na mazingira ya binadamu.

Hutumika katika kazi ya fasihi daraja la kupitisha hekima .

Mfano : Ngo'mbe akivunjika mguu malishoni hujikokota zizini kusaidiwa- hii inaonyesha mvuto kati ya watawaliwa na wakoloni, haki na uhuru wao.

- Misemo na nahau

Matumizi ya misemo na nnahau katika kazi ya fasihi hushabiana sana na yale ya methali

Mfano ya nahau

- Amekula Chumvi nyingi- ameishi miaka mingi

- Kumwaga unga – kufukuzwa kazi

c) Matumizi ya tamathali za semi.

- Sitiari:

Inahusu ulinganishaji wa moja kwa moja kwa vitu aina havifanani bila kutumia viunganishi

i. Amina ni malaika aliyeumbika haswa

ii. Asha ni mwanaume , alifukuza wezi pia

- Tashibiha

Inahusu ulinganishaji wa vitu kwa kutumia viunganishi vya maneno kama vile : kama, mfano wa mithili ,

i. Amina ni kama malaika kwa urembo

ii. Asha ni kama mwanaume

- Tafsida


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Hii ni tamthiliya za semi inayohusu kupunguza ukali wa maneno.

Juma amekwenda kujisaidia badala ya kunya

Hivyo tafsida ni kujisaidia imeficha makali.

- Dhihaka

Ni utumiaji wa maneno yanayomchoma mtu kwa bezo linaloficha hisia za mdhihaki

Mfano,

Rais Bush alipomkamata sadam Husein akasema

“rafiki yangu . rais mtukuka , mfalme wetu nitakufanyia karamu leo hii kwa uhodari wako”

- Mubalagha

Ni uwekaji wa chuku katika kisa ili kuonyesha msisitizo wa kitu kinachosemwa . hivyo watu husema kuwa mubalagha ni utiaji chumvi katika msimulizi

Katika hadhira yangu , walishinda mabilioni ya watu.

- Tashihisi

Ni namna vitu visivyo na sifa walizonazo watu (binadamu hupewa hizo ) sifa hizo.

Mfano;

Miti yote shambani ilishangilia kwa kupiga makofi

Manyunyu ya mvua hatimaye yaliimba kilio cha furaha

- Kejeli

Hii imekusudiwa kuleta maana iliyo kinyume na ile iliyokusudiwa ama kinyume na ukweli ulivyo

Lengo ni kuzuia matatizo na migongano pindi itumikapo kwa lengo maalumu la kufundishia na kuasa.

Mheshimiwa Idi Amini Dada alikuwa rafiki mkubwa wa Rais Nyerere na ndivyo walivyokuwa waheshimiwa wote.

- Kijembe


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Huu ni usemi wa mzunguko, usemi wa kimafumbo na kumsema mtu kwa ubaya,

Mfano: hakika utazaa mtoto mwenye pua ndefu "maneno haya hakipewa mama mjazito ambaye ansasadikiwa kutembea na padri wa kitaliano.

- Lakabu

Tamathali hii inahusu uhusiano wa maneno kisarufi hugeuzwa na pengine kuwekwa kinyume na za kisarufi zilivyo.

Mfano. Mti wa umeme uliogonga uso wangu

- Taashira

Ni jina la sehemu ya kitu kimoja au la kitu kidogo kinachohusiana na kingine na kikubwa hutuwakilisha kitu kamili.

Mafano

- Kiti kilimkumbusha shahidi kuwa alikuwa aliyekwisha apa! (kiti hapa ni hakimu

- Kalamu ilishindwa kujibu maswali ya mtihani(kamau hapa ni mwanafunzi)

- Majazi

Hii ni aina ya sitiari ambayo itajapo sehemu ya kitu. Hapohapo sehemu hiyo huashiria kuweka kitu hicho

Mfano .

Dodoma iliishinda Kampala vita ya kagera (Tanzania ambayo mji mkuu wake ni Dodoma ilishinda vita kati Uganda na Tanzania ambayo mji mkuu wake ni Kampala.

- Maskini! Ajali ile ilipoteza roho tano hapo hapo(roho ni watu)

- Taniaba

Hii ni tamathali ambayo kwayo jina la mtu binafsi hutumiwa kwa watu wengine wenye tabia na mwenendo , hali au kazi na ya mtu huyo.

Mfano;

- Yuda wa kongo ni Jenerali Nkunda (yuda ni msaliti aliyemsaliti yesu)

- Katika dunia nzima kuna Ma-bush Marekani, Uingereza , Israeli na Afrika (bush alikuwa rais wa marekani aliyekuwa anapenda sana vita.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

- Msisitizo bayana

- Tulikubaliana kutokubaliana na kutoaminiana kwa manufaa yetu

- Ritifaa

Hii ni tamathali ambayo kwahayo mtu huzungumza na kitu au mtu ambaye husikiliza katika fikra kitu

Hii ni tamathali ambayo kwayo mtu huzungumza na kitu au mtu ambaye kusikiliza katika fikra kitu

- Ewe mwanangu juma , lala vema humo tumboni mwa mama yako Aisha. Napenda akuzae siku zako zikifika ili uje tuishi sote katika mtaa huo wa makanyagio hapa mkwawa.

- Tabaini

Huu ni usemi unasisitiza jambo kwa kutumia maneno ya ukinzani.

- Amekuwa mrefu si mrefu, mfupi si mfupi, wa kadiri

- Usimwamini mtu , anacheka machoni, rohoni ana mabaya.

- Nidaa

Huo ni msemo unaonesha kushangazwa kwa jambo Fulani. Msemo huu huambatana na alama ya kushangaa

Mfano!

- Zeituni mpenzi wangu! Ningekuwa na uwezo ningekuandalia harusi ya ndovu kumla mwanae!

- La! Hasha! Lahaula!

Mbinu nyingine za kisanaa

- Matumizi ya Onomatopea

Hizi ni tanakali sauti ambazo mwandishi huenesha mwigo wa sauti Fulani mbinu hutumika kuibua hisia.

Mfano

Paka akalia nyau! Nyau!


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- Takriri

Hii ni mbinu ya kurudia rudia maneno , silabi , mistari n.k

Cheza! Cheza! Cheza juma

- Mjalizo

Ni mbinu ambayo huwa na mfululizo wa matendo bila kuweka viunganishi

- Aliimba , alicheza , aliruka, n.k

- Mdokezo

Hii ni mbinu ya kuanza kueleza wazo lakini humalizii

Mfano,

- Alitaka ku……..kunanihi

- Niamini lakini…..

- Tashititi

Hii mbinu ya kisanaa ambayo mhusika huuliza swali ambalo jibu lake analifahamu

Sijaamini macho yangu . Dora ……Dora ….Niwwe kweli?

Mfano;

- Yuda wa kongo ni Jenerali Nkunda (yuda ni msaliti aliyemsaliti yesu)

- Katika dunia nzima kuna Ma-bush Marekani, Uingereza , Israeli na Afrika (bush alikuwa rais wa marekani aliyekuwa anapenda sana vita.

- Msisitizo bayana

- Tulikubaliana kutokubaliana na kutoaminiana kwa manufaa yetu

- Ritifaa

Hii ni tamathali ambayo kwahayo mtu huzungumza na kitu au mtu ambaye husikiliza katika fikra kitu

Hii ni tamathali ambayo kwayo mtu huzungumza na kitu au mtu ambaye kusikiliza katika fikra kitu

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- Ewe mwanangu juma , lala vema humo tumboni mwa mama yako Aisha. Napenda akuzae siku zako zikifika ili uje tuishi sote katika mtaa huo wa makanyagio hapa mkwawa.

- Tabaini

Huu ni usemi unasisitiza jambo kwa kutumia maneno ya ukinzani.

- Amekuwa mrefu si mrefu, mfupi si mfupi, wa kadiri

- usimwamini mtu , anacheka machoni, rohoni ana mabaya.

- Nidaa

Huo ni msemo unaonesha kushangazwa kwa jambo Fulani. Msemo huu huambatana na alama ya kushangaa

Mfano!

- Zeituni mpenzi wangu! Ningekuwa na uwezo

Ningekuandalia harusi ya ndovu kumla mwanae!

- La! Hasha! Lahaula!

e) Matumizi ya ucheshi

Ni mbinu ya kifani ambayo wasanii hutumia katika kazi zao za fasihi kuzichezesha hadhira zao au walau kuzifanya hizo zitabasamu.

f) Matumizi ya taswira au/ishara

Ni picha zinazojitokeza baada ya matumizi mbalimbali ya semi na ishara.

AINA ZA TASWIRA

1. Taswira za hisi

Hizi zina nguvu kubwa ya kuganda akilini na kunasihisa ujumbe wa mwandishi kwa wasikilizaji au wasomaji. Hizi hushughulikia hisi za ndani na huweza kumfanya msomi au msikilizaji, awe na wasiwasi, aone woga, apandwe na hasira , asikie kimya n.k

2. Taswira za mawazo/ kufikirika

Hizi zinatokana na mawazo, mawazo hayo ni yale yanahusu mambo yasiyoweza kuthibitika, mabo kama kifo , pendo , uchungu, fahamu, sahau na raha.


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

3. Taswira zionekanazo

Pia hizo hujengwa kwa kutumia vielelezo tunavyo, vinavyofahamiaka katika maisha ya kila siku.

Dakika haikupita , mijusi wawili walikuwa wamebebwa

walipita haraka, midomo yao ilikuwa myekundu,

Hafla walikutana na nyoka aliyeonekana mneene

Tumboni hapana shaka alikuwa amekula panya.

UHAKIKA WA MAUDHUI

Maudhui

Ni jumla ya mawazo yote ya mwandishi katika kazi ya fasihi. Maudhui hujumuisha dhamira msimamo, mtazamo , falsafa na ujumbe.

1. DHAMIRA

Hii ni wazo au mawazo makuu ambayo yametajitokeza katika kazi yu fasihi. Dhamira hugusa mambo yote katika maisha . hugusa uchumi siasa , utamaduni na shughuli zingine za kijamii kama vile elimu , afya.

AINA ZA DHAMIRA

Kuna aina kuu mbili za dhamira aina hizo ni;

a) Damira kuu

b) Dhamira ndogondogo

DHAMIRA KUU

Hii ni dhamira ambayo , kimsingi ndiyo hubeba dhamira nyingine, huweza kuwa.

Ujenzi wa jamii mpya ukombozi . ni wazo kuu moja ambalo kutokana na dhamira ndogondogo .

DHAMIRA NDOGONDOGO

Hizi ni dhamira mbalimbali ambazo zinatumika kujenga dhamira kuu. Dahmira hizi kuhusiana na dhamira kuu, kwani ndizo hujitokeza kama matatizo na masuluhisho ya


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

matatizo hayo. Hivyo dhamira kuu msingi hutokana na jumla ya dhamira hizi ndogondogo.

2. FALSAFA

Ni kipengele kimojawapo cha maudhui ambacho kinahusu mwelekeo wa imani ya mwandishi katika kazi ya fasihi kwa mfano. Shabani Robert aliongozwa na falsfa ya maisha kuwa binadamu tenda wema maishani.

3. UJUMBE / MAADILI

Ni funzo ambalo msomaji wa kazi ya fasihi hupata baada ya kung'amua dhamira zinazojitokeza katika kazi ya fasihi.

4. MTAZAMO

Huu ni msimamo ambao mwandishi wa kazi ya fasihi anakuwa nao anaposhughulikia matatizo mbalimbali kuna aina mbili za mtazamo.

a) Mtazamo wa kidhanifu

Mtazamo huu mara nyingi hutoa masuluhisho ambayo utekelezaji wake unakuwa mgumu katika hali halisi kwa mfano. Mapenzi bora ndiyo suluhisho la kila tatizo kuna matatizo ambayo hayahiraji mapenzi bora kama suluhisho.

b) Mtazamo ya kiyakinifu

Huu ni mtazamo wa kimapinduzi ambao huanisha matatizo na masuluhisho yanayoikabili jamii. Kwa mfano umoja na mshikamano, kujotoa mhanga kuona aina zote za dhuluma ni mfano ya masuluhisho yanayosababishwa na mfumo.

5. MGOGORO

Ni mivutano na misuguano m,balimbali katyika kazi ya fasihi. Katika kipengele cha mgogoro, tunapata migogoro kati ya wahusika , familia zao , matabaka yao. N.k. na migogoro hii mara nyingi hujikita katika mahusiano ya kijamii. Migogoro yaweza kuwa ya:

a) Kiuchumi – mfano riwaya ya Shinda (1975),

- Kasri ya mwinyi fuad(1975)

- Siku ya watenzi wote (1968)

- Utubora Mkulima (1968)n.k.

b) Kiutamaduni – kama tunavyoona katika riwaya ya


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

- Pepo ya mabwege (1981),

- Shinda (1984)

- Vuta n'kuvute(1999)n.k

c) Kisiasa – kama tuinavyo katika riwaya ya

- Ubeberu utashindwa (1971)

- Kinjekitile (1973)

- Mwanzo wa tufani(1976)

- Tone la mwisho (1981)n.k

d) Kinafsi a – itokeayo katika nafsi za wahusika , kwa mfano tunamwona "Rami" katika riwaya ya "Mzalendo" (1978) akikabiliwa na mgogoro wa kinafsia unaoupima uzalendo wake.



Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/